# Nipashe

Alhamisi Machi 12, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580177

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Waziri wa Afya azuiwa nyumbani baada ya kubainika kuugua corona

UKURASA 25




UKURASA 13

# Vigogo Chadema wakwepa kifungo

**Mdee**, Bulaya, Matiko walipiwa mil. 100/-, michango yavuka mil. 234/-, CCM yamlipia Mashinji... *Endelea ukurasa wa 2*



Halima Mdee



Ester Bulaya



Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole (kushoto), akitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, kumlipia fani ya Sh. milioni 30, mwanachama wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji. **Picha ndogo**: Mashinji akiwa kwenye gari baada ya kuachiwa huru katika Gereza la Segerea. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**MSAJILI AFUNGUKA TAARIFA KUVIFUTA VYAMA VYA SIASA**

NAIBU Msajili wa Vyama vya Siasa, Mohammed Ali Ahmed, amesema ofisi yake haina uwezo wa kufuta...

**UKURASA WA 3**

**OFISA MAGEREZA KORTINI TUHUMA ZA KUBAKA WANAFUNZI**

MKAGUZI mstaafu wa Magereza, Bernard Mlambala, mkazi wa Mtandi, Masasi mkoani Mtwara...

## MWANAFUNZI AJIFUNGUA MTOTO NA KUMTUPA CHOONI

UKURASA 3

# Sura bajeti ya tano ya Magufuli hii hapa



UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


**MICHEZO** YANGA YATAMBA ZAMU YA KMC KUCHEZEA LEO UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Vigogo Chadema wakwepa kifungo

**Na Wandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimefanikiwa kuchangisha kiasi cha Sh. milioni 234.469 na kufanikiwa kulipa Sh. milioni 100 kwa viongozi wake watatu kati ya wanane waliohukumiwa kifungo cha miezi mitano jela au kulipa faini ya zaidi ya Sh. milioni 350.

Juzi, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, ilitoa hukumu hiyo baada ya kuwatia hatiani kwa makosa 12 ya uchochezi.

Viongozi wa Chadema waliotiwa hatiani katika kesi hiyo ni Mwenyekiti, Freeman Mbowe, Katibu Mkuu John Mnyika, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu na wabunge Mchungaji Peter Msigwa, Halima Mdee, Esther Matiko, John Heche na Esther Bulaya.

Jana, uongozi wa Chadema ulifanikiwa kuwalipia Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha), Mdee Sh. milioni 40, Mbunge wa Tarime Mjini na Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Serengeti, Esther Matiko Sh. milioni 30 na Mbunge wa Bunda na Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Bulaya Sh. milioni 30.

Chadema ilifanya kampeni ya kuchangisha kwa simu na benki mara baada ya hukumu kutolewa juzi na hadi kufikia jana saa nane mchana, chama hicho kilikuwa kimepata Sh. 176,945,600 kwa simu, Sh. 52,743,780 kwa benki na fedha taslimu Sh. 4,000,780.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Mwenyekiti wa Chadema kwa sasa, Issa Mohamed, aliwashukuru waandishi wa habari kwa kulibeba suala hilo na kufikisha taarifa kwa viongozi na wanachama.

“Wananchi, wanachama na wapenda demokrasia wamekuwa na mwitikio mkubwa kwa kutoa kuanzia Sh. 500 kuendelea na mafanikio ni makubwa.

“Tayari tuna stakabadhi za kibenki tunasubiri mawakili wetu wameenda kuwatoa, tunategemea watafanikisha leo (jana) ili tusaidiane nao kuhakikisha fedha yote inapatikana tuwatoe wote waliobakia. Tunawataka wapenda maendeleo, tuzidishe bidii katika kuchanga ili watolewe wote,” alisema.

Miongoni mwa waliochanga ni Chama cha ACT-Wazalendo ambacho kimetoa Sh. milioni mbili.

Akizungumza kutoka Ubelgiji jana, Makamu Mwenyekiti wa Chadema Bara, Tundu Lissu, aliziomba jumuiya za kimataifa kuona jambo hilo kwa kuwa viongozi hao, akidai wamehukumiwa kwa makosa ya kisiasa.

**CCM WAMCHOMOA MASHINJI**

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji (sasa mwana CCM), jana alikamilisha amri ya hukumu iliyowaamuru na wenzake wanane, kwa kulipa faini ya Sh. milioni 30 na kuokoka kifungo cha miezi mitano jela.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Kiongozi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, aliiambia Nipashe kuwa Dk. Mashinji amelipa faini ya Sh. milioni 30.

“Mahakama imenitaarifu imepokea risiti ya malipo ya faini ya Dk. Mashinji kwa hiyo yuko huru, bado sijapokea taarifa za wafungwa wengine kuhusu kulipa faini hiyo.” alisema.

Jana, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, alisema chama hicho Mkoa wa Dar es Salaam, kimemsaidia kulipa faini mwanachama wao huyo mpya.

***Imeandikwa na Hellen Mwango na Enock Charles***

# Sura bajeti ya 5 ya JPM hadharani



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, akiwasilisha Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na ya kiwango na ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2020/2021, bungeni, jijini Dodoma jana. Kulia ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na (wa pili kulia) ni Spika Job Ndugai. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI inatarajia kukusanya na kutumia Sh. trilioni 34.88 katika mwaka ujao wa fedha, huku Sh. trilioni 21.98 zikitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zikiwamo gharama za Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Bajeti hiyo ya tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, imeongezeka kwa Sh. trilioni 1.7 kutoka Sh. trilioni 33.1 zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha.

Imeelezwa na serikali kuwa bajeti hiyo imezingatia mahitaji halisi ya ugharamiaji miradi mikubwa ya kimkakati, ulipaji mishahara, deni la serikali na vipaumbele vingine vya taifa.

Akiwasilisha kwa wabunge jijini Dodoma jana Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Kiwango na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema serikali imejipanga kikamilifu katika maandalizi ya uchaguzi huo ikijumuisha mahitaji ya kibajeti ili kuufanikisha.

“Kama mnavyofahamu, mwezi Oktoba mwaka huu, tutafanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani, tumejipanga vyema kibajeti, nichukue nafasi hii kuwasihi Watanzania wote washiriki uchaguzi huu muhimu na wazingatie umuhimu wa kuendelea kudumisha amani ya nchi yetu,” alisema.

Waziri huyo alisema kila anayehusika na uchaguzi huo, atekeleze wajibu wake kulingana na nafasi yake kuanzia viongozi wa madhehebu ya dini, wagombea wa nafasi mbalimbali, wapigakura, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), vyombo vya ulinzi na usalama, wasimamizi wa uchaguzi, vyombo vya habari na waangalizi wa kimataifa watakaokuwapo nchini wakati huo.

“Napenda kuwahakikishia Watanzania na jumuiya ya kimataifa kuwa uchaguzi utazingatia haki na utafanyika kwa usalama, amani na utulivu wa hali ya juu,” alisema.

**MAKADIRIO MAPATO**

Akizungumzia kiwango na ukomo wa bajeti hiyo, Dk. Mpango alisema kwa kuzingatia sera ya bajeti kwa mwaka 2020/21, kiasi cha Sh. trilioni 34.88 kinatarajiwa kukusanywa na kutumika.

Alifafanua kuwa kiwango hicho kinajumuisha mapato ya ndani ya Sh. trilioni 24.07 (sawa na asilimia 69 ya bajeti yote), mikopo ya ndani Sh. trilioni 4.9, mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara Sh. trilioni 3.04 na misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo Sh. trilioni 2.87 (asilimia 8.2).

“Kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 21.98 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 12.9 za matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 37 ya bajeti yote.

“Bajeti ya maendeleo inajumuisha Sh. trilioni 10.16 fedha za ndani, sawa na asilimia 78.8 ya bajeti ya maendeleo na Sh. trilioni 2.74 fedha za nje. Matumizi haya pia yanajumuisha gharama za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020,” alisema.

Alibainisha kuwa kwenye matumizi ya miradi ya maendeleo, Sh. bilioni 400 zitatumika kulipa madeni yaliyohakikiwa, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), Sh. trilioni 2.1, mradi wa umeme wa Julius Nyerere Sh. trilioni 1.6 na mingine ni Sh. trilioni 6.06.

**VIPAUMBELE**

Waziri Mpango alisema mapendekezo hayo yanatekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21.

Alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni pamoja na viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda.

Dk. Mpango alitaja kipaumbele kingine kuwa ni kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, akibainisha kuwa serikali inalenga kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, elimu na ujuzi na huduma za majisafi na salama.

Dk. Mpango alisema kipaumbele cha tatu ni uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji.

Dk. Mpango alisema kipaumbele cha nne ni kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango, akibainisha kuwa serikali itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na kuimarisha utawala bora katika usimamizi wa miradi ya maendeleo.

**DENI LA SERIKALI**

Waziri huyo pia alisema mwaka huu wa fedha, tayari serikali imetumia Sh. trilioni 5.80 kulipia Deni la Serikali lililotokana na mikopo iliyotumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema fedha hizo zimetumika kulipa mkopo huo kwenye mradi wa maji wa Arusha, Ruvu Chini, mradi wa kufua umeme wa Kinyerezi, mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kv 400 kutoka Singida - Arusha - Namanga na upanuzi wa Uwanja wa Ndege Zanzibar.

KUMBUKUMBU



*30/11/1929 - 12/03/2017*

**Mpendwa Mume wangu Clement George Kahama(Sweetie)**

Tangu ulipotwaliwa kutoka duniani March 12, 2017, Maisha hayajawahi kuwa rahisi bila uwepo wako. Uwepo wako na Joto la Upendo wako ni mambo ambayo tunayoyakosa tangu ulipotutoka.

Ndio maana tunaendelea daima kukumbuka familia yako inakukumbuka sana. Daima tunaiombea roho yako. Tunakupenda sana na Tunafurahia muda wote tulioishi pamoja.

***Mke wako, Janet Kahama na Familia.***

215663102

## HABARI KITAIFA

# Simulizi mwanafunzi kujifungua mtoto hatimaye kumtupa chooni

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Somsom iliyoko Kata ya Kibosho Magharibi, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro (jina linahifadhiwa), ameacha gumzo mitaani baada ya kumhadaa mjomba wake kwa tabasamu mita chache alipokuwa na kwenda kujifungua mtoto wa kike kisha kumtupa chooni.

Mwanafunzi huyo alijifungua salama bila usaidizi wa muuguzi wala mkunga saa 3:20 asubuhi jana akiwa nyumbani kwao, Kitongoji cha Mandeyeni, Kijiji cha Kifuni.

Tukio hilo linaacha utata kuhusu namna alivyokaa na ujauzito akiwa shuleni bila kugunduliwa na walimu wala wazazi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Salum Hamduni, alipoulizwa jana kwa njia ya simu kuhusu taarifa za kushikiliwa kwa mwanafunzi huyo na polisi, alisema amesikia jambo hilo na atalisemea baada ya kupata taarifa kamili.

"Nitatoa taarifa muda mfupi ujao, nasubiri taarifa kamili na hakuna tatizo umma utajulishwa kilichotokea," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kibosho Magharibi, Elisha Moses, alithibitisha jana mwanafunzi huyo kujifungua mtoto na kisha kumtupa chooni.

"Baada ya kupata taarifa, nilifanya ufuatiliaji kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kifuni, Felician Ollomi, na Mratibu wa Elimu wa Kata yetu (Edes Paul) na wakanihakikishia ni kweli mwanafunzi huyo aligunduliwa na mjomba wake aitwaye Faustine Massawe, akiwa anatoka chooni na alipombana aligundua kuna mtoto katupwa chooni, ndipo alipotoa taarifa na wananchi wakafika na kuvunja choo hicho.

"Baada ya kuvunja choo, walifanikiwa kukikotoa kichanga hicho kikiwa hai na kuwakimbiza mama na mtoto wake Kituo cha Afya cha Umbwe," alisema.

Tukio hilo limetokea zikiwa zimepita siku tisa, tangu wanaharakati wanawake wa Moshi waliojengewa uwezo na mradi wa nguvu ya pamoja ya kupambana na ukatili wa kijinsia unaoendeshwa na Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organization (Kwieco) kwa ufadhiliwa na Women Tanzania Fund (WFT) kuitisha mkutano wa hadhara na wananchi wa kata hiyo.

Aidha, Diwani wa Kata hiyo (CCM), Deo Mushi, alisema mwanafunzi huyo na mwanawe baaadye mchana walihamishiwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa kitabibu.

"Hivi tunavyongea mama na mtoto wako pale na wanaendelea vizuri. tumefuatilia shuleni mwanafunzi huyu hakukuwa na taarifa ya utoro, amekuwa akihudhuria shuleni isipokuwa siku tatu za mwisho, kabla ya tukio la kujifungua na kutupa mtoto chuoni," alisitiza Mushi.

Juni 23, mwaka jana, Rais John Magufuli alisema hakuna mwanafunzi yeyote wa kike wa shule ya msingi au sekondari atakayepata ujauzito kisha kuruhusiwa kuendelea na masomo, baada ya kujifungua katika uongozi wake.



Vijana wakisimamisha vyombo vya moto na kutoza Sh. 1,000, baada ya kujaza mchanga kwenye eneo la barabara iliyoharibiwa na mvua katika eneo la Tegeta A Goba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ofisa Magereza kortini tuhuma za kubaka wanafunzi

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

MKAGUZI mstaafu wa Magereza, Bernard Mlambala, mkazi wa Mtandi, Masasi mkoani Mtwara, amepandishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Masasi kwa tuhuma za kuwabaka wanafunzi watatu.

Mlambala (60) anadaiwa kuwa aliwabaka kwa pamoja wanafunzi wa shule za msingi wilayani hapa wenye umri kati ya miaka 10 na 12 (shule na majina yao yanahifadhiwa).

Ofisa huyo alifikishwa mahakamani hapo juzi na kusomewa mashtaka yanayomkabili kupitia kesi ya jinai Na. 26/2020.

Akisomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Batista Kashusha, Wakili wa Serikali Edwin John, alidai mahakamani hapo kuwa mtuhumiwa huyo anatuhumiwa kuwabaka kwa pamoja watoto watatu ambao ni wanafunzi ndani ya eneo la nyumba yake.

Wakili huyo alidai kuwa mtuhumiwa huyo anakabiliwa na makosa manne, matatu yakiwa ya ubakaji na moja la unyanyasaji wa kingono dhidi ya wanafunzi hao.

John alidai kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa la kwanza la ubakaji kwa kumbaka mtoto mwanafunzi mwenye umri wa miaka 12 kwa tarehe tofauti tofauti kati ya Agosti, 2018 na Januari, mwaka huu.

Wakili huyo aliendelea kudai kuwa mtuhumiwa alitenda kosa la pili la kumbaka binti wa miaka 10 kati ya Agosti, mwaka jana na Januari, mwaka huu.

Pia alidai kuwa mtuhumiwa alimbaka binti wa umri wa miaka 11 na kutekeleza kitendo hiko cha ubakaji katika tarehe tofouti tofauti kati ya Agosti, mwaka jana na Januari, mwaka huu.

Katika shtaka la nne, alidai kuwa mtuhumiwa alifanya unyanyasaji wa kingono kwa mabinti hao watatu kwa pamoja kwa nyakati tofauti tofauti alikuwa akikutana nao ndani ya nyumba yake eneo la Mtandi anakoishi kisha kuwalazimisha kumchezea uume wake kisha kuwabaka.

Mshtakiwa alikana tuhuma hizo na kupelekwa mahabusu hadi kesi hiyo itakapotajwa Machi 24, mwaka huu.

# Msajili asema anabanwa na sheria kufuta vyama

**Na Romana Mallya**

NAIBU Msajili wa Vyama vya Siasa, Mohammed Ali Ahmed, amesema kuwa ofisi yake haina uwezo wa kufuta chama chochote cha siasa kwa kipindi hiki.

Akizungumza jana katika mahojiano maalum yaliyofanywa na Televisheni ya ITV kupitia kipindi cha Konani, Ahmed alisema kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa kwa muda huu wa kuelekea Uchaguzi Mkuu Oktoba mwaka huu, Msajili hana mamlaka ya kufuta chama chochote.

"Kwa mujibu wa sheria, Msajili haruhusiwi kufuta chama na hii ni baada ya miezi 12 kabla ya uchaguzi, sheria inamzuia kufuta chama, anaweza kukisimamisha ili kurekebisha mapungufu yaliyoonekana na siyo kukifuta," alisema.

Mwishoni mwa wiki iliyopita Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi alitangaza kufanyika uhakiki wa vyama utakaohusisha vyama vyote vya siasa.

Aidha, alisema hadhani kama katika uhakiki huo kutakuwa na chama chenye matatizo kiasi hicho na kufikia hatua ya kushindwa kushiriki Uchaguzi Mkuu.

Alisema endapo chama chenye usajili wa kudumu ambavyo kwa sasa vipo 19, kikishindwa kushiriki uchaguzi matatizo hayatasababishwa na ofisi hiyo bali chama chenyewe.

Aidha, aliwataka wanasisasa watumie nafasi zao kushawishi wananchi kuwachagua au wawape nafasi ya kuongoza nchi badala ya kutumia muda mwingi kulalamika.

"Dunia siku zote haina huruma wapambane kwa mujibu wa haki na taratibu zilizopo na kufuata sheria, dunia ina misingi na taratibu zake, wazifuate ili kupata haki zao, watumie fursa hiyo," alisema.

Ahmed alisema (jana) juzi ofisi yake ilikutana makatibu wakuu wa vyama vya siasa kwa sababu baada ya kutangazwa hilo, hofu ilianza.

"Lengo la uhakiki tunataka kuona vyama vyote vimetulia na vimekaa kwenye mstari, tukianza uchaguzi watakuja waangalizi wa uchaguzi kutoka nje nao hupita kwenye vyama.

"Uhakiki ni kuwekana sawa kama tumekuta kasoro watapewa muda wa kujirekebisha, hofu yao inasababishwa na mitazamo ya kutokuaminiana. Tunafanya uhakiki ili visionekane vya mfukoni au ubabaishaji."

Kwa mujibu wa msajili huyo, mambo yatakayoangaliwa ni ofisi, mahesabu, usajili wa wanachama unaoeleweka na kadi za wanachama ziwe na picha zao.

"Kama kadi zilichukuliwa basi ziwe za wanachama siyo uonyeshwe zimechomwa moto hujui ni za wanachama au zimetengenezwa," alisema.

Alisema chama kisipokidhi hatua za awali wanazochukua ni kuwapa muda wa kujirekebisha na kikishindwa kinasimamishwa kushiriki mambo ya siasa na mwisho hufutwa.

Kuhusu hali ya kisiasa Ahmed alisema katika kipindi cha miaka mitano, imetulia na wakati wananchi wakishiriki maendeleo, serikali imepata ridhaa ya kuyaleta.

"Ukiona maendeleo yanaendelea katika nchi ujue siasa imetulia, vigezo tunavyoangalia ni vitu vinajieleza vyenyewe, wanasiasa wanaotaka kuhama au kurudi wanafanya hakuna mkwaruzano wala msuguano, hakuna kuuana wala msuguano," alisema.

Kuhusu hama hama ya wanachama, alisema ni ukomavu wa kisiasa na kukua kwa demokrasia kwa sababu wananchi wana uhuru wa wanachotaka ndicho wanachokifuata.

Kuhusu malalamiko ya baadhi ya wanasiasa dhidi ya ofisi hiyo kuwa inapendelea, alisema hawana upendeleo na kusisitiza hakuna chama cha siasa ambacho kitaachwa kwa kukiuka sheria.

"Kuhusu ACT-Wazalendo tuliwataka watoe maelezo kwa matukio yalitokea na tuliuliza kwa nini yametokea na hatuyaruhusu hayo, wametoa maelezo yao hakuna maamuzi yaliyotolewa bado msajili anayafanyia kazi," alisema.

# Kortini madai kubadili namba tambulishi za simu

**Na Hellen Mwango**

FUNDI simu, Said Khalifa (30), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, kujibu tuhuma za kula njama, kufuta na kubadili namba tambulishi za simu (IMEI namba) ya simu ya mkononi aina ya Tecno.

Mshtakiwa mwingine ni mfanyabiashara Abdul Nassoro (36), mkazi wa Chanika, jijini Dar es Salaam.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustina Mmbando.

Wakili wa Serikali, Ester Martin, alidai kuwa Februari 27, mwaka huu, mtaa wa Agrey, Kariakoo Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, walikula njama ya kubadili namba tambulishi za simu ya mkononi.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku ya tukio la kwanza washtakiwa wote kwa pamoja walibadilisha namba tambulishi ya simu ya mkononi aina ya Tecno.

Upande wa Jamhuri ulidai katika shtaka la tatu kuwa, siku na eneo la tukio la kwanza na la pili, washtakiwa kwa pamoja walijaribu kubadilisha namba tambulishi ya simu ya mkononi ili kuondoa namba halisi na kuweka ya kughushi.

Washtakiwa walikana mashtaka hayo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hakimu Mmbando aliwataka washtakiwa kuwa na wadhamini wawili watakaosaini hati ya dhamana ya Sh. milioni tano, mmoja awe na barua ya utambulisho wa taasisi inayotambulika.

Hata hivyo, washtakiwa walishindwa kutimiza masharti ya dhamana na kesi hiyo imepangwa kuja leo kwa ajili ya kusikiliza maombi ya dhamana.




Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara cha Vodacom, Arjun Dhillon (kushoto), akichangia mada kwenye mdahalo wa teknolojia ya kilimo, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu, uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, ambapo mkulima anaweza kupata taarifa mbalimbali za kilimo kupitia mtandao huo. Wengine ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa SAGCOT, Geofrey Kirenga (katikati) na Mshauri wa Sera za Kilimo, Prof. David Nyange. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ufaransa yawakumbuka waliokufa kwenye ugaidi

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imeyaomba mataifa yote ulimwenguni kuunganisha nguvu na kutoa kipaumbele katika kupambana na ugaidi unaoendelea kughrimu maisha ya watu na mali.

Akizungumza jana wakati wa maadhimisho ya 16 ya Ulaya na mara ya kwanza kwa Ufaransa, kuwakumbuka waliopoteza maisha kutokana na tukio la ugaidi lililotokea Madrid mwaka 2004 na kusababisha watu 193 kufa na 2,000 kujeruhiwa, yaliyofanyika nyumbani kwa Balozi wa Ufaransa nchini.

Hayo yamo kwenye hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Waziri, Dk. Damas Ndumbaro, ambayo alisema idadi ya waathirika wa ugaidi inazidi kuongezeka duniani kwa kundi linalotumia kivuli cha imani kuteketeza maisha ya wasio na hatia.

"Ni wajibu wa Serikali zetu kuwalinda na kuwahakikishia matukio haya hayaendelei. Ugaidi umegharimu maisha ya watu kuliko tishio jingine lolote na kila nchi imeguswa moja kwa moja au kupata athari za ugaidi," alisema.

"Ni lazima tutoe kipaumbele kwenye ushirikiano kimataifa katika mipango yetu ya nchi kupambana na ugaidi kwa kuwa hadi sasa hakuna mwenye jibu sahihi la changamoto zinazosababishwa na ugaidi. Nchi zinapaswa kuungana na kushirikisha sekta binafsi, vyama vya kijamii kukabiliana na kueleza changamoto," alisema.

Aidha, alisema Tanzania ilipata tukio la ugaidi mwaka 1998 kwa Ubalozi wa Marekani nchini kushambuliwa na kundi la al-Qaida na watu wengi walipoteza maisha na majeruhi.

Awali, Balozi wa Ufaransa nchini, Fredric Clavier, alisema ni muhimu kukumbuka changamoto zinazotokana na ugaidi, kwa aina zozote zile ambazo ugaidi unalenga kuharibu demokrasia, utamaduni, kuteketeza utambulisho, kuharibu familia na imani zao.

"Ufaransa inakataa kabisa ufashisti na inapinga hali ya siasa isiyo huria kukandamizwa juu yake, kama Ulaya inavyokataa, na nafahamu vile vile kuwa demokrasa ya Tanzania inakataa pia," alisema.

Balozi Clavier alisema tangu mwaka 2012, nchi hiyo imelipa gharama kubwa inayosababishwa na ugaidi kutokana na mashambulio kwenye miji ya Toulouse, Montauban, Paris, Saint-Denis na Nice kutokana na watu 258 kujeruhiwa.

"Ni lazima kuitambua aina mpya ya ugaidi na kwa umoja wetu tuchukue hatua licha ya ugumu na kutokuelewana, lazima demokrasia yetu ibaki imara dhidi ya hatari hii," alisisitiza.

Akisoma hotuba ya Rais wa taifa hilo, Emmanuel Macron, alisema ugaidi unataka kuligawa taifa na kuondoa thamani ya utu, lakini ndiyo wamezidi kuimarika na kuwa wamoja katika kupinga.

"Leo kwa jina la Ufaransa jina la kila mmoja, nitakuwa nikisimamia sherehe ya kwanza ya siku ya kitaifa hapa Paris, popote pale ambapo taifa litatikisika, kwenye ardhi yetu na kwa jamii za nje ya Ufaransa, ninataka kila raia kupata fursa ya kuhusika katika maadhimisho haya,"alisema katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Balozi.

Hafla hiyo ilikwenda sambamba na uwekaji wa mashada ya maua kwenye mnara wa kumbukumbu na nyimbo mbalimbali kutoka kwa wanafunzi.

## Serikali yasaka fedha usimamizi mazingira

**Na Waandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imesema itaendelea kutoa kipaumbele katika kutafuta rasilimali fedha za ndani na nje, ili kupanua wigo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuboresha uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, jijini Dodoma alipowasilisha taarifa ya ofisi yake kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na ofisi hiyo.

Alisema utekelezaji wa miradi katika ofisi yake umechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira, kuongeza usalama wa chakula, kuboresha hali ya uchumi kwa jamii, kupunguza uchafuzi wa mazingira na kulinda afya ya jamii.

"Umuhimu wa kuhifadhi mazingira unatokana na ukweli kwamba matumizi ya rasilimali za mazingira ndiyo msingi mkuu wa ukuaji wa uchumi wa nchi pamoja na maendeleo ya taifa, na jitihada za kuondoa umaskini nchini zinaendana na matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira," alisema.

Zungu aliongeza kuwa uharibifu wa mazingira nchini ni mkubwa, akitolea mfano kukithiri kwa matumizi ya kuni na mkaa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema ofisi yake imedhamiria kupunguza uharibifu wa mazingira nchini kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala.

"Nimeongea na kampuni za usambazaji wa nishati ya gesi hapa nchini ili kupunguza gharama za nishati, ili kila mwananchi aweze kunufaika nayo na kwa kuanzia, Kampuni ya Kopa wamekuja na teknolojia ya kuuza gesi kwa rejareja," alisema.

Akitoa ufafanuzi juu ya kukithiri kwa magugu maji katika Ziwa Victoria, Waziri Zungu alisema serikali inaangalia namna bora ya kuvuna magugu maji hayo ili kunusuru viumbe hai na bioanuai inayopatikana katika maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Murad Sadiq, aliishauri serikali kuweka mkazo katika usimamizi wa udhibiti wa kelele katika makazi ya watu.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Hawa Mwaifunga, alishauri serikali kuendelea kutoa elimu ya athari za matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo nchini.

Alisema suala la uhifadhi na usimamizi wa mazingira ni mtambuka, hivyo utekelezaji wake unahusisha sekta zote na jamii kwa ujumla.

## HABARI KITAIFA

# Watoto 46,000 Pwani wana udumavu

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKOA wa Pwani una watoto 194,433 wenye umri wa chini ya miaka mitano huku kati yao 46,275 sawa, asilimia 23.8, wakiwa na udumavu na wengine 17,304 ambao ni sawa na asilimia 8.9 wana uzito pungufu, imeelezwa.

Aidha, imebainishwa kuwa kati ya watoto hao 5,444 sawa na asilimia 2.8 wana uzito usiozidi na 112,771 ambayo ni asilimia 58 wana upungufu wa damu.

Hayo yalibainishwa juzi mjini Kibaha na Ofisa Lishe wa Mkoa wa Pwani, Pamela Meena, wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kilichofanyika mjini hapa.

Meena alisema watoto wote wenye utapiamlo katika mkoa ni 181,795 na kwamba watoto 12,683 wana hali nzuri ambao ni sawa na asilimia 6.5 ya watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano.

"Watoto wenye utapiamlo wasipopatiwa matibabu ya haraka watadumaa na hawafundishiki. Pia wakiwa watu wazima hawana nguvu za kutosha kufanya kazi na kuzalisha kwa wingi kama watu wasio na udumavu. Hali hii hairidhishi, hivyo hatua za haraka zinahitajika kuwa na kizazi chenye lishe bora," alisema Meena.

Aidha, alisema takwimu zinaonyesha kuwa wanawake wengi wenye umri wa kuzaa wana lishe duni, huku akibainisha kuwa 272,751 sawa na asilimia 43.1 wana uzito uliozidi, 327,175 (asilimia 51.7) wana upungufu wa damu na 54.564 wana ukondefu.

"Hali hii si nzuri kwani wanawake hawa wana hatari ya kupata watoto wenye uzito pungufu au ulemavu na wakati mwingine wanaweza wakazaliwa wakiwa njiti au mfu. Wazazi wanaweza pia kupata magonjwa yasiyoambukiza, kwa mantiki hiyo, hatua za haraka zinahitajika kupambana na hali hii," alisema.

Kutokana na hali duni ya lishe, alisema serikali ilitia saini mkataba wa lishe baina ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) na wakuu wa mikoa na utekezaji wake ulianza mwaka 2018.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alitoa wito kwa viongozi wa kata na halmashauri kuhamasisha lishe bora kwa wananchi ili kuepusha hali ya udumavu kwa watoto.



Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), Pius Maneno, akifungua mkutano wa Wiki ya Uhasibu Tanzania uliofanyika Mhasibu House, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Watoto kutoka Ethiopia wadaiwa kufanyishwa biashara haramu nchini

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

POLISI mkoani Arusha inawashikilia watoto sita, raia wa Ethiopia akiwamo mwenye umri wa miaka mitano, baada ya kukamatwa wakiwa wamehifadhiwa kwenye nyumba ya mtu binafsi eneo la Ngureso, jijini hapa.

Akizungumzia tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Jonathan Shanna, alisema watoto hao wenye umri wa miaka mitano hadi 12 waligundulika Februari 20, mwaka huu wakiwa nyumbani kwa Amina Ally na Mohammed Mahamudu, wote wakazi wa Ngusero.

Aisema polisi walipata taarifa kuwa nyumbani kwa Amina, kuna watoto wamefichwa na walikuwa hawajui lugha yoyote ya hapa nchini, ndipo walipovamia katika nyumba hiyo na kuwakuta watoto hao sita.

Aliwataja watoto hao kuwa ni Rukia Tajibu Ismail (12), Zainabu Tayibu (11), Kuruthumu Tayibu (10), Yimaji Tayibu (9), Arafat Tayibu (5) na Umayi Tayibu wote raia wa Ethiopia.

Kamanda Shana alisema baada ya kuwahoji watoto hao, walidai kutoroshwa kutoka nyumbani kwa mama yao nchini Ethiopia ili wapelekwe Afrika Kusini kwa baba yao, kupitia Nairobi nchini Kenya na kwamba waliingia nchini kupitia mpaka wa Namanga.

Wakati wanaendelea kuwahoji watoto hao alijitokeza mtu mmoja Ateyibo Isumail Yusuf (45), kutoka nchini Afrika Kusini akidai kwamba yeye ni baba wa watoto hao.

Hata hivyo polisi walimtilia shaka na kuamua kumshikilia katika kituo cha polisi baada ya kubaini kwamba hana kibali halali cha kuingia nchini.

Hata hivyo, Kamanda Shana alisema polisi wamechukua sampuli za vinasaba kwa watoto hao na mtu huyo anayedai ni baba wa watoto hao ili kujiridhisha kama kweli ni baba wa watoto hao.

Kwa mujibu wa Shana, polisi bado ina wasiwasi kuwa huenda watoto hao walikuwa wanasafirishwa kwa ajili ya kufanyiwa biashara ya haramu ya binadamu kupitia nchi ya Tanzania.

Kamanda Shana, alisema kwa sasa jeshi hilo linawasiliana na askari wa kimataifa (Inter Pol) kwa ajili ya kuwarejesha watoto hao nchini kwao Ethiopia na kwamba Isumail anayedai ni baba wa watoto hao, atafikishwa mahakamani kwa kosa la kuingia nchini bila kufuata sheria.

Watoto hao ambao walikamatwa Februari 20, mwaka huu, wanafikisha siku 19 wakiwa bado wanasota mahabusu jijini Arusha wakisubiri uchunguzi wa polisi.


**The Guardian Limited**

**JOB VACANCY**

**The Guardian Limited ,publisher of leading Tanzania newspapers, The Guardian and Nipashe, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

**CIRCULATION FIELD OFFICER – DAR ES SALAAM**

**Job Purpose:**

To boost copy sales and develop relationships with agents and vendors in the sales channel in the assigned area to meet your set sales targets.

**Main Responsibilities:**

The successful candidates will be responsible for the following key results:

- Work with the agents and vendors in making sure that the business grows and The Guardian Limited publications are available and visible and sold at the set retail prices with optimal return levels.
- Develop and grow more channels of distribution.
- Monitor indicators relating to market arrivals, circulation sales and returns indicators and make appropriate reports to Circulation Supervisor.
- Identify and build rapport with existing and potential customers by communicating the benefits of Selling The Guardian and Nipashe.
- Monitor newspaper distribution and sale trends in particular areas, prepare weekly sales plans and update supervisor on a regular basis.
- Monitor daily performance of TGL brands in your particular areas of operation in comparison to our rival publications and make reports that guide growth strategies.
- Open up new markets in particular areas of operation that will in turn translate into higher sales.
- Attend customer complaints that in one's particular area of operation so as to maintain good customer relations and protect the company's interests.
- Liaise with supervisor in credit control and debt management within particular area of operation.
- Submit daily and weekly reports on progress on activities, including meeting set sales targets.
- Manage debt collection and credit control within one's respective area operation.
- Demonstrate ability to work under minimum supervision.

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 2 year's relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge, and familiarity with a wide range of newspapers brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via HRO email address: ;**vacancy@guardian.co.tz** by March 13, 2020

NB: Only shortlisted candidates will be contacted.

***The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

615654302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Leteni sheria ya kukataza matumizi simu barabarani

**MADEREVA** wa vyombo vya moto kama magari ya shehena, mabasi na mengine makubwa kwa madogo, pamoja na pikipiki na bajaji wanatumia simu barabarani bila kujali maisha yao, ya abiria wanaowabeba na watumiaji wengine.

Ni kawaida kwenye barabara za Dar es Salaam na popote nchini, hakuna hofu hata mbele ya polisi wanaosimamia usalama, madereva huongea na simu tena wapo wanaochati bila kujali.

Abiria na wanaojali maisha mara nyingi wanajiuliza hivi sheria inachukuliaje tatizo hili ambalo lina mchango mkubwa kwenye ajali za barabarani?

Ni wazi kuwa katika dunia ya sasa ni vigumu wanadamu wakiwamo madereva kutomiliki simu ya mkononi hata asipoitumia akiwa barabarani.

Madereva wengi na hata wenye magari wanafahamu kuwa Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168, haijarekebishwa na kuweka kipengele kinachopiga marufuku matumizi ya simu wakati dereva anaendesha gari, hivyo wanafanya wanavyopenda na wapo pia wanaotumia 'head au ear phones ' masikioni na kuendesha gari bila kujali japo kwa mabasi ya abiria ni vigumu maana dereva anaendeshwa kwa sauti ya konda wa dala dala anayemwelekeza kwa makelele ya shusha au pandisha abiria.

Jambo la madereva kuwa 'wateja', waraibu au watumwa wa simu hili halipendezi. Licha ya kwamba wapo wengine wanaotizama video ndani ya gari wakiwa barabarani. Yote haya yanaongeza hatari zaidi kwa abiria.

Hatuilaumu serikali kwa sababu Sheria ya Usalama Barabarani ilitungwa mwaka 1973, licha ya kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara na ya mwisho yakifanyika mwaka 1996.

Kwa hiyo simu za mkononi zilikuwa hazijaanza kutumika nchini na hata kama zilikuwapo ni watu wachache waliokuwa wanazimiliki.

Hata hivyo, tunaona kuwa ni wakati wa watunga sheria kufanyakazi kiteknolojia na kuyaleta mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani yanayohusisha matumizi ya simu ya mkononi wakati wa kuendesha.

Tunaamini kuwa matumizi haya ya simu za mikononi kwa asilimia kubwa yanachangia ajali barabarani, licha ya kwamba polisi ndiyo wanaoweza kuthibitisha hilo.

Ni wazi kuwa kutumia simu wakati unaendesha chombo cha moto ni kuendesha kunakoweza kusababisha ajali hivyo ni hatari na ni wa kipuuzi au ni 'reckless driving.'

Ni dhahiri kuwa pengine polisi wakipima na kuthibitisha vyanzo vya ajali barabarani hawawezi kuona mara moja kuwa mhusika alikuwa anatumia simu, lakini watakubaliana nasi kuwa ipo haja ya kufanyika marekebisho na sheria ya usalama kukataza matumizi ya simu za mkononi barabarani.

Tunaishauri serikali itamke kisheria kuwa ni kosa la jinai kwa dereva kuongea na simu, au kuweka 'eye phones'maskioni, kujibu ujumbe au kutongoa (kuchati) huku akiendesha chombo cha moto, ni kosa la jinai na liwe na adhabu kubwa.


Aidha, tunaishauri serikali na wasimamia usalama barabarani kuona kuwa ni vyema iwekwe wazi kisheria kuwa dereva aegeshe pembeni tena eneo lenye usalama ndipo aongee na simu na si vinginevyo.

Tunaona kuwa huu ndiyo wakati wa kupata mwongozo wa kisheria kwa abiria ili kuwafumbua macho kuhusu usalama wao wanapoendeshwa na madereva wanaoongea na simu.

Tunashauri kuwa kama ambavyo Mamlaka ya Usafirishaji Nchi Kavu (Latra) inatangaza matangazo ya kuepusha ajali kwa kukemea mwendo kasi, wakati umefika kuwa na mipango ya kutangaza kuwa kuendesha daladala, basi la mkoani au basi la mwendo wa haraka wakati unaongea na simu ni hatari kwa maisha, hata kabla ya kurekebisha sheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Lifti malori kwa wanafunzi, tahadhari ni jambo muhimu

Na Yasmine Protace

**KUMEKUWAPO** na tabia kongwe na inayoendelea kujengeka kwa baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupanda malori yanayosafirisha mchanga, wakati wanafunzi hao wanaenda na kurudi shule.

Tunatamka hayo, huku tukijua kwamba suala la usafi kwa baadhi ya maeneo, imekuwa changamoto kubwa kwa wanafunzi, inapotokea wanapoamka asubuhi kwa safari ya kwenda shule na kuagana wanapomaliza masomo, shida kubwa kwao ni namna ya kufika wanakoelekea.

Mjumuiko wa fikra hizo zote, ndizo zinazozaa mustakabali kamili wa changamoto mbele yao wanafunzi. Kwa vipi? Mambo huanza pale wako katika sare rasmi na wanaomba lifti kwa baadhi ya magari ama wanapoenda au kutoka shule.

Ni kwamba, pale wanapotaka kupanda magari ya abiria kuelekea nyumbani au shule, baadhi ya magari hayo yanawakataa.

Hayo yanajitokeza, huku kwa baadhi ya wanafunzi shule zao ziko mbali zaidi na kuna changamoto ya kuwa mbali sana, hali inayosababisha usumbufu kwa wanafunzi.

Changamoto nyingine kwa watoto hao ni miundombinu yao kutokuwa mizuri, kunachangia wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shule na kurejea kwao. Hiyo, inatokana na maeneo hayo ya usafiri kutokuwapo wa uhakika.

Katika baadhi ya maeneo, wapo wazazi wanaotambua adha hiyo ya umbali kwa watoto wao hadi shule, baadhi ya wazazi wamewanunulia baiskeli wanafunzi, wazitumie kwenda shule na kurudi nyumbani.

Nianze kwa kuwashukuru hao wenye malori au magari ya kubeba mazao mashambani, kwa kuona changamoto ambazo zinawakuta wanafunzi na kuamua kuwabeba kwa safari zao za kimasomo.

Pamoja na wema huo wa kuwabeba wanafunzi, tunapaswa kwanza kijiuliza, je, usalama wao unakuwa unaangaliwa na nani wakati gari zinapokuwa zinaondoka?

Ni kawaida kuwakuta wanafunzi wamepanda malori nyuma na hakuna watu wa kuwaangalia. Wanafunzi hao wanarukaruka wakati gari linatembea. Je, ikitokea anaanguka chini na kudhurika, atalaumiwa nani?

> **Ni kawaida kuwakuta wanafunzi wamepanda malori nyuma na hakuna watu wa kuwaangalia. Wanafunzi hao wanarukaruka wakati gari linatembea. Je, ikitokea anaanguka chini na kudhurika, atalaumiwa nani?**

Watoto wana hulka ya kutotulia, kwa sababu hawana mtu wa kuwasimamia, gari linatembea wanafunzi wanaendelea na michezo ya kuruka huku gari linaendelea na safari.

Tena, unakuta gari hizo zinachukua wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Hapo inajenga swali lingine, nini kinachotakiwa kuangalia usalama wa watoto hawa?

Mara nyingi wanahitaji uangalizi muda wote na hata ikiangaliwa na wanaotumia usafiri wa shule, kuna watu maalumu wa waandaliwa kuwasimamia, mpaka wanapofika kwao.

Katika haya malori au gari, inawezekana wanafunzi wa sekondari wakawa wanajitambua, lakini hao wa shule ya msingi uelewa wa kufikia kujitambua kikamilifu, bado ni mdogo.

Kinachotakiwa ni kuwaangalia, maana chochote kikitokea, lawama mtazibeba nyie wenye magari hata kama mkijitolea kuwasaidia usafiri.

Niseme kwenu waendesha magari, mnapoyasimamisha, mhakikishe kuna mtu nyuma ambaye anawaangalia watoto ili wasije wakaanguka barabarani wakapoteza maisha.

Tunashukuru msaada ambao mnautoa kwa wanafunzi kwa kuwapatia lifti, lakini msaada huo baadaye unaweza kugeuka kesi mbaya.

## MJADALA

# Zanzibar tunahitaji mengi ya sukari, viungo vyetu tusonge

**Na Habib Miradji**

VISIWA vya Unguja na Pemba ni kitovu cha biashara toka karne ya 18 na wakazi wake wana vionjo vya utamaduni mtambuka, kutoka na historia yao.

Zanzibar kuitwa 'Spices Island' (Visiwa vinavyozalisha viungo) kama tangawizi, karafuu, hiliki, mdalasini, manjano, giligilani, pilipili manga na kadhalika, ni uthibitisho wakazi hawa ni wazalishaji wa muda mrefu

Pia, Zanzibar inazalisha matunda kama maembe machungwa, minazi mashokishoki, matufaa namastafeli yanayostawi visiwani humo.


Zanzibar imejaliwa rutuba ya kustawisha mazao ya kila aina, hata kuwa uchumi unaowafanya Wazanzibari kutembea kifua mbele wakitumia ardhi iliyowanufaisha wakazi kwa historia zao.

Mwasisi wa taifa la Zanzibar, Marehemu Abeid Amani Karume, alianzisha ulimaji miwa ili kuzalisha sukari na ndio sababu ya kuanzishwa kwa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda.

Mwenendo na mageuzi ya kiuchumi, ndio yalifanya kuna wakati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), ikabinafsisha na kuwaalika wanaoweza kuviendesha kufanya hivyo, ili kuzalisha bidhaa na ajira.

Kulikuwepo kipindi cha mpito cha kubadili teknolojia kwenye kiwanda hicho cha sukari cha Mahonda, hasa baada ya kubainika Zanzibar inatumia fedha nyingi kununua sukari kukidhi mahitaji makubwa ya sukari Visiwani humo .

Wafanyabiashara walipewa vibali ya kuingiza sukari, jambo lililosaidia, kushamiri magendo kutoka nje kwa madai sukari ya nje ni bei rahisi kuliko inayozalishwa nchini.




Iko katika kumbukumbu, serikali inayoongozwa na Rais Dk. John Magufuli na SMZ chini ya Rais Dk. Mohamed Ali Shein, ilivyosimama kidete kupiga vita magendo ya sukari.

Kuanza kufungua ukurasa mpya kwa wazalishaji wa ndani nao kushauriwa kuongeza tija ya uzalishaji wa sukari, ili kunusuru fedha za kigeni na kuzalisha ajira Hakuna hata nchi moja duniani imeweza kuendelea kutokana na uchuuzi wa bidhaa, bali uzalishaji bidhaa ndio msingi muhimu wa uchumi wa kisasa.

Hivyo, ni wajibu wa serikali, wawekezaji na wananchi kwa pamoja, kuhakikisha wanatumia rasilimali zao hasa malighafi za asili kuzalisha, kuliko kuuza mali hizo huku wakingojea uchuuzi

Visiwa vya Zanzibar havina tofauti na Madagascar, ambavyo vina rutuba nyingi na wana sera zinazofanana vya kuwasaidia wakulima na wawekezaji kuzalisha bidhaa na kuuza hadi nje.

Mathalani, Madagascar ni wazalishaji bora wa mpunga na miwa na wanajitosheleza kwa mahitaji yao na hatimaye kuuza nje ya nchi. Iweje Zanzibar wafikirie sera za uchuuzi zitajenga uchumi wake?

Wazanzibari wapo tayari kulima miwa. Ushuhuda wao ni tangu waliposaidiwa na mwekezaji kuzalisha miwa na wamekiri ni zao la biashara linalosaidia kupunguza umaskini. Hamu ya Wazanzibari sasa, ni kupatia ardhi zaidi ya kutosha kuchangia uzalishaji wa sukari.

Mbinu nyingine bora, ni SMZ ina nafasi ya kuwasaidia waliojikita kwenye kilimo cha miwa, kwa kuwaanzishia ushirika wa wazalishaji miwa, huku maofisa ugani, ushirika na masoko wakiwasaidia wakulima hao.

Nadharia ya sayansi ya uchumi, inasema uzalishaji ukiwa mkubwa, bei ya bidhaa inakuwa ya nafuu. Hivyo, Serikali ya SMZ iko katika wakati muafaka kuwapatia ardhi ya kutosha walima miwa ili waweze kuzalisha sukari ya kutosha.

Hakuna majibu ya mkato kwa uchumi wa Tanzania, zaidi ya kuwekeza nguvu kubwa katika kuzalisha na kushinda ulanguzi.

Wakulima wa miwa wanahitaji kuhamashishwa, kwa kupewa pembejeo na wataalamu wa kilimo waliobobea kwenye kilimo hicho. Wanahitaji maofisa ushirika wenye uwezo wa kuwaweka wakulima hao kuwa vikundi vya uzalishaji mali.

Pia, wawekezaji wa viwanda vya sukari wanapaswa kusaidiwa kupunguza gharama za uzalishaji, kupewa motisha na wakati mwingine kutafuta masoko.

Ukuaji uchumi na hasa wa viwandani unategemea uzalishaji bidhaa shambani. Naamini Rais Dk. Shein, ataandika historia kwa kuisaidia sekta hiyo kukua, kuputia kuwafanya Wazanzibari kupenda kujenga uchumi wao, kwa kushiriki uzalishaji na hasa wa kisasa wenye tija kwa mazao mengi katika eneo dogo, huku wakiendeleza teknolojia bora.

Zanzibar kinachotakiwa ni uthubutu wa viongozi. Licha ya kupitia awamu saba za utawala wake tangu iwe huru, badi kuna hitaji la wanachi kuwa na uthubutu kupiga hatua, zaidi ya mahali walipo, kwani uongozi bora upo mbele yao, ndani ya duara la SMZ na Serikali ya Muungano.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED





**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK (TZ) LTD** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa **MNADA WA HADHARA.**Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MMILIKI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ALLY ADDI OMARY | HEMED ABEID | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja na.585 Kitalu "44" Hati na.163002 , Eneo la Kijitonyama manispaa ya Kinondoni | 4/4/2020 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2.Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa,au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Equity Bank (Tz)Limited**
**Head Office,**
**Ohio street-Golden Jubilee Towers,**
**P.O. BOX 110183,**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE; + 255 768985500**
**Email: info@equitybank.co.ke**

215665702

# Mmiliki shamba mkonge hatarini kunyang'anywa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema serikali inakusudia kumnyang'anya mmiliki wa shamba la mkonge la Kwashemshi Sisal Estate lililopo kata ya Kwashemshi, Wilaya ya Korogwe, Mkoa wa Tanga kwa kusababisha migogoro kwa wakazi wa eneo hilo na kukiuka masharti ya uendelezaji.

Waziri Lukuvi ameyasema hayo wakati akizungumza na wakazi wa eneo hilo pamoja na wamiliki wa shamba hilo baada ya kukagua miundombinu ambayo imeonekana kuchakaa.

"Kwanza umekiuka masharti ya uendelezaji, kwa sababu umepewa shamba tangu mwaka 2003 na hadi leo ni miaka 17 hujalima lote wakati ulitakiwa uwe umemaliza kulilima mwaka 2011. Pili tunakudai kodi ya pango la ardhi hujalipa, tatu hujatoa ajira kwa wananchi na hujatoa gawio kwa halmashauri, sasa kwa nini nisimshawishi Rais afute hili shamba?" Alihoji Lukuvi.

Awali mkazi wa eneo hilo, Musa Majaliwa, alimlalamikia mwekezaji huyo kwa madai ya kumiliki shamba hilo lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 3,000 ambalo katika eneo lote ekari 300 pekee ndiyo zenye mkonge na sehemu nyingine ni vichaka.

"Tunachoomba Waziri Lukuvi utusaidie kupata sehemu ya ardhi hii kwa matumizi ya kilimo na makazi kwa kuwa ongezeko la watu limekuwa ni kubwa tofauti na hapo awali," alisema Musa.

Lukuvi alisema, shamba hilo lenye ukubwa wa ekari 3,703 linamilikiwa na Methew Upanga Mnkande na kwamba maendelezo yake hayaridhishi kwa kuwa hadi sasa eneo lenye mkonge wakuvuna ni ekari 1,210, eneo lenye mkonge mdogo, ekari 380 na kufanya eneo lililoendelezwa kuwa na ukubwa wa ekari 1,590 sawa na asilimia 42 pekee.

Pia mmiliki huyo tangu amilikishwe mwaka 2003 alikuwa hajalipa kodi ya pango la ardhi hadi sasa anadaiwa Sh. 14,218,000.

Kwa upande wake mwakilishi wa mwekezaji wa shamba hilo ambae anatambulika kwa jina la mzee Mkande, alidai kuwa shamba hilo limeendelezwa kwa kupanda mikonge mikubwa hekta 400 thamani na mkonge mdogo ambao unatarajiwa kuvunwa hivi karibuni ni hekta 150.

Kuhusu madai ya kodi ya pango la ardhi wanazodaiwa na serikali, mwakilishi huyo amekiri kuwa awali walikuwa hawalipi kodi, lakini wameingia makubaliano na wilaya kulipa na mpaka sasa wameshalipa Sh. milioni nane.

Hata hivyo, Lukuvi alimbana mwakilishi huyo kwa kumfahamisha kuwa shamba hilo lipo kwenye hatua za ubatilishaji kutokana na uvunjifu wa masharti ya kutoendeleza ipasavyo na kulipa kodi ya ardhi kwa kusuasua.



Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe (katikati), akikata utepe kuashiria kupokea msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 22 vilivyotolewa na Taasisi ya Doris Mollel, kwa ajili ya wodi ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti) katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni, jijini Tanga, juzi. Kulia kwake ni Mwanzilishi wa Taasisi ya hiyo na Balozi wa Watoto Njiti nchini, Doris Mollel. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mapitio sera ya viwanda yaanza

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WIZARA ya Viwanda na Biashara imeanza kufanya mapitio ya sera ya viwanda ili kupata sera mpya zitakazoendana na kasi ya mabadiliko ya kiuchumi duniani.

Pia hatua hiyo itasaidia kufikia Dira ya Taifa ya Uchumi wa kati ifikapo 2025.

Kauli hiyo ilitolewa na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mawasiliano, Utafiti wa Kukuza Biashara na Masoko (ADR), Frank Mmbando kutoka Wizara hiyo wakati akifungua mafunzo ya Watalaam kwa ajili ya kujifunza jinsi ya kufanya mapitio ya sera ya viwanda.

Alisema wizara hiyo inasimamia sera mbalimbali ikiwamo ya maendeleo ya viwanda, sera ya taifa ya biashara, sera na viwanda vidogo na biashara ndogo pamoja na sera ya mauzo ya kilimo, ambazo zimepitwa na wakati.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi huyo alisema mabadiliko ya kiuchumi ya kidunia yanaisukuma serikali kupitia wizara kufanya mapitio ya sera hizo ikiwamo ya maendeleo ya viwanda ambayo hadi sasa ni miaka 23, na kuwa inafikia ukomo mwaka 2020.

"Ni matarajio ya Serikali mtazingatia kwa makini mafunzo mtakayopata na kutumia ujuzi kwa kufanya marejeo ya sera zetu yatakayowezesha kuwa na sera sahihi kwa mahitaji ya sasa na baadae yatakayoendana na kasi ya mabadiliko ya kiuchumi, sayansi na teknolojia," alisema Kaimu Mkurugenzi Msaidizi huyo.

Alisema Tanzania inapoutazama mwaka 2025 ni lazima kurejea kwenye historia ya nchi ambayo imepitia vipindi mbalimbali vya historia ya kiuchumi kuanzia 1961 hadi 1967 ilipokuwa katika uchumi wa soko huria linalotegemea uagizaji wa bidhaa karibu zote za viwanda kutoka nje ya nchi.

Alivitaja vipindi vingine vya historia ni mwaka 1967 hadi 1986 ambapo kulikuwa na uchumi uliohodhiwa na serikali kwa misingi ya ujamaa na kujitegemea na kipindi cha miaka kumi kuanzia 1986 hadi 1995 ilitekeleza program za marekebisho ya uchumi.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (Unido) nchini, Dk. Stephen Kargbo, alisema wameamua kushikiana na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuiwezesha Wizara ya Viwanda kuandaa sera zitakazosaidia kufikia uchumi wa kati.

Alisema Unido imekuwa na ushirikiano na Sweden, ambayo imewezesha kutoa fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo watalaamu na vifaa ili waweze kushiriki kuandaa sera itayotekelezeka kwa mazingira ya Tanzania na inayoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani.

# Wafurahia kupungua kwa mauaji ya wazee

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

BARAZA la Wazee Mkoa wa Shinyanga limeipongeza serikali ya mkoa huo kwa kupunguza mauaji ya wazee na watu wenye ualbino, ambao walikuwa wakiuawa kwa sababu ya imani za kishirikina.

Wazee walitoa pongezi hizo jana kwenye kikao cha baraza hilo, wakati wakijadili changamoto mbalimbali zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi likiwamo suala la matibabu.

Akisoma taarifa ya utekelezaji, Katibu wa Baraza hilo, Anderson Lyimo, alisema wanaipongeza serikali ya mkoa kwa kupunguza mauaji ya wazee na watu wenye ualbino, ambayo yalikuwa yakiwanyima haki zao za kuishi.

"Tunampongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga (Zainab Telack) pamoja na watendaji wake kwa kudumisha amani, utulivu na usalama pamoja na kupunguza kwa kiasi kikubwa mauaji ya wazee na watu wenye ualbino, tofauti na miaka ya nyuma," alisema Lyimo.

"Tuanaendelea kuomba juhudi hizi za kutokomeza unyanyasaji, ukatili, mauaji ya wazee na watu wenye ualbino, ziendelee ili sisi wazee tupate kuishi kwa amani kwenye nchi yetu pamoja na serikali kuwachukulia hatua kali watu ambao wanasababisha mauaji ya watu ambao hawana hatia," aliongeza.

Lyimo pia aliiomba serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kutunga sheria ya wazee ili watekelezewe masuala yao kwa mujibu wa sheria.

Pamoja na mambo mengine wanataka sheria hiyo iweke bayana suala la upatikanaji wa dawa kwa wazee, madirisha, madaktari pamoja na vitambulisho vya matibabu bure ili waondokane na ukosefu wa matibabu.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, Lydia Kwesigabo, alisema mkoa wa Shinyanga una wazee 66,717 wakiwamo wanaume 29,917 na wanawake 36,800 na kwamba wazee wenye vitambulisho vya matibabu bure ni 20,068 na waliokatiwa bima ya Mfumo wa Afya ya Jamii (CHF) ni 4,231.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Nuru Mpuya, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye kikao hicho, alisema serikali itaendelea kutatua changamoto ambazo zinawakabili wazee likiwamo suala la matibabu.

HABARI KITAIFA

## Mil. 200/- kupandisha zahanati kuwa kituo

**Na Tiganya Vincent**

SERIKALI imetoa Sh. milioni 200 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kwa ajili ya ujenzi wa majengo katika Zahanati ya Tumbi ili iwe kituo cha afya.

Taarifa hiyo ilitolewa leo na Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, wakati wa ukaguzi wa utekelezaji wa shughuli za Malipo kwa Ufanisi (RBF) kwenye vituo na zahanati mbalimbali katika manispaa hiyo.

Alisema fedha zimeshapatikana na wako katika mchakato wa uundaji wa kamati mbalimbali ambazo zitasaidia kusimamia ujenzi wa majengo yanayopendekezwa.

Makungu aliongeza kuwa kukamilika kwa ujenzi huo utaiwezesha Manispaa ya Tabora kufikisha vituo viwili vya afya kikiwamo cha Maili Tano.

Alisema kwa sasa zahanati hiyo inahudumia watu 600 kwa mwezi, jambo ambalo linaonyesha kuwa kunahitaji kupandishwa hadhi ili kutoa huduma nyingi zaidi.

Aliwataka watu wote ambao watapewa jukumu la ujenzi wa majengo kuhakikisha kuwa wanasimamia kwa uadilifu na kuweka wazi matumizi na vifaa vyote vitakavyotumika ili itoe matokeo ambayo yanakusudiwa na serikali.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Zahanati hiyo, Regina Kimwaga, alisema wanalo eneo la ekari saba, ambazo zimepimwa na wanayo hati kwa ajili ya upanuzi wa huduma za afya.

**Aliwataka watu wote ambao watapewa jukumu la ujenzi wa majengo kuhakikisha kuwa wanasimamia kwa uadilifu na kuweka wazi matumizi na vifaa vyote vitakavyotumika ili itoe matokeo ambayo yanakusudiwa na serikali.**

# Wafugaji washauriwa kuzingatia ubora mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, amewataka wafugaji nchini kuzingatia ubora wa mifugo na sio wingi ili kupata mazao yenye kuwanufaisha kiuchumi.

Prof. Ole Gabriel, alitoa wito huo jijini Dodoma jana, wakati akiwakaribisha wawekezaji wa kampuni ya kuchakata na kusambaza nyama ya Tanfroz Limited inayomilikiwa na wawekezaji kutoka Ubelgiji na Ufaransa, walipofika ofisini kwake kujitambulisha.

Alisema kubadilika njia ya ufugaji kutoka wa uchungaji kwenda wa kisasa unaozingatia sayansi utamletea tija mfugaji na kunufaika kiuchumi.

Prof. Gabriel alisema azma ya serikali inasisitiza uchumi wa viwanda na haiwezi kufanikiwa bila kuboresha sekta ya mifugo, ambayo hutegemewa kwa malighafi za viwandani.

Katibu Mkuu huyo aliwaahidi kutoa ushirikiano na wataalamu wake katika hatua mbalimbali za kuanzisha mradi wa ufugaji, ambao utawanufaisha Watanzania.

Mradi huo umeanza kwa majaribio mkoani Iringa katika eneo la Mgagao ambako kuna shamba lenye ng'ombe zaidi ya 200.

Mkurugenzi wa kampuni ya Tanftoz Limited, Luc Battel, alisema Tanzania ina fursa kubwa ya uwekezaji katika sekta ya mifugo kutokana na wingi wake.

Alisisitiza kupata mifugo yenye ubora ni lazima kuwapo na utaratibu unaokubalika kitaifa na kimataifa.

Alisema kupitia mradi huo, Tanzania itafanikiwa kupata masoko ya nyama katika nchi za mashariki ya mbali na sehemu mbalimbali duniani.

Aidha, alisema uboreshaji wa mazao yatokanayo na mifugo kama nyama, maziwa na ngozi ni jambo muhimu kutumika kama malighafi.

Meneja wa kampuni ya CRV, Hielke Sportel, alisema kuwa ni vema wafugaji wakawa na ushirikiano katika kubadilishana habari na elimu mbalimbali za ufugaji bora wenye tija.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti nchini (TALIRI), Dk. Eligy Shirima, aliwashukuru wawekezaji hao kwa kutambua fursa mbalimbali zilizopo katika sekta ya mifugo na kuahidi kuwapa ushirikiano kila inapohitajika ili kuwainua wafugaji nchini.



Katapila la kampuni ya ujenzi ya Nyanza Road, likijaza udongo kwenye sehemu ya barabara iliyobomolewa na mvua katika eneo la Kitunda, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waaswa kusambaza picha za utupu mitandaoni

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WANACHUO wanaosoma Chuo cha Ufundi Stadi (Veta) mkoani Shinyanga, wameonywa kutoitumia vibaya mitandao ya kijamii, ikiwamo kuposti picha za utupu.

Wameelezwa kuwa kufanya hivyo ni kuharibu mfumo wa maisha yao ya baadaye, ikiwamo kukosa ajira pamoja na kufungwa jela mwaka mmoja au kulipa faini ya shilingi milioni tano.

Hadhari hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Ziwa, Francis Mihayo, alipokuwa akitoa elimu ya mtumiaji wa bidhaa za mawasiliano zikiwamo simu za mkononi kwa wanachuo wa Veta Shinyanga, katika kuelekea siku ya maadhimisho ya haki ya mtumiaji wa bidhaa za mawasiliano Machi 15, mwaka huu.

Alisema wameamua kutoa elimu hiyo kwa wanachuo hao wa kwa sababu vijana wengi wamekuwa wakitumia vibaya mitandao ya kijami kwa kuposti picha za utupu, bila ya kujua madhara yake ya baadaye watakapohitimu masomo yao.

"Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania katika kuelekea kilele cha maadhimisho ya siku ya mtumiaji wa bidhaa za mawasiliano mwaka huu, tumeona ni vyema kutoa elimu ya matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii kwa wanachuo hapa veta ili wabaki kuwa salama," alisema Mihayo.

Naye ofisa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano wa TCRA Kanda ya Ziwa, Walter Mariki, aliwataka wanachuo hao wakawe mabalozi wazuri kwa wenzao kwa kutoa elimu hiyo, huku akiwasihi kuwa wakipoteza simu watoe taarifa Polisi pamoja na kampuni ya simu husika.

Mmoja wa wanachuo hao, Rahma Jafari, alishukuru kupewa elimu hiyo hasa kwa kutumiana picha za utupu kwa kuwa hawakuwa na ufahamu.

HABARI KITAIFA

## Washauri adhabu ya kilimo shuleni ifutwe

**Na Daniel Limbe, CHATO**

SERIKALI imeombwa kuondoa adhabu ya kilimo shuleni ili kubadili mtazamo hasi kwa jamii, hatua itakayovutia uwekezaji wa vijana katika kilimo na kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Hatua hiyo inatokana na baadhi ya wananchi kuamini kuwa kilimo ni adhabu na siyo ajira hali ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikikwamisha mtazamo wa serikali wa kilimo kuwa uti wa mgongo wa taifa.

Mkurugenzi wa taasisi ya wasomi wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) wanaojihusisha na masuala ya kilimo nchini, Revocatus Kimario, amesema hayo jana(leo) mbele ya Naibu Waziri wa Maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Hussein Bashe, wakati wa kongamano la vijana wa mikoa ya Geita, Kagera na Shinyanga.

Alisema ili serikali iweze kufikia malengo ya kuwa na uchumi wa kati ifikapo 2025, hakuna ubishi kwamba kilimo ndiyo mkombozi mkuu na kwamba iwapo serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wataamua kubadili mtazamo hasi wa jamii hakika uzalishaji utaongezeka na kuinua uchumi wa taifa.

Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mhandisi Charles Kabeho, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandishi Robert Gabriel, aliwataka vijana kuongeza bidii katika kilimo na kwamba kupitia kongamano hilo anaamimi watabadili mtazamo wao na kuzalisha kwa tija badala ya kilimo cha kujikimu ambacho kimekuwa hakina mabadiliko ya kiuchumi kwa jamii.

Aidha, aliwataka kutumia fursa zilizopo kwa kuunda vikundi vinavyoweza kukopesheka kwenye taasisi mbalimbali za kifedha na halmashauri za wilaya hatua itakayowasaidia kuendesha kilimo, ufugaji na uvuvi wenye tija kwa manufaa ya sasa na baadaye.

Awali akifungua kongamano hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema kilimo kinapaswa kuheshimiwa sana kwa kuwa asilimia 70 ya mali ghafi zinazohitajika kwenye viwanda vinatokana na kilimo.

"Tunapaswa kubadili mtazamo wa jamii...na wanaopaswa kuanza ni sisi sekta ya kilimo kuhakikisha jamii inanufaika na kilimo kiuchumi... badala ya kuendelea na kilimo cha mazoea ambacho kimekuwa hakina mabadiliko kwa miaka nenda rudi," alisema.

Aidha, aliwapa matumaini mapya ya kufufuliwa kwa viwanda vitatu vya kuchambua pamba kwenye mikoa ya Geita na Shinyanga ambavyo vipo Chato, Kasamwa na Masumbwe, jambo alilosema litawasaidia wakulima kupata bei nzuri ya pamba yakiwamo malipo ya awamu ya pili.

# Madeni sugu ya bil. 1/- yaipeleka Saccos Takukuru

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SHIRIKA la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), limekabidhi orodha ya wadaiwa sugu wa Chama cha Kuweka na Kukopa cha Mipango na Majengo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma ili kuwafuatilia.

Shirika hilo limekabidhi orodha hiyo yenye madeni ya Sh.bilioni 1.8 ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, la kuitaka taasisi hiyo kufuatilia fedha hizo kama zinaviashiria vya rushwa ndani yake.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Takukuru mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema Takukuru imefanikiwa kurejesha Sh. milioni 101 na inaendelea kuwasaka wadaiwa sugu ili kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa.

"Tunawaomba wanachama ambao ni wadaiwa sugu wajitokeze kulipa kabla ya mkono wa sheria haujawafikia, la sivyo sheria itachukua mkondo wake," alisema Kibwengo.

Alisema mchanganuo wa madeni kwa Chama cha Mipango ni Sh. bilioni 1.6 za mipango na zilizosalia ni mali ya chama cha Majengo.

Alieleza kuna Saccos nyingine ambazo zinadaiwa fedha nyingi za wanachama, na kuwataka kuzirejesha haraka ili wengine wakope.

Akizungumzia rushwa ya ngono, Kibwengo alisema wanaendelea kutoa elimu katika shule za msingi sekondari na vyuo ili kudhibiti rushwa hiyo.

Alisema rushwa ya ngono bado ni tishio kwa wanafunzi wa kike, kutokana na wengi wao kutotoa taarifa kwa Taasisi hiyo.

"Tunaomba watu waache kuwaficha wahalifu ukitoa taarifa hakuna ambaye anaweza kukutangaza," alisema Kibwengo.

Alisema lengo lao ni kuona kila mmoja anakuwa huru kutoa taarifa kwa sababu suala la kupambana na rushwa ni la kila mmoja na sio Takukuru.



Mkuu wa Kitengo cha Polisi cha Afya Mkoa wa Iringa, Mrakibu wa Polisi, Apaililia Kibona (kulia), akisimamia zoezi la kuwapa chanjo ya kuzuia saratani ya shingo ya uzazi, wanafunzi wa Sekondari ya Kreluu iliyopo Iringa jana. Zoezi hilo la wiki moja litaendelea kwa wanafunzi wengine wa sekondari zilizopo Iringa mjini. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Wanawake watakiwa kuripoti matukio ukatili

**Na Friday Simbaya, MUFINDI**

WANAWAKE watakiwa kuripoti vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyofanywa na wanaume zao kwenye vyombo vya usalama na kuachana na tabia ya kumaliza mambo chini chini.

Akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa, Happiness Seneda, alisema upo utakili unaofanyika katika ndoa hasa wanawake kupigwa mpaka kuumizwa, lakini wanawake hao wanakaa kimya na kumaliza kesi hizo kwa maelewano.

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yalifanyika kimkoa katika Kijiji cha Utosi Kata ya Sadani wilayani Mufindi, kwa kuandaliwa na ofisi ya mkuu wa mkoa kwa kushirikiana na Shirika la SOS Children's Villages Tanzania.

Alisema baadhi ya wanawake ambao wapo kwenye ndoa wanakaa kimya wanapofanyiwa vitendo vya ukatili na wanaume zao ili kulinda ndoa na hatimaye kupata ulemavu wa kudumu.

Seneda waliwataka wanawake kuripoti mambo yote ya ukatili ambapo wengine wanakatwa mikono na wanaume zao, lakini kutokana na mila na desturi ya baadhi ya makabila, wanawake wengi wanaumizwa.

Alisema wapo wanaume wanashindwa kutunza familia zao kwa kutoacha fedha za matumizi halafu mwanaume anaporudi nyumbani anaanza kumpiga mwanamke kwa kudai chakula wakati hajaacha fedha za matumizi.

Mmoja ya wanawake waliohudhuria sherehe hizo, Damiana Mwihava, kutoka kikundi cha Twiivane Uyela, alisema amefurahia siku ya wanawake kwa vile amejifunza mambo yanayohusu haki za kinamama.

Alisema kuwa kupitia ufadhili wa SOS, kikundi chao kimeweza kufikiwa kwa kufanya mambo mengi ikiwamo kilimo cha nyanya na utengenezaji wa vikapu.

Naye Zainabu Nyakunga wa Kikundi cha Tuleane kutoka Kijiji cha Ukeremi Ikweha, wilayani Mufindi, alielezea kufurahishwa na maadhimisho hayo kwa kuwa wamejifunza athari za ukatili wa kijinsia lakini pamoja na mambo mengine ameweza kuleta bidhaa ya kikundi chao.

# Wanasiasa waaswa Siku ya Wanawake

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

VYAMA vya siasa nchini vimeombwa visigawanye wanawake kwa kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kivyama, sababu sio lengo la kuanzishwa siku hiyo.

Akizungumza jana jijini Arusha na waandishi wa habari, aliyekuwa Meya wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Kalisti Lazaro, alisema siku hiyo ilianzishwa ili kupinga unyanyasaji.

Alisema lakini ameshangazwa kuona baadhi ya vyama vya siasa hasa jijini Dar es Salaam wakijitenga na kuadhimisha siku hiyo kivyama, jambo ambalo sio sahihi wala sio lengo la kuanzisha siku hiyo.

"Mimi niwaombe wenzangu vyama vya siasa tusiwagawe wanawake kwa kuadhimisha kivyama bali tuwaunganishe pamoja ili tusipoteze lengo la kuanzishwa kwa siku hii," alisema.

Aliipongeza Halmashauri ya Jiji la Arusha kupitia Madeni na Daqarro, kuadhimisha siku hiyo kwa kuunganisha wananchi wa vyama vyote vya siasa.

Alisema kwa kukutanisha wanachama wote pamoja na kusherehekea siku hiyo kunajenga umoja na mshikamano.

"Lakini tunapojitenga na kuadhimisha kila chama kivyake tunasababisha mpasuko na kubaguana, jambo ambalo kwa maoni yangu tusiache mambo haya yaendelee ili tuwe wamoja," alisema.

**"Mimi niwaombe wenzangu vyama vya siasa tusiwagawe wanawake kwa kuadhimisha kivyama bali tuwaunganishe pamoja ili tusipoteze lengo la kuanzishwa kwa siku hii," alisema.**

# RC Gambo aagiza msako wa wahalifu

**Na Cynthia Mwilolezi, NGORONGORO**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amemwagiza Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, Ramadhani Kingai, kufanya uchunguzi dhidi ya mtandao wa kihalifu na kusababisha uvunjifu wa amani.

Gambo alitoa agizo hilo juzi ikiwa ni siku ya pili ya ziara yake wilayani Ngorongoro, baada ya kuwasili katika Kijiji cha Kisangiro kwa ajili ya mkutano wa hadhara na kupokelewa na mabango ya wananchi wakieleza kero ya mgogoro wa ardhi uliodumu miaka 21.

Mgogoro huo umesababisha vifo vya watu kadhaa na wengine kupata ulemavu wa kudumu.

"Uhamiaji fanyeni operesheni maalum katika eneo hili ikiwamo kuwakamata wahamiaji haramu 55 ambao tumepewa orodha ya majina yao hapa ambao siyo raia," alisema.

Alisema mgogoro wa Kijiji cha Kisangiro na Kijiji cha Naan umeendelea kwa muda mrefu na kuchochewa na ukabila, hali ambayo imesababisha baadhi ya wananchi wanajichukulia sheria mkononi.

Wananchi hao wamekuwa wakipora mashamba ya watu kwa kuwapiga, na wakati mwingine kutumia silaha za moto na kusababisha vifo, jambo ambalo alisema halikubaliki.

"Mambo yanayofanyika hapa hayafanani kabisa na nchi yetu na mimi kama kiongozi mkuu wa mkoa huu siwezi kuvumilia mambo hayo,"alisema na kuongeza:

"RCO shirikiana na OCD mfanye upelelezi wa kina muwakamate watu wote wanaohusika kuchochea migogoro kwenye vijiji hivi pamoja na kuwakamata watuhumiwa waliohusika kuchoma moto Kanisa la TAG na nyumba ya mchungaji wa kanisa hilo."

Awali wakazi wa Kijiji cha Kisangiro baada ya kukabidhi mabango yao kwa Gambo, walimwambia kuwa mgogoro huo unachochewa na baadhi ya viongozi wa serikali (hawakuwataja majina) na wafanyabiashara wakubwa wa Loliondo, ambao wanamiliki mashamba kwenye Kijiji cha Naan, hali inayowafanya wananchi wa Kijiji cha Naan kuvamia mashamba ya wakazi wa Kisangiro kila mwaka.

Ernest Ndibedi, alisema shambani lilivamiwa na kupigwa mwaka 2019 kisha shamba hilo kuporwa na baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Naan ambao pia walimkamata na kumpeleka polisi kisha kufunguliwa kesi kwenye baraza la ardhi la wilaya, ambayo inaendelea.

"Licha ya mimi kupigwa, kuna mwananchi mwenzetu Mhaki Elikana ambaye alipigwa na inasadikiwa kuwa aliuawa kwa sababu mpaka sasa hatujui alipo tangu mwaka 2014," alisema.

Richard Katungati alisema alivamiwa akiwa shambani kwake mwaka 2018 na kupigwa vibaya na wakazi wa Kijiji cha Naan na kumsababishia ulemavu wa kudumu, ambapo mtuhumiwa anafahamika, lakini hajakamatwa.



Watalii kutoka nchini Romania, wakinywa kahawa ya asili ya Tanzania, baada ya kufanya utalii wa kitamaduni ikiwamo ukulima wa kahawa na maisha ya asili ya Mtanzania katika Kituo cha Utalii wa Kitamaduni cha Moivaro, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Ndoa za utotoni kikwazo Longido

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

OFISA Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Grace Mghase, amesema mila kandamizi ndani ya jamii ya kifugaji, imesababisha wanawake kukosa haki zao za msingi kutokana na ndoa za utotoni.

Akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika juzi wilayani humo, alisema kwenye vituo vya afya wanawake wengi walio chini ya miaka 18 wana watoto wadogo.

"Kwa kweli ndoa za utotoni ni kikwazo katika wilaya hii na imekwamisha ndoto za wanawake wengi," alisema Mghase.

Alisema wanawake katika jamii hiyo wanabaguliwa katika utoaji wa maamuzi pamoja na kutoshirikishwa katika shughuli za maendeleo, hivyo aliwaomba wanawake mwaka huu wa uchaguzi mkuu, kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, ili wapate sehemu ya kusemea matatizo yao.

"Huu ni mwaka wa uchaguzi, msikubali kubaki nyuma kwa kuwa ndani ya jamii mnanyimwa nafasi njooni kwenye majukwaa, mpate nafasi ya kusemea haya yote yanayowakabili," alisema Mghase.

Aidha, alisema wanawake wameachiwa majukumu ya kifamilia na waume zao, hali ambayo imeleta mgawanyo wa majukumu, usiozingatia usawa japo serikali ikipigia kelele haki sawa kwa wote.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Juma Mhina, alisema kuanzia mwaka 2016 hadi 2019 halmashauri imetoa mikopo ya Sh. milioni 132 kwa vikundi vya kinamama, vijana na walemavu asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Dk. Mhina alisema kwa mwaka 2019 halmashauri ilitoa mkopo wa Sh. milioni 79 kwa vikundi saba vya kinamama vilivyosajiliwa na kujishughulisha na miradi ya kujenga uchumi.

"Kuna jumla ya vikundi vya kinamama 132, lakini hadi sasa ni vikundi saba ndio vimepata mkopo na mwezi Machi mwaka huu, tunatarajia kutoa mkopo zaidi ya Sh. milioni 100 kwenda kwa vikundi vya kinamama, hivyo changamkieni fursa hii mjikomboe kiuchumi na kuacha kunyanyasika kwenye familia zenu," alisema Dk. Mhina.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema siku chache zilizopita katika Kata ya Engikaret iliyopo Tarafa ya Longido, kuna mwanamke alifungwa kamba kwenye mti na kuchapwa viboko hadi kufa.

"Hakika jambo hili ni la kusikitisha sana katika jamii yetu...wanawake ni taifa kubwa na hata dunia inatambua, ndiyo maana ikatengwa siku muhimu ya kuadhimisha na kusherehekea siku yao, kemeeni ukatili ndani ya jamii," alisema Mwaisumbe.





# Wananchi wachanga kujenga jengo la wagonjwa

**Na Godfrey Mushi, SAME**

WANANCHI wa Kijiji cha Mtii katika Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, wameamua kuchangishana fedha kwa ajili ya kujenga jengo la wagonjwa wa nje (OPD) kwenye zahanati yao ili ipandishwe hadhi na kutoa huduma za dharura ndani ya saa 24.

Walisema kwa sababu zahanati hufanya kazi kwa saa 12 pekee, wanataka mamlaka husika zisaidie kukamilisha ndoto yao ili waweze kupata tiba kwa siku nzima na kuokoa maisha yao.

Jana wakizungumza kwa niaba ya wenzao kwenye viwanja vya zahanati hiyo wakati wa hafla fupi ya kupokea ufadhili wa Sh. milioni 25 zilizotolewa na Benki ya Posta (TPB) ili kukamilika ujenzi wa jengo hilo, Rahel Mbaga na Emmanuel Mghamba, walisema wananchi walipata wazo hilo baada ya kuibuka changamoto za baadhi yao kukosa tiba nyakati za usiku pale wanapouguliwa ama wajawazito kushikwa na uchungu.

Kwa mujibu wa Mbaga, baada ya kusoma mwongozo wa sera ya afya na kubaini kuwa zahanati haziruhusiwi kulaza wagonjwa, walihamasishana kila kaya kuchangia fedha ambazo zitajenga jengo hilo.

Mkuu wa Wiaya ya Same, Rosemary Senyamule, alipoulizwa na Nipashe kuhusu uamuzi wa wananchi hao, alisema serikali inawaunga mkono kwa hali na mali kutokana na juhudi za kujenga pia zahanati hiyo wakiishirikisha serikali ya wilaya na wafadhili katika hatua zote.

Kutokana na juhudi hiyo ya wananchi, Senyamule amemwagiza Mganga Mkuu wa Wilaya ya Same (DMO), kupeleka daktari atakayetoa huduma katika zahanati hiyo na kituo hicho kianze kazi mapema mwezi Aprili mwaka huu.

Awali, Meneja wa Benki ya TPB Kanda ya Kaskazini, Ayub Mkwawa, alisema waliguswa kusaidia juhudi hizo za wananchi hasa kutokana na umuhimu wa huduma za afya vijijini.

Aliwahakikishia kuwa serikali itahakikisha mchango wao unaenziwa kwa kituo hicho kuanza kazi, kwa kuwa wao ni taasisi ya serikali na kazi waliyoifanya ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

# Kilimanjaro chini kiwango ukusanyaji mapato ardhi

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wilium Lukuvi, amesema Mkoa wa Kilimanjaro uko chini ya asilimia 50 katika ukusanyaji mapato ya ardhi na umilikishaji ardhi kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, hali hiyo ndiyo inayochangia kukithiri kwa migogoro ya ardhi isiyoisha kwenye maeneo ya vijijini na mijini.

Alikuwa akizungumza jana na Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Wataalamu wa ardhi wa mkoa huo kuhusu mabadiliko ya kimfumo kutoka ngazi ya kanda kwenda kwenye mikoa.

Alisema zipo wilaya ambazo kwa mwaka mzima, hazijatoa hati miliki 100 jambo ambalo linashangaza na imekuwa likisababisha serikali kukosa mapato.

Waziri Lukuvi pia amepiga marufuku tabia ya wananchi wa mkoa huo kuondoka wilayani kwenda ofisi za ardhi mkoa kufuatilia hatimiliki zao.

Badala yake, amewaagiza makamishna wa ardhi kuwafuata wananchi hao kwenye wilaya zao husika.

Kutokana na kauli hiyo, baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Moshi, Michael Mwandezi na Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo kwa nyakati tofauti walieleza namna mpango huo utakavyosaidia kuondoa usumbufu kwa wananchi na kuwawezesha kupata hati miliki zao kwa urahisi bila kutumia gharama kama ilivyokuwa awali.

Mwezi Julai mwaka jana, Lukuvi alitangaza kusudio la wizara yake kuanzisha ofisi mpya za ardhi katika kila mikoa ili kuboresha utoaji huduma za ardhi nchini.

Alisema kutokana na mabadiliko hayo, huduma zote za ardhi zilizokuwa zikitolewa katika ofisi za ardhi za kanda, sasa zitatolewa mkoani na wananchi hawatahangaika tena kufuata hati au kusajili kiwanja katika ofisi za kanda.

Alifafanua kuwa katika kila mkoa kutakuwa na Mkuu wa idara ya ardhi wa mkoa, mpima na mthamini wa mkoa, lengo likiwa kuondoa kero kwa wananchi waliokuwa wakipata shida ya kwenda umbali mrefu kufuata huduma za ardhi.



Diwani wa Kata ya Kilimanjaro, Manispaa ya Moshi, Priscus Tarimo (wa pili kushoto waliokaa), akiwa pamoja na viongozi wengine wa kata hiyo, akizungumza na wanachama wa kikundi cha Vicoba cha kata hiyo, jana, ikiwa ni sehemu yao ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mghwira atamani wilaya ya Siha iwe kama Ulaya

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameanza 'kuipigia hesabu' Wilaya ya Siha akisema anatamani iwe moja ya miji ya mkoa huo anayotaka ifanane na majiji ya Ulaya katika suala zima la upandaji na ustawishaji wa miti kando kando ya barabara kuu.

Kutokana na ndoto hiyo, tayari ameagiza Halmashauri ya Wilaya ya Siha kutumia msimu huu wa mvua za masika, kupanda miti pembezoni mwa barabara kuu ya Sanya Juu hadi Elerai ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami ili kutunza mazingira ya barabara hiyo.

Alitoa agizo hilo jana, baada ya kwenda kukagua barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 32.2 iliyojengwa kwa kiwango cha lami na Kampuni ya Kimataifa ya China Geo Engineering (CGC).

Akiwa wilayani humo, Dk. Mghwira alisema, kazi ya Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) ni kujenga na kuzitunza barabara na kwamba jukumu hilo kwa upande wao wameshalitimiza.

"Lakini kwa upande wa mazingira ni jukumu la halmashauri kuotesha miti kando kando mwa barabara hii kuu inayounganisha nchi za Tanzania na Kenya, natamani sana Siha iwe kama majiji ya Ulaya yanavyopendeza kwa miti iliyopandwa kwa ustadi mkubwa.

"Sasa naagiza muanze mchakato huo kipindi hiki cha masika na mbebe wenyewe jukumu la kuitunza ili iweze kupendezesha mwonekano wa barabara hii na kuwawezesha wananchi kupata hewa safi kutoka kwenye miti hiyo."

"Miti itakapooteshwa pamoja na faida zingine itatunza mazingira na kupunguza vumbi pamoja na mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na upepo."

Akipokea maelekeza hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Ndaki Mhuli alisema, amepokea maelekezo hayo na anaahidi kuyatekeleza katika muda uliokusudiwa.

Mara kwa mara, Mghwira amekuwa akiagiza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) na Wakala wa Barabara (Tanroads), kuja na mwongozo wa kisheria utakaomaliza pia malalamiko ya wadau wa mazingira ya kupanda miti katikati ya eneo la barabara pacha na kisha miti hiyo kung'olewa.

Mpango huo wa kuifanya Siha kuwa ya kijani ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, inayotaka kuongeza eneo la upandaji miti kutoka hekta 60,000 mwaka 2015 hadi hekta 130,000 ifikapo mwaka 2020.

ama

ALHAMISI MACHI 12, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 20

**KITENDAWILI CHA CORONA SI MASIHARA BARA AFRIKA**



Ukurasa 16

Waziri Ummy na viongozi wa dini walipokaa kimkakati kujadili corona



Ukurasa 14

**Maisha kuwa 'bonge' yanamnyima ujauzito**



## AFYA MATATANI

# Kuendekeza zebaki kunavyoweka rehani uhai wa wachimba dhahabu wadogo

Ukurasa 18



Najda Khan. **PICHA: MTANDAO.**

# Maisha kuwa 'bonge' yanamnyima ujauzito

**Na Mwandishi Wetu**

NAJDA Khan (34), ni mwanamke ambaye amekuwa akiutafuta ujauzito kwa muda mrefu, bila ya mafanikio kutokana na uzito wake.

"Sijafanikiwa bado lakini sijakata tamaa nitaendelea kujaribu tena na tena" anasema Najda.

Mama huyo aliyeko katika ndoa ya pili, baada ya kukosa uzazi kwa mume wa kwanza kwa mwaka mmoja, akaamua kujaribu katika ndoa ya pili

Najda anaeleza tangu akiwa na umri wa miaka 18, alikuwa na usumbufu wa hedhi na alipowaona madaktari wa afya ya uzazi, alielezwa alikuwa na ugonjwa ujulikanao kama Polycystic Ovarian Sydrome.

Ni hali inayomsababishia Najda matatizo ya homoni na mojawapo ya athari za ugonjwa huo ni kuwa na uzito wa mwili usio wa kawaida, jambo ambalo hadi sasa anapigana nalo, japo hajafanikiwa.

Alipewa dawa ya kutuliza hali hiyo, Najda amekuwa akipata hedhi zake kila mwezi lakini hajaweza kupata ujauzito.

"Licha ya kuwa mimi sio mlaji wa chakula kingi sana, mwili wangu ni mnene kutokana na hitilafu za homoni mwilini. Daktari ananishauri nipunguze uzito niwe na uwezekano wa kupata ujauzito," anasema.

Ni miaka minne hivi sasa tangu akutane na mume wa sasa, lakini bado hajajaliwa kupata ujauzito, ingawa anaendelea kudumu kwa matumaini.

**BBC**

AFYA

# Kijiwe cha unyonyeshaji kazini kutekeleza umegeuka mtihani

## • Walimu Missenyi wafunguka 'wanavyosota'



Mratibu Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, Zainath Hassan (mbele), akizungumza na wanawake katika zahanati ya Ngando, wilayani Missenyi. **PICHA: LILIAN LUGAKINGIRA.**

**Na Lilian Lugakingira,** MISSENYI

KITAALAMU inaelezwa mtoto mwenye umri chini ya miezi sita, anapaswa kunyonya maziwa ya mama kila baada ya saa mbili, ili kujenga afya yake pasipo kupewa lishe nyingine.

Hata hivyo, katika uhalisia baadhi ya kinamama wanashindwa kuwanyonyesha watoto wao katika muda unaokubalika, hali iliyo hatari kwa afya ya watoto.

Waathirika zaidi ni waajiriwa, ambao baada ya mapumziko ya miezi mitatu ya kujifungua, wanahangaika kupanga mahali sahihi wanakoweza kunyonyeshea au kupumzisha watoto wao, ili waendelee na majukumu.

Emiliana Kasharu, ni mwalimu mwenye mtoto wa mwaka mmoja, analalamika kukosa chumba maalumu cha kunyonyeshea na analazimika kutumia mazingira jirani na shule anakofundisha, kupata faragha hiyo.

Mwalimu mwingine, Jaida Badru, mwenye mtoto wa umri mwaka mmoja na wiki tatu, anasema kila mara anapohitaji kunyonyesha, hutumia faragha ya maktaba ya shule anakofundisha.

> **"Hali hiyo inaathiri ukuaji wake, anapotimiza miezi minne anapaswa kukaa, lakini kama afya yake imeathirika anaweza asikae kwa umri huo.**

"Huwa naitumia maktaba muda wa mapumziko, na wakati mwingine huwa naomba kutumia chumba cha mwalimu mkuu endapo nikikosa namna," anaeleza.

Rai yake ni serikali itekeleze tamko la kutenga chumba cha kunyonyeshea katika ofisi za umma, ili kusaidia wanawake watumishi kunyonyesha watoto wao kwa wakati.

Anasema, kuna wakati wanashindwa kupata muda wa kuwanyonyesha watoto katika muda muafaka, akiongeza: "Lakini, tunajitahidi kukabiliana na hali hiyo ili watoto wetu waweze kufikisha umri wa miezi sita, waanze kuwagawiwa vyakula vingine."

**UAMUZI MISSENYI**

Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, sasa iko katika mpango wa kutenga chumba maalumu cha kuwawezesha watumishi wanaonyonyesha, kupata faragha ya kumnyonyeshea.

Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Hamis Abdallah, anaunga mkono kwamba inachangia kulinda afya za watoto na kupunguza udumavu wao, unaoanza na lishe duni.

"Umuhimu wa kuwapo kwa chumba hiki upo, lakini hadi sasa hakuna kinachofanyika, zaidi ya wazazi kukaa miezi mitatu nyumbani baada ya kujifungua na kurejea kazini," anasema.

Anasema, kisheria mtumishi anapaswa kuwapo kazini kati ya saa nane na tisa, lakini mnyonyeshaji anaruhusiwa kurudi nyumbani saa 6.30, ili akamhudumie mtoto.

Dk. Abdallah anasema baadhi ya wazazi wanatumia mbinu ya kuwaomba wasaidizi kuwaletea watoto kazini wawanyonyeshe, ingawa inajitokeza changamoto, kutokuwapo faragha cha kunyonyeshea.

"Tunayo majengo mengi. Tutaangalia kila litakalowezekana ili tupate chumba maalumu kwa ajili ya watumishi wanaonyonyesha. Hii itasaidia sana kujenga afya za watoto," anasema.

Dk. Abdallah anasema maziwa ya mama yanatumika kama chakula na maji kwa mtoto, maana ina virutubisho vyote muhimu na mtoto anapoyakosa, na hatari ya kudumaa mwili na akili.

Pia, inamzuia mtoto kutoka magonjwa nyemelezi, kama vile kuharisha, kutokana na ulaji vyakula visivyo salama na anafafanua:

"Hali hiyo inaathiri ukuaji wake, anapotimiza miezi minne anapaswa kukaa, lakini kama afya yake imeathirika anaweza asikae kwa umri huo."

Anatumia fursa hiyo kuwaasa waajiri kuzingatia sheria za kazi zinazowataka kuwapunguzia majukumu watumishi wanaonyonyesha, ili wapate muda wa kuwahudumia watoto wao.

Kuhusu kuhifadhi maziwa ya mama kwa ajili ya kuwanywesha watoto ambao hawajaanza kula vingine, Dk. Abdallah, anasema katika jokofu yanakaa kuanzia siku tatu hadi saba kulingana na yalivyohifadhiwa (usafi) na ubora wa jokofu, nje hayapaswi kuzidi saa moja.

Tahadhari yake, maziwa hayo hayachemshwi na Dk. Abdallah, anaeleza:"Maziwa ya mama yanayokuwa katika jokofu yanapaswa kupashwa joto kwa kufisha kifaa na kuweka maziwa kidogo, ambayo mtoto anaweza kunywa yakaisha, kisha kuweka kifaa hicho ndani ya kifaa chenye maji ya moto."

Anasema, wapo kinamama wanaotumia pampu kukamua maziwa ya mtoto, lakini watalaamu wanawakataza kwamba, wafanye hivyo inapolazimika.

Kwa mujibu wa Dk. Abdallah, mtoto mchanga anapaswa kunyonya kila baada ya saa mbili, akifafanua: "Ndani ya saa 24 mtoto angalau anyonye mara nane."

**PA KUNYOYESHA**

Shirika la Afya Duniani (WHO), lina mwongozo wa ulishaji watoto wachanga na wadogo na mtaalamu Idda anaunga mkono kwa misistizo kuwa, watoto kunyonya kwa mama peke yake katika miezi sita ya uhai wa kwanza, ni muhimu kwa ukuaji ubongo, mwili na mifumo iliyoko.

"Inachukua dakika kati ya 15

AFYA

# Kijiwe cha unyonyeshaji kazini kutekeleza umegeuka mtihani

mpaka 30 au zaidi kukamua maziwa ya mama," anasema Idda Katigula, mtaalamu wa afya na lishe, akifafanua Shirika la Kazi Duniani (ILO), linaloshauri mama kupatiwa dakika 30 za kukamua maziwa pamoja na saa za kupumzika.

ILO inabainisha chumba cha kunyonyesha kinapaswa kuwa na sifa: Chenye faragha: mwanga; mlango unaofunga na kiwe safi, kiti chenye ubora kwa mama aweze kukaa vizuri anaponyonyesha au kukamua maziwa.

Zingine kwa mujibu wa ILO, ni kuwapo jokofu kwa ajili ya kuhifadhia maziwa ya mama yaliyokamuliwa, kama mama anafanya kazi muda mrefu kabla ya kurudi nyumbani; kuwapo kabati dogo la kuhifadhia vifaa na meza ya kuweka vifaa wakati wa kukamua maziwa,

Aidha, inabidi kuwapo umeme kwa ajili ya mwanga, jokofu na baadhi ya mashine za kukamulia maziwa hutumia umeme, na sehemu ya kunawa mikono kwa maji yanayotiririka na sabuni, ili kuhakikisha mikono ya mama ni safi.



Kinamama wanaonyonyesha wakiwa katika zahanati. **PICHA ZOTE: LILIAN LUGAKINGIRA.**

**MTAALAMU UNYONYESHAJI**

Idda Katigula, mtaalamu lishe na mhamasishaji unyonyeshaji kwa wajawazito na wanaonyonyesha, anatumia ukurasa wake wa mitandao kuelimisha umma.

Anasema, maziwa ya mama pekee ni chakula bora kinachojitosheleza katika ukuaji mwili na ubongo wa mtoto mwenyc chini ya miezi sita tangu kuzaliwa, bila nyongeza ya vingine kama maji, uji na vyakula.

Idda anasifu Tanzania kupiga hatua katika unyonyeshaji maziwa ya mama na kuwapo haki za uzazi katika Sheria ya Kazi nchini (2004), lakini bado zipo changamoto za kunyoyesha maziwa ya mama pekee, miezi sita tangu kuzaliwa.

Mtaalamu huyo anasema wanawake wengi nchini baada ya likizo ya uzazi wanaporejea kazini, baadhi huanza kukamua maziwa kuhakikisha watoto wao wanaendelea kuyapata mpaka wanapotimiza umri miezi sita.

Anasema, kuhakikisha yanapatikana ya kutosha kwa mahitaji ya mtoto, inabidi mama ayakamue anapoenda mbali, iwepo akiba muda wote asiyokuwapo.

Ni aina ya tatizo analosema, inachukua nafasi zaidi kinamama wanaporejea kazini, kutokana na mazingira ya kazi kutokuwa rafiki pale wanapohitaji kunyonyesha au kukamua maziwa ya mama.

Idda analalamika, mazingira yasiyo rafiki katika maeneo ya umma, sehemu za kazi na biashara yanachangia kwa kiasi kikubwa wanawake kukata tamaa kunyonyesha maziwa ya mama pekee, wanaporejea kazini.

Anataja faida ya maziwa ya mama ni kwamba yanampatia

> **Jamii itambue kuwa maziwa ya mama yana maji kwa asilimia 88.1 ambayo mtoto anapata akinyonya, na anapata virutubisho vyote kwa uwiano sahihi.**

mtoto virutubisho muhimu kwa uwiano sahihi na ukuaji wake, huku akiwa na kinga madhubuti dhidi ya maradhi kwa mtoto.

"Maziwa ya mama pekee yanasaidia kuimarisha mfumo wa hewa pamoja na mfumo wa kumeng'enya chakula kwa mtoto, pia yanampatia mtoto Vitamini A na madini chuma kwa ajili ya kuimarisha kinga mwili, macho na mtoto kuwa na kiwango cha damu cha kutosha,"anaeleza na kudokeza kunyonyesha kunavyosaidia afya ya mwili wa mama na saikolojia.

Anataja athari za kutokuwapo chumba maalumu cha kunyonyeshea, ni kasi ya utendaji kazi inapungua, hata uzalishaji ya mama nayo yanapungua, kutokana na kuwepo msongo wa mawazo.

"Kinamama wengine wanabanwa na mazingira na kulazimika kuwapa watoto wao maziwa ya wanyama ambayo gharama yake ni kubwa, lakini wanafanya hivyo tayari wakijua watoto wanakosa virutubisho muhimu kutoka kwenye maziwa ya mama," anasema.

Anataja athari nyinginezo, ni mtoto kushambuliwa na magonjwa ya kila mara, hali inayosababisha tija ya utendaji kazi kwa mama inashuka, muda mrefu akiuguza hospitali na gharama za tiba zinaongezeka.

Idda anawashauri waajiri watambue, umuhimu wa kuwapo chumba maalumu kwa ajili ya unyonyeshaji kazini, kwani inawaathiri sana kinamama wanyonyeshaji, ikienda sambamba na kujali kumpa muda mama aliye mbali na mtoto wake.

"Sera za kampuni, mashirika zijumuishe sera inayolinda na kutambua umuhimu wa mama anayenyonyesha kupatiwa mazingira rafiki anapokuwa katika eneo la



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, Dk. Hamis Abdallah, akizungumza na wananchi (hawako pichani) katika zahanati ya Ngando, mkoani Kagera.

kazi," anashauri.

Idda anasema, elimu ya unyonyeshaji inapaswa kupewa kipaumbele katika maeneo ya kazi, ili kuwawezesha watumishi kutambua haki zao.

Anaona ni wakati kwa wadau lishe kushirikiana na serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, pia asasi zinazodhibiti lishe kuhakikisha jamii inapata elimu ya kutosha kuhusu unyonyeshaji.'

Hapo ni msisitizo wa matumizi ya vyombo vya habari, vipeperushi na mafunzo kazini kwa wataalamu na wahudumu wa afya katika ngazi zote.

Idda anasema, kinamama wengi wamekuwa wakilalamika kukosa uhuru na uamuzi katika malezi na wanapata wakati mgumu kuzingatia ushauri wanaopatiwa na wataalamu, kutokana na ushauri wa lazima wanaopata kutoka kwa ndugu wa karibu.

"Wengi wao hulazimisha watoto wachanga wapatiwe vimiminika kama maji, asali, uji mwepesi mara wanapozaliwa, kama walivyokuwa wakifanya wao walipojifungua miaka ya nyuma, wakiamini mama akifanya hivyo, mtoto anakata kiu, watoto watakua haraka na kuwa wanene, wakidhani unene ni afya," anasema.

Anasema, ni mambo yanayofanyika bila ya kumshirikisha mama mtoto na endapo akionekana kutokuridhia na anachoshauriwa, wanaweza kuanza kumshambulia, hali inayomuumiza kisaikolojia.

Kwa mujibu wa Idda, mama anapopata mtoto wa kwanza, mengi yanayomhusu mtoto yanakuwa mapya, hata kama amepata elimu, anahitaji watu wa karibu kumtia moyo.

"Jamii itambue kuwa maziwa ya mama yana maji kwa asilimia 88.1 ambayo mtoto anapata akinyonya, na anapata virutubisho vyote kwa uwiano sahihi," anasema Idda.

AFYA

# Waziri Ummy na viongozi wa dini walipokaa kimkakati kujadili corona

## • Awapa darasa, kisha awatoa hofu • Alipowaomba ubia, wasema 'sawa'



Viongozi wa dini wakiomba, kabla ya kuanza kikao chao na Waziri, Ummy Mwalimu. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

DUNIA sasa inaendelea kuteswa na virusi hatari vya corona na Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema kumepotezwa maisha ya zaidi ya watu 3,400 huku jitihada mbalimbali zikiendelea kwa ajili ya kuvidhibiti.

Nchini, serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kuhakikisha Watanzania wanabaki salama dhidi ya virusi hivyo, vilivyogundulika kwa mara ya kwanza nchini China, ingawa huko kunaelezwa kasi ya maambukizi yanazidi kupungua.

Katika mkutano na viongozi wa dini kuhusu kukabiliana na ugonjwa wa ebola, virusi vya corona nchini, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jámii, Jinsia, Wazee, na Watoto, Ummy Mwalimu, anawahimiza kushirikiana na serikali katika vita kukabili virusi vya corona, kwa kuelimisha jamii kujua jinsi inavyoambukiza, namna ya kujikinga.

Anawaeleza: "Serikali haijalala na inaendelea na jitihada kukabiliana na tishio la ugonjwa huo kwa kila njia."

Waziri Ummy anasema tayari serikali imeshaweka wataalamu wa afya na vifaa katika maeneo yote muhimu, ikiwamo mipakani, bandarini na viwanja vya ndege, ili kuhakikisha abiria wanaoingia nchini wanapimwa afya zao.

### VIONGOZI DINI

Viongozi wa dini mkutanoni wanaishauri serikali, pia kuomba mambo kadhaa yafanyike, ili waweze kuwa na mchango wa kutosha kuwasaidia waumini kujikinga na ugonjwa huo.

> Pamoja na hayo, ni muhimu kuepuka kugusana na mgonjwa m wenye dalili za magonjwa ya njia hewa, kuzingatia usafi binafsi ikiwamo kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka.



Waziri Ummy Mwalimu, alipozungumza na viongozi wa dini.

Nchini Korea Kusini, hivi karibuni iliripotiwa kasi kubwa ya coroma uambukizaji wake ulianzia kanisani, hata kiongozi mkuu wa kiimani, wiki iliyopita aliamua kuitisha mkutano wa waandishi wa habari kuiomba radhi umma.

Katika mkutano wa jijini Dar es Salaam, Sheikh Twahir Amran, kutoka Misenyi mkoani Kagera, anasema viongozi wa dini wako tayari kushiriki kuelimisha waumini wao na jamii kuhusu madhara ya virusi vya corona.

"Ombi na ushauri wangu ni kwamba, serikali iangalie uwezekano wa kutenga fungu za fedha kwa viongozi wa dini, ili wawe na muda wa ziada kuelimisha waumini kuliko kusubiri siku za ibada tu," anasema Amran.

Anafafanua:"Kutegemea siku za ibada tu hazitoshi, ni lazima tuwe na siku nyingine za ziada za kuelimisha, lakini hili linaweza kufanikiwa kama tutatengewa fungu la fedha kwa ajili ya kazi hiyo kwa hizo siku za ziada."

Mchungaji Benjamin Kissanga wa Kanisa Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Pemba, anasema viongozi wa dini wanahitaji elimu ya kutosha kwanza kuhusu ugonjwa huo, kabla nao hawajaanza kuwajibikia .

"Tukielimishwa vya kutosha, itakuwa rahisi kuwapa elimu waumini na jamii kwa ujumla, kwani bado yapo mambo mengi ambayo bado hatujayajua kuhusu hivi virusi vya corona," anasema Kissanga.

Mchungaji huyo anatoa matazamo katika suala la mavazi kuanzia kofia za abiria kwenye usafiri wa bodaboda, ambazo zinatumiwa na abiria wengi na anahoji kama zinaweza kuambukiza virusi vya corona au la.

Viongozi hao, ambao ni wa Ushirika wa Dini na Taasisi za Kidini (Tanzania Interfaith Partnership), walikuwa na mkutano wao jijini Dar es Salaam na kumwalika waziri huyo kuzungumza nao.

Ummy anasema, elimu hiyo ni watu kutopeana mikono, kutokumbatiana, pia kunawa kwa sababu kama njia mojawapo ya kusaidia kuwa salama zaidi na hata wakikumbwa na ugonjwa, wajue jinsi ya kupata matibabu.

"Takwimu za leo za WHO zinaonyesha kuwa idadi ya watu 90,870 wameambukizwa virusi hivyo, pia 3,112 wamefariki dunia na sasa ugonjwa sasa upo katika nchi 72," anasema Ummy.

### KWA NINI WAO?

Waziri Ummy anasema, viongozi wa dini wana ushawishi mkubwa katika jamii na kwa waumini wao kwa ujumla, hivyo anaamini wana mchango wa kuwahamasisha wakazingatia kile kinachoelekezwa kuhusu corona.

"Kwa kutambua umuhimu na mchango mkubwa wa viongozi wa dini katika sekta ya afya hususan kuelimisha jamii na kulinda afya za Watanzania, wizara yangu imeona kuna umuhimu wa kuwashirikisha," anasema.

Katika mkutano wake na viongozi hao, anasema matarajio ya serikali ni kwamba kupitia uelewa wa pamoja, serikali itaendelea kutoa mafunzo katika jamii ijikinge na kuepuka magonjwa hatari ya mlipuko.

"Nchi yetu kama zilivyo nchi nyingine za Afrika na duniani kwa ujumla, imekuwa ikikabiliwa na tishio la magonjwa ya mlipuko na majanga, kwa mfano ugonjwa wa ebola," anasema.

Waziri Ummy anasema, katika kupambana na magonjwa ya mlipuko na majanga yake, ni muhimu kushirikiana na jamii kupitia viongozi wa dini, ili kuleta uelewa mpana dhidi ya magonjwa hayo.

Anasema, lengo kuu ni kuwataka Watanzania wote wachukue tahadhari dhidi ya magonjwa ya mlipuko kwa kupata na kutoa taarifa sahihi na muhimu, za kujilinda wao, familia na wapendwa wao.

"Kwa sababu, hatua za utayari na tahadhari zinatakiwa kuwa kubwa zaidi, ikiwamo kuelimisha na kuhamasisha jamii ili ichukue tahadhari ya hali ya juu. Hii itawezekana kwa ushirikiano na viongozi wa dini," anasema.

Waziri anasema, mnamo Januari mwaka huu, WHO, ilitangaza virusi vya corona ni janga la kimataifa na nchi zilishauriwa kuongeza uwezo na utayari kukabiliana nao.

### HOFU TUPU

Waziri Ummy anakemea tabia ta baadhi ya watu kuzusha taarifa zisizo sahihi kuhusu ugonjwa huo, inayowafanya wengine kuangukia hofu.

Aidha, anawataka Watanzania kuzingatia kanuni za afya na usafi, ikiwa ni pamoja na kukaa mbali na mwenye dalili za mafua na mwenye historia ya kusafiri katika nchi zinazokumbwa na mlipuko wa ugonjwa huo.

"Vilevile ninapenda kuwahakikishia ninyi na jamii nzima ya Kitanzania na kimataifa kuwa hadi sasa Tanzania haina mgonjwa wala mshukiwa wa ugonjwa unaosababishwa na 'COVID-19' wala ebola," anasema.

Waziri Ummy anasema, kutokana na mwingiliano mkubwa uliopo na hasa kibiashara na kijamii kati ya Tanzania na nchi za Bara Asia na Ulaya, Watanzania wanakuwa katika hatari ya tishio la ugonjwa huo.

### CHA KUZINGATIA

Anasema, suala la kufunika mdomo na pua wakati wa kukohoa au kupiga chafya kwa kitambaa safi au nguo uliovaa hasa sehemu za kiwiko, kuzuia hewa kusambaa na kuhatarisha wengine ni muhimu.

> Serikali haijalala na inaendelea na jitihada kukabiliana na tishio la ugonjwa huo kwa kila njia.

"Kutokana na mwenendo na kasi ya kusambaa kwa ugonjwa huo kipindi hiki cha mlipuko, wizara inashauri kusubiri na kuepuka safari zisizo za lazima, kwenda kwenye maeneo yaliyoathirika," anasema.

Anasema, inapolazimu kusafiri ni muhimu wapate maelezo ya kitaalamu kabla ya kuondoka na hata baada ya kurudi nchini, hasa kuzingatia uvaaji wa 'mask' kwa kujikinga watakapotembelea maeneo au nchi zenye mlipuko wa ugonjwa huo.

"Pamoja na hayo, ni muhimu kuepuka kugusana na mgonjwa m wenye dalili za magonjwa ya njia hewa, kuzingatia usafi binafsi ikiwamo kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka," anasema.

Waziri anasema, pia ni muhimu kuwahi kwenye kituo cha kutoa

# Tiba inayopatikana Misri, Afrika Kusini pekee, sasa ipo Ocean Road



Mgonjwa akitibiwa kwa mashine katika Taasisi ya Kansa, Ocean Road. **PICHA: MTANDAO**

**Na Yasmine Protace**

UTOAJI wa huduma za kisasa sehemu yoyote ile, ni hali inayosaidia kuleta mabadiliko makubwa katika sehemu hiyo.

Huduma za kisasa zinachangia hata sehemu hiyo inayotoa huduma, kujulikana katika sehemu mbalimbali, pia jamii kukimbilia katika sehemu hiyo, ili kupata huduma za bora na za kisasa.

Ni kawaida jamii inajua matukio katika baadhi ya sehemu au kusikia sehemu fulani kuna huduma zinazotolewa. Hapo ndipo jamii inahamasika na kukimbilia mahali hapo, kutaka kupata huduma bora.

Hivi karibuni, Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), imeanzisha huduma mpya ya kibingwa ya kutibu ugonjwa wa saratani kwa miale ya mionzi, kwa njia ya kisasa zaidi ijulikanayo kama 'Intensity Modulated Radiation Therapy' (IMRT), ambayo mionzi inatibu eneo mahususi yenye tatizo pekee.

Tanzania inakuwa ya kwanza kutumia huduma hiyo ya IMRT kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki, huku kwa barani Afrika, inaingia kuwa nchi ya tatu baada ya Afrika Kusini na Misri.

Kwingine kulikobaki, huduma hiyo inayotolewa kwa nchi kama za Marekani na India na baadhi ya nchi ya za Ulaya.

Akizungumza na waandishi wa Habari, Mkurugenzi Mtendaji wa ORCI, Dk. Julius Mwaiselage, anasema kwa sasa wagonjwa waliokuwa wakienda kutibiwa nchini India watakaporejea wataweza kutibiwa nyumbani, kwani tayari wamenzisha huduma hiyo.

"Huduma hii awali ilikuwa inapatikana nje ya nchi, hasa nchi zilizoendelea ikiwemo, India. Hivyo hata wagonjwa watakaporejea hapa nchini wataweza kupata tiba hii hapa hapa na wakaendelea na matibabu," anasema.

Anasema, awali walikuwa wakitoa tiba ya kiteknolojia ya '3D' ambayo kwa sasa wameziongezea uwezo na inatumika kwa mashine hizio hizo za 'Linac Accelerator,' anasema Dk. Mwaiselage.

Dk. Mwaiselage anasema, mashine hizo zimenunuliwa kwa fedha za serikali zikiwa mpya kabisa kutoka kiwandani kwa bei ya Sh. bilioni 9.5 mbili za mionzi na kupanga tiba, mwaka 2018 na zilizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan mwaka jana.

Anasema zimekuwa na uwezo wa kutoa tiba mbalimbali za mionzi, ikiwamo teknolojia ya '3D' na zingine za upasuaji mionzi.

'Toka zimefka hizo mashine, tulianza na hiyo ya mionzi kwa teknolojia ya '3D', lakini kwa sasa mashine hizi tumeziongezea uwezo (upgrade) na kuanza kutumia tiba hiyo ya kisasa zaidi ya 'IRMT' ambayo kwa sasa inatumika duniani kote, ikiwamo Afrika Kusini, India na Marekani.

"Tiba hii ni mahususi kabisa kwa kutibu maeneo yale ambayo ungeona hauhitaji kufikiwa na miale ya mionzi mikali, kwenye eneo ambalo usingetaka iguswe," anasema.

Tabibu bingwa wa saratani wa Ocean Road, Dk. Sikudhani Muya, anasema tiba hiyo mpya ni maalum na itasaidia kuzuia mionzi mikali isipenye maeneo hata mengine yakadhurike.

"Huduma hii inasaidia kutibu eneo lenye saratani kwa miale yake ya mionzi kuenda kutibu eneo lile pekee lenye tatizo. Mfano, uvimbe wa saratani ukiwa eneo la kichwa basi tiba hii mionzi yake itaenda kutibu tu eneo hilo na sehemu za ubongo hazitaguswa," anasema.

"Hii ndio faida kuu ya tiba hii na ni ya kipekee sana ambapo inachukua dakika kuanzia 10 hadi 30,' anasema Dk. Sikudhani.

MAZINGIRA

AFYA MATATANI

# Kuendekeza zebaki kunavyoweka rehani uhai wa wachimba dhahabu

## • Wapo waelewaji, wengine hawajui • Baadhi wakiri wenzao wameshaumia • Wakutana na serikali, Ngo shida kuacha



Shughuli ya uchimbaji madini Geita. **PICHA: MAKTABA**

**Na Marco Maduhu,** Geita

UNAIJUA zebaki? Hiyo ni kemikali inayotumiwa na wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu kwa ajili ya kukamatia dhahabu wakati wa kuichenjua ndani ya mchanga wenye madini hayo.

Matumizi yake ni kwamba, kemikali hiyo huwekwa kwenye karai lenye mchanga wa madini ya dhahabu, pamoja na maji kwa ajili ya kukorogwa kwa mikono, ili ziweze kukamata dhahabu na kuisugua vizuri.

Huo ni upande wa kwanza, lakini upande wa pili, kitaalamu inaelezwa ni hatari kiafya, endapo inapenya kwenye mwili wa binadamu.

Kimsingi, wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu, wengi hawazingatii usalama wao wakati wa kuchenjua dhahabu, wakitumia kemikali ya zebaki, bila ya kuvaa vifaa kinga, kama vile kofia ngumu, nguo maalumu, viatu ya usalama na glovu, baadhi kwa makusudi na wengine kutojua.

Hatari inayotajwa inatokana na kutovaa vifaa hivyo vya kinga, ni endapo wakipatwa na mchubuko wakati wa kuisugua kemikali hiyo ya zebaki, kuna uwezekano mkubwa zebaki ikaingia mwilini na kuleta madhara ya kiafya.

> **"Ukiangalia hapa, karibu wachimbaji wote wadogo hatujavaa vifaa kinga, kwa sababu tumeshazoea kufanya kazi tukiwa tupu na hatuoni madhara yoyote ya zebaki.**

**MZIZI WA MADHARA**

Simulizi ya madhara hayo, inaenda mbali katika tukio la mwaka 1956, sasa ikitimu miaka 64 huko nchini Japan, katika Mji wa Kumamoto, ambako wafanyakazi waliokuwa kazini katika Kiwanda cha Maji Taka, wanaelezwa kuathirika na kemikali hiyo ya zebaki, ambayo ugonjwa huo ulipewa jina la Minamata.

Wafanyakazi walioathirika wanaelezwa kupatwa na maradhi ya malaria kali, kifafa na kupoteza kumbukumbu haraka, ikaishia wengi kupoteza maisha ndani ya muda mfupi.

Lakini, kinachoendelea katika migodi midogo nchini, wachimbaji madini ya dhahabu, wanapenda kutumia zebaki kuwasaidia kupata dhahabu haraka, licha ya kuwa na uelewa wa madhara yake, wengi wana kawaida ya kupuuza.

Wanaelezwa hawajali kuvaa kinga, kutokana na matumizi ya kemikali hiyo na huchukua muda mrefu kuanza kuonyesha madhara kwa binadamu.

**ZIARA MIGODINI**

Nipashe ilipofanya ziara katika baadhi ya migodi midogo ya uchimbaji madini ya dhahabu ya Nyakagwe, Nyarugusu na Msasa, mkoani Geita hivi karibuni kushuhudia uchenjuaji madini kwa matumizi ya kemikali ya zebaki, iliona namna utendaji hatari unavyotawala.

Iligundulika, vijana wengi wakiwa hawana vifaa vya kinga wakati wa kusugua zebaki iliyochanganyika na mchanga wa madini ya dhahabu, mikono yao ikiwa mitupu, hawajavaa viatu, pasipo kujali usalama wa afya zao.

Boniphace Charles, ni mchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu katika mgodi wa Mtalingi, uliopo Nyakagwe Geita, anayekiri kutambua zebaki ina madhara ya kiafya na kubainisha wameshazoea kuchenjua dhahabu bila ya kuvaa vifaa kinga.

Anasema wachimbaji wadogo wengi wa dhahabu, hawana elimu ya kutosha kuhusu madhara ya zebaki, zaidi ya kusikia tu ina madhara kiafya na wamekuwa hawavai vifaa kinga, kwa sababu wameshazoea kuchenjua dhahabu kwa mikono mitupu, bila viatu miguuni.

"Madhara haya ya matumizi ya zebaki tunayajua kwa kusikia tu, lakini hatujawahi kumshuhudia mchimbaji ameathirika na zebaki. Utasikia tu fulani sasa hivi anaumwa kweli na wengine kufa, lakini kuwaona kwa macho bado ndio maana tunaendelea kuitumia zebaki bila ya hofu kuwa hatuwezi kuugua.

"Ukiangalia hapa, karibu wachimbaji wote wadogo hatujavaa vifaa kinga, kwa sababu tumeshazoea kufanya kazi tukiwa tupu na hatuoni madhara yoyote ya zebaki," anaeleza mchimbaji huyo.

Shida Lupanga ni mchimbaji mdogo wa dhahabu, katika mgodi wa Msasa, wilayani Chato, mwenye ushauri kwamba kinachopaswa kwa wachimbaji wadogo, ni kujikinga na madhara ya matumizi ya zebaki kwa kutolewa elimu ya kuvaa vifaa kinga, ili wabaki salama.

Anasema, wachimbaji wengi kwenye migodi midogo, wanatoka sehemu mbalimbali kufuata riziki mahali hapo penye uchimbaji na hawajui madhara ya zebaki, wanaishia kufanya kazi kwa mazoea, baada ya kuwakuta wenzao wanachenjua dhahabu bila ya kinga.

Lupanga ana ufafanzi: "Kitu kikubwa tunachokiomba ni utolewaji elimu juu ya madhara haya ya matumizi ya zebaki,"

Joseph Shindika, ni mchimba madini mdogo katika mgodi wa Nsangano, anasema hivi sasa wamebadilika, baada ya kupewa elimu ya afya dhidi ya zebaki na sasa wanavaa vifaa kinga.

Anasema mgodini, hivi sasa kuna taasisi inayojishughulisha na uwezeshaji wachimbaji wadogo, walifika kwenye mgodi huo na kutoa elimu juu ya madhara ya zebaki, hasa wanakochenjua dhahabu bila ya kuvaa vifaa kinga, ndipo wakaona umuhimu wa kuvaa vifaa hivyo ili wawe salama.

**MMILIKI MGODI**

Mmilikiwa wa mgodi mdogo wa madini ya dhahabu, Mtalingi, uliopo Nyakagwe, Mtalingi Hamzeh, anakiri kutambua madhara ya matumizi ya zebaki katika kuchenjua madini ya dhahabu, lakini wanashindwa kuepuka, kutokana mbadala una gharama kubwa zaidi.

Anasema, kutokana na kutambua madhara hayo ya zebaki wamekuwa wakitoa elimu kwa wafanyakazi wao, wanawagawia vifaa kinga na wanapochenjua dhahabu, lakini baadhi yao hawavai wamekuwa wakikaidi kwa kuendelea na mazoea ya siku zilizopita.

"Umaskini nao unachangia wachimbaji wadogo kuitumia zebaki katika shughuli zetu za uchenjuaji madini ya dhahabu. Hatuwezi kumudu gharama za teknolojia nyingine za kukamatia dhahabu ambazo ni salama.

"Ili tupate kuwa salama tuna-

MAZINGIRA

# Kuendekeza zebaki kunavyoweka rehani uhai wa wachimba dhahabu

ziomba taasisi za kifedha zitukopeshe wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu, tumudu gharama za kutumia teknolojia nyingine ya kuchenjua dhahabu na kuondokana na matumizi ya zebaki ambayo ni hatari kwa afya zetu," anaongeza.

Ibrahim Makala, Meneja wa Mgodi wa Nsangano Gold uliopo Nyarugusu, anasema kwa sasa wapo kwenye hatua ya kuacha matumizi ya zebaki kuchenjua dhahabu, na wanatumia njia mbadala anayoiita 'gold culture' ambayo wako katika majaribio.

Anasema, baada ya kupewa elimu ya madhara ya matumizi ya zebaki, kwa sasa wanawajali sana wafanyakazi wao na wamekuwa wakiwapatia vifaa kinga, pamoja na kufuatilia matumizi yake, ili kuepukana madhara ya zebaki.

"Sasa tupo kwenye hatua ya kuachana kabisa na matumizi haya ya zebaki kuchenjulia dhahabu. Tupo kwenye hatua ya kutumia 'gold culture'... tupo kwenye hatua ya majaribio, japokuwa mashine hizi nazo zina gharama kubwa takribani Sh. milioni 10 na ukiangalia sisi wachimbaji wadogo mtaji wetu ni mdogo," anasema.



Shughuli za kuchenjua madini zikiendelea, katika njia inayotajwa hatari kupitia matumizi ya zebaki. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

### WADAU WAELIMISHAJI

Theonestina Mwasha, Mkurugenzi wa taasisi ya kiraia FADeV inayojishughulisha na kuendeleza wachimbaji wadogo nchini, ikiwamo kuwapatia elimu, namna ya kujikinga na madhara ya matumizi ya zebaki, vifaa kinga wakati wa kuchenjua dhahabu au kutumia njia salama ya kisasa ya 'gold culture.'

Anasema, walifanya utafiti kwenye baadhi ya migodi midogo ya madini na waligundua wachimbaji kukosa elimu kabisa, kuhusu madhara yanayowakabili, ikiwamo uchenjuaji kwa zebaki na bila ya kutumia kinga, kwa athari ya miili yao.

"Mchimbaji anavyochenjua dhahabu, mikono yake ikiwa tupu, ambapo akipatwa na mchubuko na zebaki ikiingia ndani ya mwilini wake, tayari inaanza kumletea madhara ya kiafya taratibu, ikiwamo kichwa kuuma, kupoteza kumbukumbu, kutosikia, kuathiri figo na hatimaye kupoteza maisha," anasema.

Mwasha anasema, kwa sasa wanajikita kutoa elimu hiyo ya madhara ya matumizi ya zebaki kwenye migodi midogo iliyopo mkoani Geita, ili wanaoelimishwa wabadilike na kuwa mabalozi wazuri kwa wenzao wajikinge, ili kuondoa athari ndani ya jamii na hata vizazi vyao.

### SERIKALI MKOA

Katibu Tawala Msaidizi, katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, Hermani Matemu, anasema sekta ya madini ni muhimu na serikali imeboresha Sheria ya Madini, ili wachimbaji wanufaike na rasilimali zao, wainuke kiuchumi bila ya kuathiri afya zao.

> **Sasa tupo kwenye hatua ya kuachana kabisa na matumizi haya ya zebaki kuchenjulia dhahabu. Tupo kwenye hatua ya kutumia 'gold culture'...**



Kipande cha dhahabu, baada ya kuchenjuliwa.

Anasema taasisi hiyo ya Fadev imejitokeza katika wakati muafaka wa utoaji elimu dhidi ya madhara ya zebaki, hasa kwa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu na wamekuwa wakiitumia kwa kiwango kikubwa bila ya kujua madhara yake.

Matemu anaahidi, serikali itashirikiana na shirika kutoa elimu inayohusu madhara ya zebaki.

Ofisa Madini wa Mkoa Geita, Daniel Mapunda, anasema serikali kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali, imeshatoa elimu kwa wachimbaji wadogo juu ya madhara ya matumizi ya zebaki, kupitia kwenye mikutano na warsha na imeshauri utumiaji vifaa kinga kuchenjua madini hayo, ili wawe salama.

Anasema, hadi sasa serikali imeshaingia mkataba wa kimataifa kufuta matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo na kuhamia mbadala wa kuchenjua dhahabu, lakini ni njia zenye gharama kubwa na wachimbaji wadogo hawazimudu, hivyo kinachofanyika ni kuwabadilisha taratibu.



Mapunda anafafanua: "Tukisema leo tuzuie kabisa matumizi ya zebaki, nadhani tutaathiri sekta ya uchimbaji kwa sababu zebaki ina gharama ndogo na rahisi kupatikana na ina uharaka wa kukamata madini kuliko njia zingine."

"Unakuta mchimbaji ana mifuko miwili ya mawe ya dhahabu, ukimwambia atumie teknolojia ya kemikali ya (cynide) ambayo ni nzuri zaidi kwa ukamataji wa dhahabu, hawezi kuimudu sababu ya gharama, hivyo tuendelee kutumia zebaki ambayo ina gharama ndogo, licha ya kujua ina madhara kiafya," anafafanua.

Pia, anasisitiza azma ya serikali kuendelea na utoa elimu kwa wachimbaji wadogo, kuhusu madhara yaliyoko kutoka kwenye zebaki, pamoja na kuwa na mpango wa kuwarasimisha, ili waone namna ya kuwasaidia kutumia teknolojia mbadala katika kuikamata dhahabu, na siyo hatari ya zebaki kwa afya zao.

AFYA

# KITENDAWILI CHA CORONA SI MASIHARA BARA AFRIKA



Waziri Mkuu wa China, Chung Sye-kyun, akiongoza kikao cha serikali kujadili tiba ya maradhi ya corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Michael Eneza**

ZIKIANGALIWA picha zinazotoka katika maeneo kadhaa yenye mikutano rasmi hivi karibuni, kuna mwelekeo wa baadhi ya wasanii na wanahabari wanaoona katika sura ya mzaha, ingawa waliofanya maonyesho hayo hawakuwa wanafanya mzaha.

Kuwapo tahadhari dhidi ya maambukizi yasiyotarajiwa ya virusi vya corona, ilihisiwa kwamba, virusi hivyo bado havijaingia nchini.

Hapo ina maana kwamba hawakuwa na shaka ya kuambukizana wenyewe, bali haja ya kuonyesha 'demo' ya kuzuia ugonjwa huo usienee, yaani jinsi ya kusalimiana. Ni hapo wanaoishia katika tafsiri ya mzaha, kumbe yenyewe 'ina maana' kubwa zaidi.

Mtu anapoangalia kinachofanyika, kuna shaka halisi ya kuingia katika mazingira ya maambukizi ya homa ya corona katika mataifa duniani, kila moja katika tahadhari.

Hao ni wadau wakuu katika mazungumzo yao, yanafuatilia kwa mbali, ikihitajika kuongea basi simu zinaweza kutumika au kama ni kufanyika kwa wengi ni kwa video.

Mikutano muhimu duniani kama ya kila mwaka au miezi sita, kwa Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) inayofanyika mwezi Aprili, imefutwa.

Pia, Hijja ya mwaka huu imefutwa rasmi, katika jitihasa kuunda mwelekeo wa kumaliza tatizo la homa ya corona. Ni maeneo mengi duniani corona ndiyo inapiga hodi na ziko, baadhi ni zilizopiga hatua ndefu ya maendeleo, lakini maambukizi bado ni ya kasi.

> **Mtu anapoangalia kinachofanyika, kuna shaka halisi ya kuingia katika mazingira ya maambukizi ya homa ya corona katika mataifa duniani, kila moja katika tahadhari.**



Sehemu ya harakati kujinusuru na corona.

**INAVYOPENYA**

Nchi ambazo hadi sasa zimenusurika, ni zilizogundua kuambukizwa katika viwanja vya ndege na mgonjwa kufanyiwa utaratibu maalum wa kutengwa wa kumtenga, ila ambao hawakugundulika wanaweza kuingia mtaani na janga.

Hatua hiyo inafikiwa, endapo mtu mmoja aliyeathirika alijipenyeza, kwa mfano baharia ambaye meli yake inatia nanga na anaingia mitaani pasipo kujulikna kuugua kwake.

Kuna tofauti kubwa zilizoonekana kati ya uwezo wa nchi moja na nyingine kuzuia kuenea virusi vya corona na hadi sasa, China inaelekea imefanya vizuri zaidi kuliko Iran, Italia na hata Korea Kusini.

Hata hivyo, kuna tatizo la kulinganisha nchi zilizo katika hatua tofauti tangu maambukizi ya kwanza yaonekane, pia kuna suala la upana wa kiini cha maambukizi yenyewe.

Ni kiini kikubwa kwa upande wa China kuanzia soko la nyamapori la kitaifa, nyakati za kuandaa sikukuu na kikubwa kiasi kwa Korea Kusini, mkusanyiko wa kidini uliotembelea China awali.

Iran na Italia hazikuwa na mikusanyiko ya maambukizi ya awali kama hiyo, hata hivyo zimepata tatizo katika kuzuia kuenea virusi hivyo, ila haiwezekani kusema ni kiwango gani zimefaulu kuvizuia au zinatofautiana vipi na China au Korea Kusini.

Mtu akisikiliza kinachozungumzwa na Kamati Maalum ya Shirika la Afya Duniani (WHO), mtu anapata picha kuwa hadi idadi ya maambukizi mapya ianze kupungua kitaifa kwa njia endelevu, kama inavyoonekana China hadi mwanzoni mwa mwezi Machi, siyo rahisi kusema nchi imefaulu kiasi gani.

**KUSINI SAHARA?**

Jambo linalotia hofu ni kuanza kutafakari kitakachotokea katika nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara, maambukizi yakiingia na kuanza kushika kasi na hasa siyo mtu anayepitia uwanja wa ndege aguduliwe.

Ni kama maambukizi ya mtu anayeingia kinyemela au kwa njia za njia hafifu ambazo hazikaguliwi, hali ambayo ni rahisi kutokea baadaye ya virusi vitakuwa vimesambaa katika nchi jirani.

Hofu hiyo haikuwahi kufikia hatua kubwa zaidi wakati wa hofu ya ugonjwa wa ebola. Kuna eneo lingine la kutoa tegemeo ambalo nalo ni gumu kufikirika, kama lina chembe ya uwezekano kisayansi.

Mara nyingine inafika wakati kunakuwapo virusi vinavyoambatana na watu wa aina moja au tofauti ya vinasaba.

Kwa mfano, wakati virusi vya ukimwi vilipoanza kusambaa duniani wastani wa miongo minne iliyopita, iligundulika kuwa nchi za Ulaya na Marekani, virusi hivyo vilienea kwa watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja.

Barani Afrika, ni virusi vilivyoenea zaidi kwa tendo la mapenzi ya njia ya kawaida. Leo hii, hadi sasa hapajakuwapo nchi ya Afrika iliyoathirika na virusi vya corona, halafu vikaenea kwa haraka.

Hiyo inafanya kusiwepo sababu, ya kudhani kuwa hali hiyo ingedumu, kwani maambukizi tayari yalishaanza kutajwa, ila hayakuwa yameanza kuenea kwa kasi kubwa.

Siyo rahisi kulinganisha uwezo wa Bara Afrika katika kupambana na virusi hivyo, endapo vitaanza kuenea kwa kasi, kwani hata nchi zenye uwezo wa kufanyia kazi hizo kwa haraka kama Marekani, kuna idadi ya vifo vinavyoongezeka.

Nchini China ilifikia kwenye maelfu, wakati tahadhari zilishaanza kuchukuliwa yapata karibu mwezi mmoja tayari. Kimbunga cha maambukizi na ukali wake, au ugumu unaoonekana kutoa dawa, inayofaa kwa wakati ukiwa ule ule itakuwa balaa.



HABARI MBEYA

# Daraja lakata mawasiliano Busokelo

**Na Nebart Msokwa, BUSOKELO**

MAWASILIANO ya barabara kati ya Kata ya Lufilyo na maeneo mengine ya Halmashauri ya Busokelo yamekatika baada ya daraja la Mto Lufilyo kuchanika nyufa na hivyo kusababisha wenye magari kusitisha kupeleka huduma ya usafiri.

Kutokana na hali hiyo, shughuli za usafirishaji wa mazao ya kakao, ndizi, viazi na madini ya mable kusimama na hivyo kuhatarisha uchumi wa wananchi wa kata hiyo, pamoja na huduma zingine za kijamii kuporomoka.

Wakizungumza na Nipashe juzi wananchi hao walisema daraja hilo ndilo pekee linategemewa katika eneo hilo kwa ajili ya kuvuka kutoka ng'ambo moja kwenda nyingine na kwamba baada ya nyufa hizo kuonekana hakuna gari inayovuka.

Mmoja wa wananchi hao, Obed Mwampo, alisema barabara hiyo inaunganisha pia wilaya za Rungwe na Makete mkoani Njombe na kwamba kukatika kwake kumesababisha adha kubwa kwao.

Alisema hata watembea kwa miguu katika daraja hilo wameanza kuogopa kutokana na kuwa na hofu ya kuvunjika wakiwa wanapita na kupoteza maisha.

Alisema wakitaka kwenda Tukuyu Mjini yalipo Makao Makuu ya Wilaya ya Rungwe, wanalazimika kupita njia ya Kyela ambayo ni ndefu na inaongeza gharama za usafiri na usafirishaji wa vitu mbalimbali.

"Kwa sasa biashara ya mazao yetu imesimama kwa sababu hatuwezi kusafirisha, lakini gharama za usafiri zimekuwa kubwa kwa sababu tunatakiwa kama unaenda Tukuyu unalazimika kwenda kupitia Kyela, tunaiomba serikali itusaidie," alisema Mwampo.

Naye Daud Mwakaliku, alisema baadhi ya wanafunzi wa kata hiyo wanasoma shule ambazo zipo ng'ambo ya pili na kutokana na kukatika kwa mawasiliano hayo na wao wamekwama kuhudhuria masomo.

Alisema endapo daraja hilo halitatengenezwa haraka kuna hatari wananchi wa eneo hilo wakaathirika kwa kukosa huduma muhimu za kijamii na kiuchumi.

Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete, ambaye alikuwa kwenye ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata hiyo, alisema daraja hilo ni kiungo muhimu cha shughuli za uchumi katika jimbo lake.

Aliiomba serikali kulijenga upya daraja hilo katika bajeti ijayo ya mwaka wa fedha 2020/2021 ili wananchi waendelee na shughuli zao za maendeleo kama ilivyokuwa miaka yote.

"Kwa sasa hatuna namna nyingine ya kusafirisha bidhaa zetu, hata viongozi wetu wa kitaifa wakija hapa watajionea umuhimu wa daraja hili kwa wananchi maana kwa sasa wananchi hawawezi kuvuka tena," alisema Mwakibete.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) wa Halmashauri ya Busokelo, Mhandisi Derick Mwamala, alisema daraja hilo lilijengwa miaka mingi na ndio maana limechoka.

Alisema walibaini tatizo hilo mwaka 2016 baada ya Tarura kuundwa na kwamba walipolikagua walibaini kuwa kuna baadhi ya nguzo zimepinda na hivyo kuwa katika hatari ya kuvunjika.

Alisema wanakusudia kulijenga upya daraja hilo na kwamba kwa sasa wameshaanza kuweka alama litakapojengwa daraja jipya katika eneo hilo.

## Mbarali wajenga shule sita sekondari

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

SERIKALI kwa kushirikiana na wananchi wilayani Mbarali, imefanikiwa kujenga shule mpya za sekondari sita kwa lengo la kuongeza fursa kwa wanafunzi wanaofaulu mitihani ya darasa la saba, kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari.

Aidha, shule hizo zimejengwa ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa lililojitokeza baada ya idadi kubwa ya wanafunzi kutakiwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya hiyo ya Mbarali, Ruben Mfune, na kubainisha kuwa wananchi wengi wamekuwa na mwamko mkubwa katika kuunga juhudi za serikali za kuhakikisha kila mwanafunzi anapata elimu ya sekondari.

Mfune alisema shule zilizojengwa kwa nguvu ya serikali na wananchi ni Shule ya sekondari Muwale yenye madarasa matano, Shule ya Sekondari Kapunga yenye madarasa matatu, shule ya sekondari Itamboleo yenye madarasa vitatu, shule ya sekondari Ihanga yenye madarasa matano na Shule ya Sekondari ya Nyamakuyu yenye madarasa vitano.

Alisema ujenzi wa shule hizo ni mwendelezo wa ujenzi wa shule za sekondari na vyumba vya madarasa kwa shule zilizopo na kuwa kwa mwaka 2019 serikali kwa kushirikiana na wananchi walifanikiwa kujenga shule mbili ambazo ni Shule ya Sekondari Ipwani ambayo ilikuwa na madarasa vitatu na kuwa kwa mwaka huu wameongeza ujenzi wa madarasa mawili.

Alisema shule nyingine iliyojengwa mwaka jana ni Shule ya Sekondari Mwakaganga iliyokuwa na vyumba vitano na kuwa kwa mwaka huu wameongeza vyumba vingine vitano na kuwa mpango uliopo kwa mwaka ujao ni kujenga shule zingine tatu za sekondari.

Alisema jitihada za ujenzi huo unatokana na mwamko wa wananchi kutambua mchango wa serikali ya Rais Magufuli katika kutoa elimu bure kwa wanafunzi kuanzia shule za awali mpaka shule za sekondari kote nchini.

Alisema mafanikio ya ujenzi wa shule hizo unatokana na michango ya hiyari ya wananchi katika kuharakisha sekta ya elimu wilayani humo, pamoja na mipango thabiti ya wilaya katika kuondokana na changamoto ya wanafunzi wanaokosa elimu kwa sababu ambao zipo ndani ya uwezo wa wilaya.



Baadhi ya vijana wakisukuma gari la abiria linalofanya safari zake, kati ya Iyunga na Sokomatola, jijini Mbeya, baada ya kupata hitilafu jirani na Kituo cha Polisi Kati, jijini humo jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Elimu bila malipo yaongeza wanafunzi

**Na Innocent Ng'oko, MMBEYA**

OFISA Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Paulina Ndigeza, amesema kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya wanafunzi kwa shule za serikali walioanza elimu ya awali, msingi na sekondari kutokana na mwamko wa wazazi na utekelezaji wa elimu bila malipo.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake ambapo alibainisha kuwa shule za awali zinazomilikiwa na serikali kuna jumla ya wanafunzi 47,320 walioanza masomo mwaka huu idadi ambayo ni sawa na asilimia 94.

Alisema katika shule za msingi za serikali kuna jumla ya wanafunzi 53,559 walioanza masomo yao katika shule mbalimbali zinazomilikiwa na serikali kwa mkoa mzima na kuwa kiasi hicho ni sawa na asilimia 103.

Alisema kwa shule za sekondari kuna jumla ya wanafunzi 30,733 sawa na asilimia 89 .2 ya wanafunzi walioanza masomo yao katika shule za sekondari mkoani Mbeya kwa mwaka huu.

Alisema ongezeko hilo linatokana na mwamko wa wazazi katika suala la elimu mkoani Mbeya na hamasa za watoto wenyewe kutaka kusoma zaidi kwa lengo la kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya dunia.

Paulina alisema wanafunzi wote ambao awali walikosa nafasi ya kuanza kidato cha kwanza wapatao 2,617 walishaanza masomo kulingana na agizo la waziri na kuwa kwa sasa uhaba wa vyumba vilivyokuwa vinaukabili mkoa wa Mbeya vimekamilishwa.

"Kwa Mkoa wa Mbeya tulikuwa na wanafunzi 2,617 ambao walikosa nafasi ya kuanza kidato cha kwanza, lakini mpaka sasa tunavyozungumza wanafunzi wote waliofaulu kwa ajili ya kuanza elimu yao ya sekondari wapo darasani na wanasoma," alisema Paulina.

Alisema kwa Wilaya ya Chunya vyumba sita vilivyokuwa vinahitajika vimeshakamilishwa, vyumba 36 vilivyokuwa vinahitajika kwa wilaya ya Mbarali vimeshajenga, vyumba 11 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini vimeshajengwa na vyumba sita katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe vimeshajengwa.

Alisema halmashauri za wilaya za Kyela na Mbeya jiji hazikuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa kwa mwaka huu, ingawa wapo katika mpango endelevu wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika miaka ijayo kwa wanafunzi wa sekondari wanaofaulu.





# Unyanyapaa wamtoa machozi Spika Ndugai

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameeleza namna alivyototkwa na machozi na kulazimika kuvunja Kamati ya Bunge ya masuala ya Ukimwi ya awali kutokana na wabunge walioteuliwa kutokuwa na utayari kufanya kazi kwenye kamati hiyo.

Amesema tatizo la unyanyapaa kwa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) halipo kwenye jamii pekee bali hata ndani ya Bunge na kutaka wabunge na jamii kwa ujumla kubadilika kwa kuachana na vitendo hivyo.

Spika Ndugai alitoa kauli hiyo juzi jijini Dodoma wakati wa kampeni ya kushirikisha viongozi wa dini kupinga unyanyapaa na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Kampeni hiyo inaratibiwa na Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) kupitia mradi wa Tuyajenge, unaofadhiliwa na Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Ukimwi (PEPFAR) na Shirika la USAID.

"Tulipoanza Bunge la 11 ambalo tunafikia mwisho, katika kamati nilizounda ni pamoja na Kamati ya Ukimwi na wajumbe wa kamati ile waliniita si chini ya mara tatu katika nyakati tofauti wakinihoji, 'Spika umetumia kigezo gani kututeua sisi katika kamati hii?'

"Yaani wameniweka kiti moto, wakasema 'wenzetu umewapa kamati kama kilimo, maji, barabara na sisi tumeteuliwa na watu, yaani umetuona sisi tuna Ukimwi?' Wakauliza ni utaratibu gani umeniongoza.

"Baada ya kuniita mara tatu wakihoji, leo niseme wazi nilirudi ofisini kwangu na kutokwa na machozi, sisi ni viongozi, ni nani sasa afanye?

"Ilinibidi nivunje kamati ile, niunde nyingine kwa kuwaomba sana hao niliowateua waifanye kazi hii, leo nakiri wamefanya kazi kubwa sana na kwa uadilifu na ndiyo maana leo tupo hapa," alifafanua.

Spika Ndugai alisema kamati hiyo ni miongoni mwa zilizofanya kazi nzuri katika Bunge la 11 na kampeni hiyo ni matunda ya kazi yao.

Alisema Watanzania ni wepesi kupima magonjwa mengine, lakini ni wazito katika kupima VVU.

"Yaani ningesema leo nimeweka kipimo kwamba kabla ya kuingia bungeni apimwe malaria, UTI au corona, wabunge wote wangekuja, lakini nikisema huingii bungeni hadi upimwe VVU, kwanza nadhani akidi sitapata, sijui kuna nini kwenye jambo hili," alisema.

Kiongozi huyo wa Bunge alisema unyanyapaa ndiyo sababu inayosukuma watu kuogopa kupima afya zao na kuwataka kuondoa wasiwasi na uoga kwa kuwa ugonjwa huo ni sawa na magonjwa mengi.

Akizindua kampeni hiyo, Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, alisema serikali inatambua nguvu kubwa waliyonayo viongozi wa dini katika jamii kusaidia kutokomeza unyanyapaa.

Majaliwa alisema kampeni hiyo inalenga kuhamasisha umma kuungana na kutokomeza unyanyapaa dhidi ya VVU na Ukimwi nchini.

Waziri Mkuu alisema kila mmoja akipima na kutambua afya yake itasaidia kuondokana na maambukizo mapya.

"Tambueni kwamba mnayo kazi kubwa ya kufanya katika kuhakikisha unyanyapaa na ukatili wa kijinsia unakwisha kabisa katika jamii yetu kwa kupitia ibada katika madhehebu yenu na makongamano," alisema.

Alisema licha ya dini zote kukemea ubaguzi na unyanyapaa, bado unyanyapaa na ukatili wa kijinsia hasa kwa watoto vimeshamiri katika jamii.

"Watu wanaoishi na VVU hukumbwa na kadhia ya unyanyapaa katika jamii zetu. Kadhalika, watoto wa umri mdogo nao wanatendwa ukatili mkubwa sana kama vile kunajisiwa na kutelekezwa," alisema.

Majaliwa alitumia fursa hiyo kupiga marufuku matumizi ya neno waathirika badala yake yatumike maneno 'watu wanaoishi na VVU' ili kuondoa unyanyapaa dhidi ya kundi hilo.

Aliwataka wanaume kujitokeza kwa wingi kupima VVU kwa kuwa kusuasua kwao kunasababisha maambukizo mapya.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Jenista Mhagama, alisema maambukizo mapya ya VVU yamepungua kutoka watu 100,000 hadi 72,000 kwa mwaka, huku akisema asilimia 40 ya maambukizo hayo yanatokana na vijana.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema Watanzania milioni 1.2 wanatumia dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo (ARVs).

Aliwaomba wabunge kupima afya zao ili wanapokwenda majimboni kwenye uchaguzi wawe na afya njema na kuhamasisha wananchi kupima pia.

Katika kampeni hiyo viongozi wa madhehebu yote nchini walitia saini tamko la kutokomeza unyanyapaa huo, huku baadhi ya taasisi vikiwamo vituo vya ITV na Radio One zikitambulika kwa mchango wake kwenye mapambano dhidi ya VVU.



Spika wa Bunge, Job Ndugai akipanda mti katika eneo la Hospitali ya Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma juzi, ili kuboresha mazingira. Wa pili kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kongwa Dk. Omari Mkulo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Aagiza ukaguzi maalum mradi wa kitalu nyumba

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imeagiza kufanyika ukaguzi wa fedha za mradi wa kitalu nyumba kwenye halmashauri zote za mikoa 12 ulikotekelezwa.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alipofungua mkutano wa vijana wanaoshiriki mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa teknolojia ya kitalu nyumba jijini hapa.

Alisema lazima ukaguzi maalum ufanyike ili kuangalia kiasi cha fedha ambacho kipo kwenye akaunti za vijana wanaojishughulisha na kitalu nyumba.

"Ni lazima ukaguzi ufanyike huko kwenye halmashauri na hawa vijana watakuwa mashahidi, maana watatueleza walivuna kiasi gani, kiliuzwa kiasi gani na kiasi gani cha fedha kipo kwenye akaunti," alisema.

Kuhusu mikopo, Mhagama alitaka mikopo kwa vijana itolewe kwa wakati na kisiwapo kikwazo kwenye utekelezaji wa programu hiyo kwa kuwa kuna mifuko ya uwezeshaji kiuchumi 54 nchini.

Pamoja na hayo, alimwagiza Katibu wa Wizara hiyo kuhakikisha wanaanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa mradi huo na vitalu hivyo vitakapokabidhiwa kwa vijana.

"Huu mfumo pia uwapo kwenye mapato na matumizi ya vitalu nyumba, tunataka mfumo wa kufuatilia fedha na matumizi, ili fedha zikiingizwa kwenye akaunti ya vijana zionekane na hata zinapotolewa zionekane kama zinatolewa na mtu mmoja au wawili au ni uamuzi wa kikundi," aliagiza.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huo, ofisi yake imeshatoa mafunzo kwa vijana 100 kwa kila halmashauri kuhusu vitalu nyumba na kama wakitumika ipasavyo, watasaidia nchi kupiga hatua kimaendeleo.

Alisema ofisi yake pia imejenga vitalu nyumba kwa ajili ya vijana katika halmashauri 84, lakini mpaka sasa vitalu nyumba hivyo vipo chini ya mkurugenzi ambaye yuko ofisini na hakuna uendelezaji badala ya kukabidhi kwa vijana ili kuwe na uendelevu.

Awali, Mkurugenzi Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Juma Madaha, alisema wanatarajia kuwa na utaratibu wa kuweka kumbukumbu za uendeshaji, ukusanyaji wa mazao na fedha ambazo zitaweka kwenye akaunti maalum.

Ofisa Kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, Masumbuko Weswa, alisema wizara itahakikisha pembejeo zinapatikana kwa uhakika kwenye programu hiyo.

# Aona fursa kwa wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**


KATIBU wa Chama cha Wenye Ulemavu Mkoa wa Dodoma, Mchungaji Kalebi Shedrack, amewataka watu wenye ulemavu kuondokana na dhana ya kuomba misaada mitaani na badala yake watumie fursa ya mikopo inayotolewa na halmashauri kujikwamua kiuchumi.

Alitoa rai hiyo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu fursa hiyo jijini Dodoma, akisema serikali inatoa mikopo kupitia mapato ya halmashauri kutenga asilimia mbili ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kundi hilo.

"Hii mikopo inatolewa kwa vikundi, watu wenye ulemavu waunde vikundi na kusajili ili kupata mikopo isiyo na riba badala ya kuwa tegemezi na omba omba," alisema.

Katibu huyo alisema hatua hiyo ya serikali ni utekelezaji wa Sheria Na. 9 ya Mwaka 2010 inayohusu haki na ulinzi kwa watu wenye ulemavu. Mchungaji Shedrack aliipongeza serikali kwa kudhamiria kuwaondoa watu wenye ulemavu kwenye utegemezi.

"Wapo watu wenye ulemavu wana uwezo mkubwa sana na endapo wakipewa fursa ya kufanya vitu, wana uwezo wa kufika mbali zaidi kimaendeleo," alisema.



# Dk. Shein asisitiza amani, usalama

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema ipo haja kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuendelea kusimamia amani na usalama wa wananchi na mali zao wakati wote.

Alisema hayo wakati alipofanya mazungumzo na Waziri wa wizara hiyo, George Simbachawene, Ikulu Zanzibar, alipofika kwa ajili ya kujitambulisha kufuatia kuteuliwa kushika wadhifa huo hivi karibuni.

Alisema Serikali ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na wizara hiyo kuhakikisha amani, usalama na utulivu unaendelea kudumu nchini.

Kadhalika, serikali kwa upande wake itaendelea kuhakikisha amani, usalama na utulivu unakuwapo kwa wananchi pamoja na mali zao na ndio sababu imeanzisha mradi wa mji salama katika maeneo mbalimbali ikiwamo Mji Mkongwe.

Alifafanua kuwa mradi huo wa mji salama pia una lengo la kuhakikisha wageni wote wakiwamo watalii wanaotembelea Zanzibar wanakuwa salama.

Alisema ipo haja kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha linaendelea na utaratibu wake wa kuwalinda wananchi na mali zao.

Vile vile, alieleza juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Jeshi la Polisi kusimamia ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao pamoja na kusifu juhudi za Idara ya Uhamiaji kwa kuendelea kudhibiti na kupambana na wahamiaji haramu.

Alilitaka Jeshi la Polisi kuendelea kusimamia vyema usalama wa barabarani kwa lengo la kuepuka ajali zisizo za lazima.

Alimpongeza Waziri Simbachawene kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo na kumwahidi kuwa yeye pamoja na serikali anayoiongoza wataendelea kumsaidia.

Naye Simbachawene, alimhakikishia Dk. Shein kuwa atahakikisha amani na usalama kwa pamoja vinaendelea kudumishwa ili Tanzania iendelee kusifika ndani na nje ya Afrika.

Simbachawene alisema jukumu la wizara hiyo la kuhakikisha usalama na amani kwa wananchi pamoja na mali zao unakuwapo wakati wote na kusisitiza kuwa kwa ushirikiano wa pamoja wa vikosi vya ulinzi na usalama jambo hilo litaendelea kutekelezwa.

Alimpongezi Dk. Shein kwa kupatiwa eneo la kujenga ofisi za Idara ya Uhamiaji.

Alimhakikishia Dk. Shein kuwa juhudi zitaendelea kuchukuliwa na Jeshi la Polisi katika kuhakikisha sheria na kanuni zinafuatwa hasa zile za usalama barabarani.



Umati wa wakazi wa mjini Zanzibar wakiwa kwenye foleni ya kusaka vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi kwenye Kituo cha Elimu Mbadala, Rahaleo mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Wastaafu Juwaza wataka kujadiliwa changamoto zao

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIBU wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahaya Mzee, ameziomba taasisi za serikali kukaa pamoja na Jumuiya ya Wastaafu na Wazee Zanzibar (JUWAZA), kujadili changamoto zinazoikabili jumuiya hiyo.

Alisema hayo katika mkutano wa pamoja uliowashirikisha Makatibu Wakuu na jumuiya hiyo uliojadili masuala ya wazee, uliofanyika mjini hapa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kutoa mapendekezo kwa pande zote mbili na kuyawasilisha serikalini ili yaweze kupatiwa ufumbuzi.

Alisema ni vyema kwa taasisi zinazohusika kutoa kipaumbele kwa huduma za kijamii kwa wazee ikiwamo afya, kilimo, usafiri, maji, umeme na nyingine ili waweze kuzipata kwa haraka.

Pia, alisema kuna umuhimu wa kuthaminiwa wazee kwa kuwa wametoa mchango mkubwa na kuleta maendeleo ya nchi, hivyo wanahitaji kuungwa mkono na kushughulikiwa ili mchango wao walioutoa wasione umeenda bure.

Kwa upande wao makatibu wakuu walisema ni vyema serikali kubuni miradi mbalimbali ya maendeleo itakayosaidia wazee hao kuinua kipato chao.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda, Juma Hassan Reli, alisema wazee wengi wameelekeza nguvu zao katika kilimo, hivyo ni vyema serikali kuweka mikakati ya kuwasaidia.

Akiwasilisha mada ya wazee, Salum Rashid Mohammed, alisema ni vyema serikali ikaandaa mikakati ya kukabiliana na ongezeko la wazee Zanzibar kwa kuwawekea mazingira bora ya maisha yao.

Wakizitaja changamoto hizo, walisema ni pamoja na kutokuwa na kanuni ya kuendesha mabaraza ya wazee kisheria, kutumia muda mrefu kulima kilimo chenye tija ndogo, kupewa kipaumbele kidogo katika sekta za huduma za kijamii ikiwamo afya, usafiri na huduma nyingine za nishati.

# Malengo ya milenia yalivyotekelezwa kielimu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIBU Mkuu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Fatma Gharib Bilali, amesema kuwa malengo endelevu ya (SDGS) namba nne ambayo yanahusu elimu yametoa kipaumbele sio tu upatikanaji wa elimu bali elimu bora yenye manufaa kwa watoto.

Akifunga mkutano wa tatu wa pamoja wa kutathmini maendeleo na changamoto za sekta ya elimu, alisema kwa upande wa Zanzibar watoto wote wana haki ya kupata elimu na ndiyo maana Rais wa Zanzibar, Dk. Mohamed Shein, ameondoa michango yote ya wazazi katika ngazi ya maandalizi, msingi na sekondari ili kila mtoto awe na haki sawa ya kupata elimu bora.

Alisema pia serikali ina wajibu wa kuhakikisha watoto wanajifunza katika mazingira mazuri na rafiki na ndiyo maana kila mwaka kuna ujenzi wa shule mpya pamoja na umalizaji wa ujenzi wa madarasa yaliyoanzishwa na wananchi.

"Wapo walimu waliobobea katika masomo yao na wana ari ya kujifunza hivyo Wizara ya Elimu inaendesha programu mbalimbali kwa walimu wa masomo yanayofundishwa," alisema.

Kadhalika kwa upande wa wanafunzi kwa kawaida, alisema wanafanyiwa tathmini na upimaji wa ubora wa elimu kupitia mitihani yao na kutaka kuwapo na njia nyingine mbadala katika tathmini kwa maendeleo ya elimu badala ya kutumia mitihani pekee.

Aliahidi kuwa maadhimio yaliyotolewa katika mkutano huo ni muhimu kwa maendeleo ya watoto hivyo atayafikisha katika ngazi za juu za serikali kufanyiwa kazi.

Pia alisema kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, itaendelea kusimamia sera na mipango ya elimu, mafunzo ya walimu, mitaala, ubora wa elimu na uwekaji viwango na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala ya Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itaendelea na jukumu la kusimamia uendeshaji wa shule za maandalizi na msingi kupitia mfumo wa ugatuzi wa madaraka kwenda katika serikali za mitaa.

"Napenda kuwahakikishieni kuwa Wizara ya Elimu itaendelea kufanya kazi kwa karibu na mfumo huu wa ugatuzi katika kuimarisha elimu kama sekta," alisema.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Radhia Rashid Haroub, alisema licha ya mafanikio makubwa yaliyopatika katika sekta ya elimu, bado kuna changamoto mbalimbali ikiwamo uchakavu wa majengo ya shule yaliyojengwa kwa miaka mingi.

# Wazabuni korosho wapewa siku tatu

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ametoa siku tatu kwa wazabuni walioshinda kununua korosho kulipa fedha benki na watakaokaidi watalipia fedha hizo kwa Kamanda wa Polisi Mkoa.

Ndikilo alitoa agizo hilo juzi Mjini Kibaha katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa huo.

Alisema, ifikapo kesho kama hakuna atakayekuwa ameingiza fedha benki, atahakikisha anafikisha majina yao kwa Kamanda wa Polisi wa mkoa huo ili awashughulikie.

"Fedha za wakulima zinatakiwa zilipwe, wale walioshinda zabuni na hadi sasa hawajaingiza fedha benki, siku tatu zikipita watapigiwa simu na RPC na watatakiwa kwenda Polisi na cheki si vinginevyo," alisisitiza Ndikilo.

Aidha, aliwataka wakuu wa wilaya ikiwezekana kutumia dola kuhimiza wakulima kusafisha mashamba ya korosho daraja la kwanza na la pili ambayo soko lake ni kubwa.

Kuhusiana na korosho zilizopo kwenye ghala hadi sasa, Ndikilo alisema wanasubiri Waziri wa Kilimo atembelee na kujionea hali halisi na baadaye watajadili njia ya kuziuza ili wakulima wapate fedha zao.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Pwani (CORECU) wa korosho, Rajabu Ng'onoma, alisema hali ya utunzaji wa mashamba ya korosho katika Mkoa huo hairidhishi, hivyo wakulima wanatakiwa kuelimishwa umuhimu wa kusafisha mashamba yao. Rajabu alibainisha kuwa hadi sasa tani 3,700 za korosho bado zipo kwenye ghala zikisubiri wanunuzi.

Katibu Tawala Msaidizi (uchumi na uzalishaji), Shangwe Twamala, alisema, katika msimu wa korosho 2019/2020 ambao ulianza Novemba 27, kwa kufungua mnada Wilaya ya Mkuranga, matarajio yalikuwa ni kununua kilo 26,096,000 toka katika Halmashauri zote tisa za Mkoa wa Pwani.

Twamala alisema hadi Februari, kiasi cha kilo 8,958273 zilikuwa zimenunuliwa na wanunuzi toka kwa wakulima kupitia CORECU.

Alisema hadi sasa mkoa huo una kilo 4,888,479 za korosho daraja la tatu ambalo halipo kisheria, ambalo limejitokeza zaidi msimu huu kutokana na mvua nyingi ambazo zimenyesha kwa muda mrefu, hivyo kuwazuia wakulima kuokota korosho kwa wakati na kuzianika.




Meneja Masoko wa Benki ya Exim, Mariam Mwapinga (kulia), akizungumza na wanahabari (hawapo pichani) wakati wa kuwatangaza washindi watano wa mwezi waliojishindia simu janja (smartphone) katika kampeni ya 'Chanja Kijanja na Exim Mastercard' jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Meneja Mwandamizi Huduma kwa wateja wa Benki hiyo, Frank Matoro (katikati) na Mkuu wa Idara ya Mauzo ya Kidigitali, Paritosh Babla. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Washindi wengine droo Exim watajwa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imetangaza washindi watano wa mwezi katika kampeni yake ya 'Chanja Kijanja na Exim Mastercard'.

Kampeni hiyo inalenga kuhamasisha wateja wa kutumia kadi zao za Mastercard katika manunuzi ya mtandaoni au kufanya malipo kupitia mashine za malipo (POS) katika maduka mbalimbali na maeneo mengine nchini.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya kuwatangaza washindi wa droo ya kwanza wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam, Meneja Mwandamizi Huduma kwa wateja benki ya Exim, Frank Matoro, aliwataja washindi hao ni Fahim Mohamed (Dar es Salaam), Baraka Rom Kimaro (Dar es Salaam), Hendrick Hopley (Arusha), Humphrey Henry (Mbeya) na Amani Makungu (Zanzibar) ambao kila mmoja atazawadia simu janja (smartphone).

"Mpaka sasa wateja 40 wameshajishindia vocha za manunuzi zenye thamani ya Sh. 50,000 kila mmoja na zinaendelea kutolewa kila wiki. Pia tunatoa zawadi kama hizi za leo za simu janja kwa washindi watano kila mwezi hadi mwisho wa mwezi Aprili, 2020 kwani ndio tutakuwa tunafika kilele cha kampeni yetu," Matoro.

"Katika kuhitimisha kampeni hii tutatoa zawadi kubwa zaidi kwa washindi watatu ambapo mshindi wa kwanza ataenda Dubai, mshindi wa pili ataenda Cape Town, Afrika Kusini na wa tatu ataenda visiwa vya Zanzibar. Washindi hao pamoja na wenza wao watagharamiwa gharama zote ikiwamo visa, tiketi ya ndege pamoja na pesa za matumizi," alifafanua.

Kwa mujibu wa Matoro, kampeni hiyo inayoendelea ikishirikiana na Mastercard ilianza katikati ya Februari, 2020 na kwamba ipo wazi kwa wateja wote wanaomiliki kadi za Exim Bank MasterCard, pamoja na wateja wote ambao wameomba au wataomba kadi mpya katika kipindi cha kampeni.

# NIT kuanzisha mafunzo utengenezaji meli

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

KUTOKANA na nchi kutokuwa na wataalamu (wahandisi) wenye uwezo wa kujenga meli, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kinatarajia kuanza kutoa mafunzo ya stashahada ya ujenzi wa meli sambamba na Shahada ya kwanza ya Usanifu wa meli kwa wanafunzi watakaokuwa tayari kusoma kozi hizo.

Hayo yalibainishwa jijini Mwanza na Mkuu wa Chuo NIT, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), Prof. Zacharia Mganilwa, wakati wa ziara ya mafunzo ya wajumbe wa Baraza la Uongozi wa chuo hicho ya kutembelea MSCL na kujionea namna wataalamu kutoka Korea wakitekeleza miradi ya ujenzi wa chelezo, meli mpya pamoja na ukarabati wa meli ya Mv. Victoria na Mv. Butiama.

Prof. Mganilwa, alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika miradi hiyo minne walio tembelea, hivyo ili iwanufaishe watu, kuna uhitaji wa kuzalisha rasilimali watu katika masuala ya usafiri wa meli ambao wana taaluma ya kutosha na weledi.

Alisema, kutokana na ombwe la upungufu wa wataalamu wazawa katika kazi hizo zinazoendelea wameweka mipango kwa mwaka wa masomo 2020/2021 kuanza kufundisha kozi ya utengenezaji na usanifu wa meli ambapo wanategemea kusaili wanafunzi 50 wa stashahada ya ujenzi wa meli, huku 30 wa usanifu wa meli ili kuzalisha wataalamu wazawa wenye uwezo wa kuhudumu katika sekta hiyo.

Pia alisema, hadi sasa wameona kuna fursa kubwa katika usafiri wa njia ya maji ambapo serikali imeweka mipango ya kujenga meli ndani ya Ziwa Victoria na baadaye Ziwa Tanganyika na pia katika Bahari ya Hindi, huku shughuli zote hizo zitahitaji wataalamu, hivyo kama taifa litakuwa limeandaa wataalamu wake wa ndani basi miradi hiyo itakuwa na tija zaidi kwa wazawa.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa MSCL, Eric Hamissi, alisema miradi hiyo inatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani, ambayo italeta mapinduzi makubwa kwenye sekta ya majini.

HABARI KIMATAIFA

# Waziri afya Uingereza akutwa na corona

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI wa Afya nchini Uingereza, Nadine Dorries amekutwa na maambukizi ya virusi vya Corona, baada ya kupimwa jana.

Dorries ambaye pia ni mbunge wa Chama Cha Conservative nchini humo, anakuwa mbunge wa kwanza kugundulika na maambukizi ya ugonjwa huo.

Hata hivyo, alichukua tahadhari zote baada ya kubaini kuwa ameathirika kwa kuamua kujifungia karantini nyumbani kwake.

Tukio hilo limetokea wakati kukiwa na taarifa ya kifo cha mtu wa sita kutokana na virusi vya corona nchini Uingereza ambako kuna matukio ya watu 382 kuambukizwa.

**Haijulikani ni vikao vingapi Dorries alihudhuria Westminster au katika jimbo lake hivi karibuni.**

Mtu aliyepoteza maisha hivi karibuni ni mzee mwenye umri wa miaka 80 ambaye alikuwa na changamoto za kiafya.

Wakati huohuo, hospitali kuu Uingereza imesema inaboresha uwezo wake wa kuwapima watu, wakati idadi ya maambukizi ikitegemewa kuongezeka. Hiyo inamaanisha kuwa vipimo 10,000 kwa siku vitakuwa vinafanyika na kwamba kwa saa watu 1,500 wataweza kupimwa. Pia itawezesha kupatikana kwa majibu ya vipimo ndani ya saa 24.

Dorries, mbunge wa Bedfordshire ya kati, alisema kuwa idara ya afya imeanza kuwafuatilia watu waliokuwa karibu naye na ofisi yake ya bunge inafuatilia hilo kwa karibu.

Dorries alieleza kwenye ukurasa wake wa kijamii wa Twitter kuhusu hali aliyokuwa nayo, lakini akielezea hofu aliyonayo kuhusu mama yake mwenye miaka 84 anayeishi naye ambaye naye ameanza kukohoa.

Haijulikani ni vikao vingapi Dorries alihudhuria Westminster au katika jimbo lake hivi karibuni.

Idara ya afya imesema alianza kuonesha dalili siku ya Alhamisi juma lililopita -alipohudhuria dhifa iliyofanyika Downing Street iliyohodhiwa na Waziri Mkuu, Boris Johnson- na akawekwa karantini tangu siku ya Ijumaa.

Lakini hakuna taarifa yoyote kama Waziri Boris Johnson alifanya vipimo vyovyote, au atapimwa sasa.

Mawaziri wote wa afya, akiwamo Waziri Mkuu wa afya, Matt Hancock, watafanya vipimo, sambamba na maofisa wengine ambao walikaribiana na Dorries.

Hancock aliandika kwenye ukurasa wake wa twitter kuwa alifanya sahihi kwa kujitenga nyumbani na alimtakia afya njema.

Alisema: "Ninaelewa kwanini watu wana wasiwasi kuhusu ugonjwa huu. Tutafanya vyovyote tunavyoweza kuwaweka watu katika hali ya usalama." **BBC**



Mji wa Kinshasa ambao mtu mmoja ameshagundulika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: RFI**

## Mtu wa pili athibitishwa kupona ugonjwa Ukimwi

**LONDON,** Uingereza

MWANAUME mmoja kutoka Jiji la London Uingereza, Adam Castillejo amethibitishwa kuwa ndiye mtu wa pili kupona virusi vya HIV vinavyosababisha Ukimwi, wamesema madaktari.

Castillejo bado hajapatikana na virusi baada ya kukaa siku 30 bila kumeza dawa za kupunguza makali ya virusi vya HIV zinazofahamika kama anti-retroviral.

Imeelezwa kuwa Castillejo hakupona kutokana na dawa za HIV bali kwa tiba ya uboreshaji wa seli alizopewa kwa ajili ya matibabu ya saratani ambayo alikua nayo, limeripoti jarida la kitabibu la the Lancet linaloandika juu ya HIV.

Mwaka 2011, Timothy Brown, kutoka Jiji la Berlin alikua ni mtu wa kwanza kuripotiwa kuwa amepona HIV baada ya kupita miaka mitatu na nusu alipopata tiba sawa na hiyo.

Upandikizaji wa seli zinazoboresha seli nyingine ama Stem-cell transplants unaonekana kuzuia virusi hivyo kuendelea kuwa na uwezo wa kuzaana mwilini kwa kuchukua nafasi ya mfumo wenyewe wa seli za kinga za mwili na kutumia seli za mtoaji ambazo zinazuia maambukizi ya HIV.

Castillejo ambaye sasa ana umri wa miaka 40 aliamua kujitangaza kuwa hana virusi vya HIV katika damu yake, maji maji ya mwili au nyama za mwili wake, madaktari wake walisema. **BBC**

## Watu sita kuwania urais Burundi

**BUJUMBURA,** Burundi

KATI ya wagombea 10 waliowasilisha maombi yao Tume Huru ya Uchaguzi (CENI) kuwania nafasi ya urais nchini Burundi, ni sita tu waliopitishwa.

Mwenyekiti wa CENI, Dk. Pierre Claver Kazihise alisema wagombea ambao majina yao hayajapitishwa wana siku mbili za kukata rufaa.

Hatua hiyo imewashangaza wengi baada ya kusikia jina la aliyekua Rais wa Burundi, Domitien Ndayizeye katika kipindi cha mpito kati ya mwaka wa 2003 na 2005 kuondolewa.

Ndayizeye kwa sasa ni kiongozi wa muungano wa Kira Burundi unaoundwa na vyama vidogo vya upinzani. Sababu za kukataliwa kwa jina lake bado hazijajulikana.

Wagombea wengine ambao majina yao hayajakubaliwa ni viongozi wa vyama vidogo vitatu vya siasa: Anicet Niyonkuru wa chama cha CDP, Jaques Bigirimana wa chama cha FNL na Valentin Kavakure wa chama cha FPN. Wagombea hao wote sasa wana siku mbili za kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Tume ya Uchaguzi kwa Mahakama ya Katiba.

Jina la kiongozi wa upinzani, Agathon Rwasa, limekubaliwa hivyo ataweza kuwania katika uchaguzi wa urais wa Mei 20, lakini kiongozi huyo wa zamani wa kihistoria wa FNL atapeperusha bendera ya chama cha CNL.

Chama chake kilisajiliwa mwaka mmoja uliopita, lakini leo inachukuliwa kama chama cha pili chenye wafuasi wengi nchini Burundi.

Rwasa atakuwa mshindani mkuu wa Jenerali Évariste Ndayishimiye, atakayepeperusha bendera ya chama tawala cha CNDD-FDD katika uchaguzi huo. **RFI**

## Askofu ajiuzulu kupisha uchunguzi dhidi yake

**CANBERRA,** Australia

MMOJA wa maaskofu waliohudumu muda mrefu zaidi kwenye Kanisa Katoliki nchini Australia, Christopher Saunders amejiuzulu wadhifa wake jana.

Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi nchini humo zinaeleza kuwa wanamchunguza askofu huyo kwa tuhuma za udhalilishaji kingono ambazo anatuhumiwa nazo.

Askofu Saunders aliyeongoza dayosisi ya Broome iliyo magharibi mwa Australia anaripotiwa kuamua mwenyewe kukaa kando kupisha uchunguzi dhidi yake.

Hata hivyo, Askofu Saunders hakutaka kuongea zaidi kuhusu tuhuma inayomkabili zaidi ya kuamua kukaa pembeni.

Askofu Mkuu, Timothy Costelloe alisema uamuzi huo umefanywa kutokana na hali iliyojitokeza na kwa kulinda dhamana ya kichungaji na wajibu wa kidini wa dayosisi hiyo. **DW**

# Benki UBA yatambua mchango wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wanawake wa UBA Tanzania wamesherehekea Siku ya Kimataifa ya Wanawake kwa kuwaalika wateja wanawake kushiriki kifungua kinywa katika hafla iliyoandaliwa na benki hiyo ikiwa ni kutambua mchango wa wanawake katika jamii.

Katika kuadhimisha siku hiyo maalum kwa wanawake, uongozi wa UBA Tanzania pia ulitembelea wanawake wenye matatizo ya fistula katika Hospitali ya CCBRT na kuchangia vifaa vya matibabu, pampas za wanawake watu wazima.

Mbali na hilo, pia walitoa mafuta ya kujipaka, sabuni za kufulia, dawa za meno, miswaki, sahani na mabakuli, vikombe vya chai, kanga, vyandarua, dawa za mbu za kupuliza, mabeseni, kandambili na taulo za kike.

Wanawake wa UBA Tanzania walitekeleza jukumu lao muhimu kwa kuwawezesha pia wanawake wengine kupitia shughuli mbalimbali zilizofanywa na benki hiyo kusaidia wanawake na wanafunzi wa kike kwa kuwapatia taulo za kike, taulo za wajawazito na vifaa vingine.

Katika hafla ya kuadhimisha siku hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi, timu ya viongozi wanawake wa benki hiyo na wafanyakazi wengine wanawake walitoa elimu na kujadili masuala mbalimbali wanayopitia wanawake na mwisho walipata kifungua kinywa na wateja wote wanawake walioalikwa.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa Benki hiyo, Flavia Kiyanga, aliwataka wanawake kujishughulisha katika shughuli za ujasiriamali na shughuli nyingine za biashara ili kujimarisha kiuchumi.




Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga (kushoto), akisalimiana kwa kugonganisha miguu na Mwenyekiti wa wafanyabiashara Mkoa wa Lindi, Hamisi Livembe, wakati wa uzinduzi wa Klabu ya Biashara ya Benki ya NBC mkoani humo juzi. Wengine ni Meneja wa Bidhaa na Huduma za Kifedha wa benki hiyo, Jonathan Wilson (wa pili kushoto) na Meneja wa Tawi NBC mkoani humo, Iovin Mapunda. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Afungwa miaka 10 kuua bila kukusudia

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara, imemhukumu kifungo cha miaka 10 jela mkazi wa Tarafa ya Kipatimu,Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, Omari Kawaida Kipengele (26), baada ya kupatikana na hatia ya kuua bila ya kukusudia Mwanaidi Kipengele.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji wa Mahakama hiyo, Paul Joel Ngwembe, baada ya mshtakiwa kukiri kosa.

Baada ya mshtakiwa kukiri kosa, wakili wake, Issa Chiputula, aliiomba mahakama hiyo kutompatia mteja wake adhabu kubwa, kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza, bado kijana anayehitaji kulitumikia Taifa na amekaa rumande kwa muda mrefu.

Wakili huyo alidai kuwa mshtakiwa amejutia kitendo alichokifanya cha kuua bila ya kukusudia.

Nae, Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, aliiomba Mahakama hiyo kumpatia mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya aina hiyo.

Jaji Ngwembe akitoa hukumu katika shauri namba 18/2018, huku akitumia vifungu vya Sheria 195 na 198, alisema amesikiliza maombi ya pande zote mbili, lakini kutokana na kosa alilolifanya anamhukumu Omari Kipengele kutumikia kifungo cha jumla ya miaka (10) Gerezani.

Awali ilidaiwa Mahakamani hapo na mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba alidai kuwa Oktoba 25/2017, huko Kipatimu,Wilaya ya Kilwa katika Mkoa wa Lindi,mshitakiwa alimuuwa bila ya kukusudia mpenzi wake Mwanaidi Kipengele, kufuatia mwanamke huyo kushindwa kutekeleza kile walichokubaliana.

# Wazazi walalamikia mtuhumiwa kubaka mtoto

**Mwandishi Wetu,** PEMBA

NASSOR Issa Nassor (21), mkazi wa Kizimbani Wete kisiwani Pemba, anatuhumiwa kumbaka mtoto wa miaka saba.

Mtuhumiwa anadaiwa kutenda kosa hilo eneo la Kiwani katika Shehia ya Mchangamdogo Wilaya ya Wete.

Mama wa mtoto huyo alisema katika mtaa wao wana tabia ya kukaa nje inapofika jioni kwa ajili ya kuzungumza, huku watoto wao wakicheza karibu yao.

"Ghafla nilimuona jirani yangu anakuja kwa kasi huku amemkamata mwanangu mkono, alipofika tu aliniambia 'muulize mwanao anatoka wapi?... Ndipo nikaanza kumuuliza," alisema mama huyo.

Alieleza kuwa aliambiwa na mtoto wake kuwa alipita mtuhumiwa na kumwambia amchukulie mzigo wake na kumjibu kuwa hauwezi.

"Aliniambia kuwa baada ya kukataa alimchukua kwa nguvu na kumtia matambara ya mdomo na kwenda nae miembeni kumbaka, hapo tukaanza kumtafuta mtuhumiwa na tulipomuona tukampeleka kituo cha Polisi Mchangamdogo," alieleza mama huyo.

"Alikuwa hamjui kwa jina kwa sababu sio mtu wa hapa, isipokuwa alioa tu hapa Kiwani, lakini mke alimuacha, ingawa huwa ana tabia ya kuja...mwanangu aliniambia kutokana na nguo alizovaa mtuhumiwa huyo," alisema.

Bibi wa mtoto huyo alisema kuwa, tukio hilo lilitokea Januari 10, mwaka huu, ambapo walimpeleka mtoto huyo hospitali kisha kuripoti kituo cha Polisi.

Alisema kinachomshangaza ni kuwa toka siku walioripoti Polisi hawajawahi kuitwa na wala hawajaona askari kwenda kufanya upelelezi zaidi ya siku ya mwanzo tu, jambo ambalo linawatia wasiwasi kuhusu kesi.

Bibi huyo alisema kinachomuhuzunisha ni kuona mtoto huyo anashindwa hata kutoka nje kucheza na wenziwe kutokana na kuona aibu, hivyo alitaka Jeshi la Polisi limkamate mtuhumiwa.

"Serikali iwachukulie hatua wale wote wenye tabia hii kwa sababu wanawakosesha watoto haki zao za msingi, kwani wakimuachia utakuwa ni uonevu na wataendelea kuwadhalilisha," alisema.

Baba wa mtoto huyo, alisema kuwa, siku ya tukio alikuwa nje ya kisiwa cha Pemba akifanya shughuli zake za kibiashara, na aliporudi nymbani kwake alipewa taarifa ya mtoto wake kufanyiwa ukatili huo.

"Tangu siku niliporudi nafuatilia kesi hiyo kituo cha Polisi mpaka hivi leo narudi huko, ila majibu ninayopewa yananikatisha tamaa," alisema.

Naye Mratibu wa Shehia ya Mchangamdogo, Mbeu Makame Bakar, alisema matukio ya udhalilishaji yanaongezeka kwa kasi, kwani kuanzia Januari hadi Febuari 15 amepokea kesi tatu, mbili za ujauzito wa watoto wa miaka 14 na 17 na nyingine ni hiyo.

Aliwataka wazazi na walezi kuwa waangalifu kwa watoto wao na wanapoona wameondoka muda mrefu, wawafuatilie ili wajue walipo, kwa lengo la kuwaepusha kufanyiwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji.

Mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA) kisiwani Pemba, Fat-hiya Mussa Said, aliwataka wazazi wa mtoto huyo kuepuka rushwa muhali na wawe mstari wa mbele kutoa ushahidi wanapohitajika kwenye vyombo vya sheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alithibitisha kuripotiwa kwa tukio hilo, na kusema kwamba mtuhumiwa amekamatwa na wanaendelea na upelelezi.

"Tukio hilo liliripotiwa kituo cha Polisi Wete, mtuhumiwa tumemkamata na upelelezi utakapokamilika atafikishwa mahakamani," amesema kamanda huyo.

Jumla ya kesi tisa (9) za udhalilishaji zikiwamo za kubaka tano zimeripotiwa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba kuanzia Januari hadi Februari mwaka huu.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BEATRICE MOSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 985 DFV TOYOTA PASSO.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MBD/RB/572/2020.

115664602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEORGE P. MABALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 352 ASB TOYOTA LANDCRUISER PRADO.** Chassis namba **KZJ 780005245.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/BUG/RB/2220023/2020.**

2155665302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JONESIA ADOLPH BANYENZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 508 AKH DAIHATSU ROCKY.** Chassis namba **F300S009557.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/BUG/RB/219973/202**

115665402

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**(JUDICIARY)**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI NA. 1/2020**
**MDAI........NEEMA JOSEPH MNYENYELWA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA:........EMMANUEL BONZA BARIDI**
**KWA: EMMANUEL BONZA BARIDI**
**POPOTE ULIPO.**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba Mdai amefungua madai dhidi yako,nakala ya madai hayo inapatikana katika Mahakama hii.

Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 26/03/2020 saa 2:00 asubuhi na unatakiwa kuwepo,au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya madai haya.

Zingatia kwamba kutokufika kwako tarehe hiyo,Shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena,na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26 mwezi 2 mwaka 2020.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI MOROGORO

115665102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;77/2020**

**Ombi la ZOO NASSOR BINZOO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ABDALAH NASSORO BINZOO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 01/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/03/2020

Sahihi ya Hakimu

MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANOWATANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;75/2020**

Ombi la **EDNA NYENGA MANASE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **STANSLAUS MISIGARO KIGADYE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 13/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/03/2020.

1566647

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;73/2020**

**Ombi la SALUM RAJABU TONYOKE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu AMINA SALUM TONYOKE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/03/2020.

HAKIMU

MOROGORO

115665002


***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# CHELSEA YAMNYATIA KIPA WA BARCELONA

**LONDON,** England

CHELSEA imeendelea na harakati zake za kutafuta kipa mpya na sasa imemgeukia Marc-Andre Ter Stegen wa Barcelona, huku kukiwa na ripoti kuwa Frank Lampard yuko tayari kumuuza Kepa Arrizabalaga kwenda Real Madrid.

Licha ya kuhusishwa na Gianluigi Donnarumma wa AC Milan na Andre Onana wa Ajax, lakini pia Chelsea inatajwa kuisaka saini ya Ter Stegen anayedaiwa kuwa mbioni kuondoka Nou Camp baada ya kuripotiwa kwamba amegombana na Lionel Messi.

Inasemekana Messi amewataka viongozi wa Barcelona kumuuza Ter Stegen, huku pia akiwataka viongozi wa timu hiyo kumfuata Neymar mwenye thamani ya pauni milioni 198, hivyo Lampard anataka kutumia nafasi hiyo kumnasa kipa huyo.

Wakati Chelsea ikiwekeza nguvu zake kwenye kusaka saini ya Ter Stegen, inadaiwa kuwa Real Madrid imeanza harakati za kuisaka saini ya Kepa ambaye anaonekana kupoteza imani ya Kocha Lampard.

# Mourinho: Hakuna timu itahimili majeruhi Spurs

**LONDON,** England

JOSE Mourinho anaamini hakuna timu duniani ingeweza kuhimili majeruhi iliyonayo Tottenham kwa sasa.

Tottenham imeondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi Jumanne baada ya kufungwa 3-0 na RB Leipzig kwenye mchezo wa pili wa hatua ya 16-bora.

Makosa kutoka kwa Hugo Lloris yalimsaidia Marcel Sabitzer kuiweka mbele Leipzig kwa mabao mawili ya kipindi cha kwanza kabla ya Emil Forsberg aliyetokea benchi kuipa ushindi wa uwiano wa 4-0.

Hiyo inamaanisha kwamba matumaini ya Spurs kushinda taji msimu huu yamefikia mwisho.

Tottenham imekuwa haina huduma ya Son Heung-min tangu Februari baada ya kuvunjika mkono, huku mshambuliaji Harry Kane akiwa majeruhi tangu mwaka mpya.


Beki Ben Davies alikosa safari ya kwenda Leipzig kutokana na kuumia misuli na Davinson Sanchez pia hakuwapo, huku safu ya ulinzi ya Spurs ikionekana kupwaya.

Alipoulizwa na waandishi wa habari baada ya mchezo wa juzi, Jumanne kama majeruhi yamechangia matokeo mabaya kwa timu yake Mourinho, alijibu: "Ni ngumu kuzungumzia kuhusu majeruhi, lakini unataka nizungumze kuhusu vitu ambavyo vipo wazi?

"Vipo kama Leipzig wangekuwa hawana Sabitzer, (Patrik) Schick, (Timo) Werner, unafikiri wangeshinda kama hivi?

"Ingewezekana Liverpool ikafanya vizuri bila (Mohamed) Salah, (Sadio) Mane, (Jordan) Henderson au Barcelona bila (Antoine) Griezmann, (Lionel) Messi, (Luis) Suarez na (Gerard) Pique.






# *Mpango wa Pogba kusepa bado upo*

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba ameripotiwa kudai mpango wake wa kutaka kutimka Old Traffod mwishoni mwa msimu huu uko pale pale, licha ya kutarajiwa kurejea kucheza na nyota mpya, Bruno Fernandes.

Mfaransa huyo, ambaye amekuwa nje ya uwanja tangu Desemba kutokana na majeraha ya 'enka', amedhamiria kurejea kikosini ili aungane na Bruno aliyetua akitokea Sporting.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Tuttosport, supastaa huyo mwenye umri wa miaka 26, bado anataka kuwahama 'Mashetani Wekundu' hao mwishoni mwa msimu huu ili atimkie Juventus au Real Madrid.

Hatima ya Pogba imekuwa mjadala kwa muda wote wa msimu licha ya staa huyo kutumia muda mrefu wa msimu akiwa nje ya uwanja akiuguza majeraha ya enka. Pogba pia alikosa mechi ya karibuni ya Man United waliyoshinda 3-0 kwenye Kombe la FA dhidi ya Derby County.

HABARI MICHEZO

# GUARDIOLA: STERLING ATARUDIA UBORA WAKE



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anajiamini Raheem Sterling atarudi kwenye ubora wake wa kufunga mabao baada ya kuwa kwenye kipindi kigumu hapo Manchester City.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England, Sterling alifurahia mwanzo mzuri wa msimu kwa kufunga hat-trick dhidi ya West Ham na Atalanta.

Hata hivyo, sasa hajafunga katika mechi 12, huku mabao yake 20 aliyofunga kwenye mashindano yote mara ya mwisho akifunga mawili wakati wakishinda 3-2 dhidi ya Wolves Desemba.

Lakini sasa Guardiola anaamini kwamba Sterling atarudi kwenye ubora wake hivi karibuni.

"Ni mchezaji mwenye kiwango cha kuvutia, najua kwamba hajafunga muda mrefu, lakini atafunga tu," alisema.

"Aliumia kwa wiki mbili au tatu na wakati mwingine unahitaji muda zaidi wa kupona ili kurudi kwenye ubora wako.

"Naamini kwamba Sterling ataanza kufunga tena, wakati huu haujawa mzuri kwake, lakini nina imani kubwa kwamba atakuwa bora kwenye kufunga."

## Liver wamwongezea kasi Werner

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imeripotiwa kwamba wana mpango wa kumsajili Timo Werner na kumrudisha kwa mkopo katika klabu yake RB Leipzig mwishoni mwa msimu huu.

Werner mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na vinara hao wa Ligi Kuu ya England baada ya mshambuliaji huyo kuwa na kiwango cha kuvutia kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Lakini kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani atasajiliwa pale Liverpool kwa ajili ya msimu wa 2020-21, hatakuwa kwenye mipango yao ya awali.

Liverpool wanaweza kumrudisha kwa mkopo Werner kule RB Leipzig kwa ajili ya msimu ujao kama watafanikiwa kuipata saini yake, kwa mujibu wa gazeti la Bild.

Werner amefunga mabao 27 katika mechi 35 alizocheza msimu huu, na amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa za Ulaya.

Mjerumani huyo ambaye ameichezea timu yake ya taifa jumla ya mechi 29, alisema mwezi uliopita kwamba anajisikia fahari kutakiwa na Liverpool.



## Wan-Bissaka beki bora - Carragher



**LONDON,** England

BEKI Aaron Wan-Bissaka wa Manchester United, ametajwa ndiye beki bora duniani kwa sasa.

Kauli hiyo imetolewa na mchambuzi nguli Jamie Caragher ikiwa ni muda mfupi baada ya kucheza kwa kiwango bora dhidi ya Manchester City.

Wan-Bissaka alimpa ulinzi mkali winga msumbufu wa Man City Raheem Sterling katika mchezo huo walioshinda mabao 2-0.

Carragher alisema Wan-Bissaka ni beki bora wa kulia duniani mwenye uwezo wa kumkabili mshambuliaji ana kwa ana.

Usajili wa beki huyo aliyetua Man United kwa pauni milioni 50, umekuwa na manufaa kwa kocha Ole Gunnar Solskjaer.

"Ndio kulikuwa na mechi kali kati ya timu mbili za Manchester, lakini kulikuwa na kivumbi kingine kati ya Raheem Sterling dhidi ya Aaron Wan-Bissaka," alisema Carragher.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# CORONA YAWAZUIA PEP, ARTETA, EPL KUENDELEA

## Hatua zote muhimu zinachukuliwa na Premier League haina mpango wa kuahirisha...

**LONDON,** England

UONGOZI wa Ligi Kuu England (Premier League), umesema hauna mpango wa kuahirisha mechi yoyote baada ya jana, Jumatano kuahirisha mchezo kati ya Manchester City na Arsenal ikiwa ni kuchukua tahadhari ya kuenea kwa virusi vya corona 'coronavirus'.

**City ilikuwa iikaribishe Arsenal katika Uwanja wa Etihad ambapo ingeshuhudiwa Pep Guardiola akikutana na msaidizi wake wa zamani, Mikel Arteta anayeinoa Gunners kwa sasa, hata hivyo mchezo huo haukufanyika hapo Manchester kutokana na ushauri wa kitabibu.**

Uamuzi huo ulikuja "baada ya kuibuka taarifa kuwa wafanyakazi kutoka Arsenal waligusana na mmiliki wa Olympiacos na Nottingham Forest, Evangelos Marinakis, ambaye ametajwa kuwa na maambukizi chanya ya COVID-19."

Arsenal iliongeza kuwa wachezaji wao watajitenga nyumbani kwa siku 14, wakati viongozi wanne pia watabaki nyumbani hadi wiki mbili zitakapomalizika ambapo kuungana tena itakuwa ni hadi mara ya mwisho walipowasiliana siku 13 zilizopita.

Katika taarifa ya Premier League ilisema: "Tunatambua hili litasababisha usumbufu na kuwagharimu mashabiki waliopanga kuhudhuria mechi hiyo, lakini Arsenal, Manchester City na Premier League wamekubaliana kuwa taarifa fupi ya maambukizi ya Marinakis inamaanisha hakuna njia nyingine ila kuchukua muda wa kukamilisha tathmini sahihi ya hatari.

"Hatua zote muhimu zinachukuliwa na Premier League kwa sasa haina mpango wa kuahirisha mechi nyingine."

Kikosi cha Guardiola, City kitaikaribisha Burnley Jumamosi, wakati siku hiyo Arsenal yenyewe itasafiri kuifuata timu iliyopo katika ukanda wa kushuka daraja, Brighton and Hove Albion.

Italia imeathiriwa sana na corona mbali na China, hivyo kusababisha mechi zote za Serie A na shughuli zote za michezo kuahirishwa hadi Aprili 3, mwaka huu kufuatia watu zaidi ya 10,100 kuripotiwa kuambukizwa huku vifo vikiwa ni 600.

Zaidi ya watu 3,000 wamefariki kwa ugonjwa huo nchini China, wakati kumekuwapo na vifo sita na zaidi ya watu 380 walioripotiwa kuwa na maambukizi hayo nchini Marekani.

## ZISIKUPITE

### ATLETICO INAYE LACAZETTE

ATLETICO Madrid bado imebaki kuvutiwa na mshambuliaji Mfaransa Alexandre Lacazette, 28, kutoka Arsenal. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### BARCA NA MARTINEZ, WERNER

BARCELONA imemweka katika nafasi ya pili, mshambuliaji wa RB Leipzig na Ujerumani, Timo Werner, 24, katika orodha ya wachezaji inaowawinda majira ya joto akiwa nyuma ya straika wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez, 22. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### CORONA KUAHIRISHA EURO 2020

UEFA inazingatia kuahirisha michuano ya Euro 2020 kwa mwaka mmoja kwa sababu ya corona, kufuatia maombi ya mashirikisho kadhaa. ***(Tuttosport - in Italian)***

### ARSENAL KUMFUNGA SAKA

ARSENAL inajaribu kuhakikisha inampa mkataba wa muda mrefu winga Muingereza Bukayo Saka, 18, huku kukiwa na taarifa ya Manchester United kuvutiwa na kinda huyo. ***(Express)***

### FERGUSON AMVUTA JUDE UTD

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson anajaribu kuisaidia klabu hiyo mchakato wa kumsajili Jude Bellingham, 16, kutoka Birmingham na tayari amekutana na kiungo huyo pamoja na wazazi wake wakati walipotembelea uwanja wa mazoezi wa United Jumatatu. ***(Star)***

### SIDIBE ANOGEWA EVERTON

BEKI wa pembeni wa Monaco, Djibril Sidibe, 27, amesema anataka kuufanya mkataba wake wa mkopo hapo Everton kuwa wakudumu. ***(RMC Sport, via Liverpool Echo)***

### MBAPPE APIMWA CORONA

MSHAMBULIAJI Mfaransa Kylian Mbappe, 21, alipimwa kuangaliwa kama ana maambukizi ya corona kabla ya Paris-St Germain kuikaribisha Borussia Dortmund kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mkondo wa pili wa hatua ya 16-bora, na hajaambukizwa. ***(L'Equipe - in French)***

### ARSENAL NAYO KWA WHITE

ARSENAL inavutiwa na beki wa kati wa Leeds United anayeichezea kwa mkopo akitokea Brighton, Muingereza Ben White, wakati Liverpool, Manchester United na Leicester pia zikiwa tayari kuisaka saini ya mchezaji huyo. ***(Sun)***

### BATSHUAYI ANUKIA PALACE

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Michy Batshuayi, 26, anaweza kuwa njiani kuelekea kujiunga na Crystal Palace, wakati huu Mbelgiji huyo akiwa tayari kubaki klabu ya London atakitafuta nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza. ***(Star)***

### ZIDANE KUMPISHA POCHETTINO

Real Madrid inamatumaini ya kuzipa nafasi ya kocha Zinedine Zidane kwa kumtwaa kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino ama aliyewahi kuinoa Juventus, Massimiliano Allegri. ***(Marca - in Spanish)***

### LIVERPOOL KUMRUDIA DOKU

Liverpool bado inatumai kumsajili mshambuliaji Mbelgiji Jeremy Doku, 17, baada ya hivi karibuni mchakato wao wa kumsajili kinda huyo wa Anderlecht kushindikana. ***(Het Nieuwsblad, via Star)***

HABARI MICHEZO

# YANGA YATAMBA ZAMU YA KMC KUCHEZEA LEO

Na Saada Akida

BAADA ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya watani zao, Simba katika mechi iliyopita ya Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael amewaita mashabiki wa timu hiyo Uwanja wa Taifa leo kushuhudia KMC FC ikichezea kichapo kutoka kwao.

**Hata hivyo, Yanga itaingia uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare kwenye mchezo wa mzunguko wa kwanza dhidi ya timu hiyo ya Manispaa ya Kinondoni.**

Lakini Eymael alimeambia Nipashe jana kuwa wachezaji wake wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo, na watapambana kuhakikisha wanapata matokeo chanya kwa kuwa kila mmoja anatambua majukumu yake na ana imani kila kitu kitakwenda sawa.

"Malengo yetu ni kupata alama muhimu katika mechi zetu zote, tumefanya maandalizi ya kutosha, nina imani kila kitu kitakuwa sawa ni suala la kusubiri na kuona itakuaje," alisema.

Alisema mikakati yake ni kufanya vizuri kwa kila mechi na kuvuna pointi ili kuweza kupambana kuiondoa Azam FC katika nafasi ya pili.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Haruna Hererimana, alisema amejiandaa kwenda kutafuta pointi tatu muhimu kwa ajili ya kujiweka katika mazingira mazuri katika msimamo wa ligi hiyo.

Alisema wapo katika nafasi mbaya, hivyo wanahitaji kupambana kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao ukiwamo dhidi ya Yanga.

"Tulifanyia kazi mapungufu yetu, tukashinda mchezo na Mbao, kesho (leo), tunaingia uwanjani dhidi ya Yanga kutafuta alama muhimu, tunajua utakuwa mchezo wa ushindani na kila mmoja wetu anafahamu tunataka alama tatu," alisema Hererimana.

KMC inashika nafasi ya tatu kutoka mkiani ikiwa tayari imecheza michezo 27 na kujikusanyia pointi 27, huku Yanga iliyoshuka dimbani mara 25 IKIWA NA ALAMA 50 KATIKA NAFASI YA Tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo kinara ni Simba yenye pointi 68 kabla ya mchezo wao wa jana dhidi ya Singida United.



Winga wa Azam FC, Iddi Kipagwile (kushoto), akifanyiwa madhambi na wachezaji wa Ruvu Shooting katika mchezo wa Ligi Kuu uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Azam ilishinda 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam kurejesha Ligi Kuu Chamazi

Na Saada Akida

UONGOZI wa Azam FC umesema wiki ijayo uwanja wao wa Chamazi utakuwa umekamilika na kuanza kutumia katika michezo yao iliyobakia ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Uwanja wa Azam ulikuwa katika ukarabati mkubwa wa kubadili nyasi za bandia, hali hiyo iliyowalazimu kucheza dimba la Taifa na Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema baada ya mapumziko ya kupisha mechi za kimataifa, timu hiyo itaanza kutumia uwanja huo kwenye michezo yao ya Ligi Kuu.

Baada ya mechi za Ligi Kuu kesho, ligi hiyo itasimama na wachezaji watajiunga na timu zao za taifa kwa ajili ya kujiandaa mechi za kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021, zitakazochezwa kati ya Machi 23-31.

Na baada ya mechi hizo, ligi hiyo itaendelea kusimama fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) zitakazofanyika Cameroon kuanzia Aprili 4-25, mwaka huu.

Popat alisema waliathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na kukosa kutumia uwanja wao huo katika michezo yao ya ligi kwa kipindi ukiwa katika ukarabati huo.

"Uwanja wetu upo katika hatua ya mwisho na wiki ijayo utakuwa umekamilika, imani yetu kubwa ni kwamba baada ya CHAN tunarudi kucheza uwanja wetu wa Azam," alisema Popat.

Naye kocha wa timu hiyo, Aristica Cioaba alisema kutumia Uwanja wa Taifa na Uhuru kumewaathiri kutokana na kikosi chake kufanya mazoezi tofauti na sehemu nyingine.

"Nimefurahi kupata mapumziko ya wiki tatu, vijana wangu wanapata muda wa kupumzika kutokana na ratiba iliyokuwa, lakini nafurahi baada ya mapumziko hayo tutatumia uwanja wetu kumalizia ligi," alisema Cioaba.

## Tambwe atamani kurejea Ligi Bara

Na Shufaa Lyimo

HUKU akisifu kikosi cha Taifa Stars kilichoitwa na Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, mshambuliaji wa zamani wa Simba na Yanga, Hamisi Tambwe (pichani chini) amesema yupo tayari kurejea Ligi Kuu Bara endapo atapata timu sahihi ya kujiunga nayo.

Juzi, Ndayiragije aliita kikosi cha wachezaji 35 watakaoingia kambini kujiandaa na mechi za kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021 na fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) zinazotarajiwa kuanza April 4-25, mwaka huu nchini Cameroon.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya barua pepe, Tambwe alisema Etienne ametumia wigo mpana kwa kuita kikosi hicho ambacho kinaingia kambini leo.

"Kocha ameita kikosi kizuri ameweza kuingiza wachezaji ambao hawakuitumikia timu hiyo kwa muda mrefu naamini watafanya vizuri," alisema Tambwe.

Akiizungumzia Yanga, alisema timu hiyo kwa sasa imebadilika kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na kipindi alichokuwa anaitumikia timu hiyo.

"Yanga sasa hivi inacheza vizuri tofauti na kipindi chetu, vilevile kocha wao Luc [Eymael] anajua kucheza na akili ya kila mchezaji," alisema.

Kuhusu kurejea kucheza soka nchini, alisema: "Nipo tayari kurudi kucheza Tanzania kikubwa ni maslahi kwa sababu mpira ndio kazi yangu."



## Mgunda: Sababu kuichapa Lipuli

Na Shufaa Lyimo

KOCHA Mkuu wa Coastal Union Juma Mgunda, amesema ushindi walioupata wa mabao 2-0 dhidi ya Lipuli FC juzi, umetokana na wachezaji wake kufuata kwa makini maelekezo aliyowapa.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana kutoka mkoani Tanga, Mgunda alikiri kufurahishwa na uwezo wa wachezaji wake katika mchezo huo baada ya mechi iliyopita kulazimishwa suluhu nyumbani dhidi ya Ndanda FC.

"Wachezaji wametumia vizuri maelekezo niliyowapa, wameyafanyi kazi na tumepata ushindi japo kuna makosa kidogo ambayo nimeyaona nitayafanyia kazi zaidi," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema mchezo uliopita ulikuwa na ushindani kutokana na kila timu ilikuwa inahitaji ushindi, lakini juzi wachezaji walipambana na kufuata maelekezo yake vizuri.

"Mchezo ulikuwa mgumu, timu zote zilionyesha uwezo, lakini mwisho wa siku bahati ikaangukia kwetu," alisema.

Alisema kwa sasa wanajiandaa na mchezo ujao dhidi ya timu ya Namungo FC ambao utachezwa Machi 14, mwaka huu mkoani humo.

# Michezo

Alhamisi Machi 12, 2020

Nipashe




## Corona yawazuia Pep, Arteta, EPL kuendelea

UKURASA 30

KAKA HAT-TRICK...



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, katika harakati za kucheka na nyavu dhidi ya beki wa Singida United, Hajji Mwinyi (chini), kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. Simba ilishinda 8-0 huku Kagere akipiga hat-trick. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KAGERE NA REKODI YA GHARIKA SIMBA

## ●●● Hat-trick ya sita Ligi Kuu yatingishwa, Singida United yafungua ukurasa mchafu...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wameweka rekodi ya gharika ya kucheka na nyavu baada ya jana kushuhudiwa idadi kubwa ya mabao kwa timu kushinda au kufungwa kwenye ligi hiyo kufuatia kuichakaza Singida United 8-0 katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Uhuru.

**Mbali na Simba kutakata kwa ushindi huo wa rekodi msimu huu, pia mshambuliaji wake, Meddie Kagere alifunga mabao manne hivyo kuendelea kung'ang'ania kileleni katika orodha ya wafungaji akiwa na jumla ya mabao 19 hadi sasa.**

Simba imepata idadi hiyo kubwa ya mabao, ikionekana ni kama hasira ya kupoteza mechi iliyopita dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga kwenye mechi iliyopigwa Machi 8, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, ilipochapwa bao 1-0.

Dakika ya kwanza tu, Kagere alifunga bao la kwanza, na wakati wachezaji wa Singida wakitafakari nini kimetokea, Mkongomani Deo Kanda alipachika la pili lililotokana na kazi nzuri iliyofanywa na John Bocco kumpenyezea pasi safi, akiwa katikati ya walinzi na kuujaza nyavuni.

Kanda tena alifunga bao la tatu dakika ya 18, alipowalamba chenga mabeki kadhaa wa Singida United pamoja na kipa wao raia wa Malawi, Owen Chaima, kabla ya kuukwamisha wavuni.

Bocco alifunga bao la nne, akiunganisha krosi maridadi kutoka kwa Shomari Kapombe dakika moja tu baada ya bao la tatu.

Kagere alifunga bao la tano na la pili kwake katika mchezo huo katika dakika ya 25 baada ya kutokea piga nikupige ya Luis Miqussone na walinzi wa Singida, mpira ukamkuta mfungaji akauzamisha nyavuni, na ni yeye aliyeingia kwenye kitabu cha wachezaji waliofunga 'hat-trick' msimu huu, alipopachika bao la sita na la tatu kwake katika dakika ya 41.

Dakika za mwanzo tu za kipindi cha pili, mchezaji wa Singida United Haruna Moshi 'Boban' alizawadiwa kadi nyekundu baada ya kumpiga kiwiko kipa wa Simba, Aishi Manula.

Mchezaji aliyeingia kipindi cha pili, Sharaf Shiboub alifunga bao la saba dakika ya 59, huku Kagere aliyeanzisha karamu hiyo ya mabao, akihitimisha kwa kufunga bao la nane na la nne kwake katika mchezo huo.

'Hat-trick' hiyo inakuwa ni ya sita kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, huku wachezaji wengine waliofanya hivyo ni Ditram Nchimbi wakati huo akiichezea Polisi Tanzania, Daruweshi Saliboko wa Lipuli, Obrey Chirwa wa Azam, Kelvin Sabato wa Kagera Sugar na David Richard wa Alliance.

Matokeo hayo pia yameendeleza ukurasa mchafu wa rekodi mbaya kwa Singida United mbele ya Simba kwani mara sita zilipokutana, imefungwa zote, huku ikiwa haijafunga hata bao moja, tangu ilipopanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 20178/18.

Ni matokeo yanayoifanya Simba kufikisha pointi 71, ikiwa imefunga mabao 63, ikiruhusu nyavu zake kutikiswa mara 15 kwenye mechi 28 ilizocheza na kuendelea kujikita kileleni ikiusaka ubingwa kwa msimu wa tatu mfululizo.

Hali ni mbaya kwa upande wa Singida United kwani ni miujiza tu itakayoifanya kubakia Ligi Kuu msimu ujao, kutokana na kuendelea kuburuza mkia ikiwa na pointi zake 12 tu kwa mechi 28 ilizocheza, ikishinda mbili tu, sare sita, lakini ikipoteza mechi 20, mabao 14 ya kufunga na 48 ya kufungwa.

Nayo timu ya Tanzania Prisons, ikiwa kwenye uwanja wake wa Sokoine jijini Mbeya jana iliichapa Alliance FC bao 1-0, huku Polisi Tanzania ikilazimishwa suluhu ya bila kufungana dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

# 'Mbuyu' Cecafa wang'oka rasmi

**Na Saada Akida**

HATIMAYE 'mbuyu' umeanguka! Hivyo ndivyo unavyoweza kusema baada ya Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), kumtangaza mrithi wa nafasi ya Katibu Mkuu, Nicholas Musonye.

Rais wa Cecafa, Wallace Karia ndiye aliweka wazi suala hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akimtangaza Mtendaji Mkuu wa baraza hilo, Auka Gecheo ambaye anachukuwa rasmi nafasi ya Musonye ambaye amedumu katika baraza hilo kwa zaidi ya miaka 20.

Karia ambaye ni Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), alisema walipokea barua Machi 9, mwaka huu kutoka Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), likimwidhinisha Gecheo kuwa Mtendaji Mkuu wa Cecafa.

Alisema baada ya Musonye kumaliza muda wake katika nafasi hiyo, walipeleka majina CAF kwa mujibu wa katiba yao kama inavyoelekeza kuwa Mtendaji Mkuu wa Cecafa anapaswa kuidhinishwa na shirikisho hilo.

"Makao Makuu ya Cecafa yapo Kenya, hivyo kuteuliwa kwa Auka, tumefuata katiba yetu inavyotaka na mtendaji anatakiwa kuishi katika makao makuu hayo," alisema Karia.

Alisema mtendaji huyo atakuwa akisaini mkataba wa miaka miwili na kila anapomaliza huongezwa.

Naye Gecheo alisema amefurahi kupata nafasi hiyo na atahakikisha anashirikiana vizuri na viongozi wake ili kufikia malengo.

"Matumaini yangu ni kufanya yale Musonye alikuwa akiyafanya kwa kipindi chote cha miaka 21, kuhakikisha soka linakua juu kwa Ukanda wa Cecafa," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >